Kikao cha Kumi – Tarehe 10 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Ripoti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Hati mezani ya Ripoti ya Wzara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Maryam Thani Juma: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii, naomba kuweza mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Yussuf Hasssan Idd: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, naomba kuweka hati mezani Hotuba ya maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 80

Wizi wa Mifuko ya Saruji katika Ujenzi Wa Uwanja wa Mao Tse Tung

Mhe. Jaku Hashim Ayoub– Aliuliza**:**

Mwishoni mwa mwezi wa Julai, 2017 kumeripotiwa wizi wa aibu wa mifuko ya saruji katika eneo la ujenzi wa Uwanja wa Mao Tse Tung ambapo wahusika inadaiwa ni walinzi wa moja ya Vikosi vya Idara Maalum za SMZ.

Je, Walinzi wa aina gani walioshiriki wizi huo na hatua gani zimechukuliwa dhidi yao ili kudhibiti aibu hiyo isitokee tena.

Mhe. Waziri wa Nchi OR Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Askari wa KVZ kwa kushirikiana na raia wasiokuwa waaminifu wanatuhumiwa katika wizi wa saruji katika Uwanja wa Mao Tse Tung.

Hata hivyo, wakati wa vyombo vinavyohusika vikiendelea na uchunguzi wa tukio hilo na itakapothibitika watuhumiwa watafikishwa Mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo tu lenye kifungu a na b.

(a) Kuna msemo unasema "abebwae hujikaza" nilisema jana hapa hata masaa 24 hayajifika, kama kuna watu wa kuwashukuru sisi Zanzibar kama hakuna watu wa China basi hatujafanyia haki wametusaidia kwa kila sekta elimu, afya, barabara mambo mengi tu. Lakini kitendo kile cha aibu na kutia fedheha Zanzibar kama serikali au wizara mmechukua hatua gani kuwapa maneno mazuri wanaojenga uwanja ule, ukizingatia askari wale wanalipwa ni kitu cha aibu na kama hamjakaa ni lini mtakaa na wajenzi wa uwanja ule kuwaeleza angalau maneno mazuri. Ni lini mtakaa kuwaeleza maneo hayo ni kitu cha aibu.

(b) Wakandarasi wale wanaojenga uwanja ule hebu tueleze shilingi ngapi wanaolipwa askari wale wa KVZ na hichi ilikuwa si mara ya kwanza ulikuwa mtego maalum unaotegwa. Mimi ni Mjumbe wa kamati ile ikiongozwa na Mhe. Ali Suleiman Ali. Ule mtego ulikuwa ni maalum, mifuko katika 320 ilitaka kuibia iko mpaka leo Madema. Hebu fanya utaratibu.....

Mhe. Spika: Swali lako Mheshimiwa, swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni lini saruji ile itakabidhiwa baada ya kielelezo ili uwanja ule upate kumalizwa kwa haraka.

Mhe. Waziri wa Nchi OR Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Kwanza Mhe. Spika, nataka nimfahamishe Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba baada tu ya tukio lile la aibu kutokea serikali kupitia mamlaka ya nidhamu ya KVZ tuliamua kuchukua hatua ya kuwaweka ndani askari ambao wanahusika na tukio lile na kwa taarifa yako walikaa ndani kwa muda wa miezi miwili na halafu tukachukua hatua ya kuwasimamisha kazi mpaka hapo suala la kisheria litakapokamilika. Kwa hivyo, sisi serikali wala hatukufurahishwa na jambo lile na ndio maana tumechukuwa hatua za haraka na tunaacha vyombo vinavyohusika viweze kufanya kazi yake watuhumiwa

watakapofikishwa Mahakamani kwa upande wetu kama KVZ ikiwawatakuwa Mahakamani watahukumiwa kwa kiasi ya miezi 6 maana yake *automatic* watakuwa hawana kazi na hatuwezi kuwarejesha kazini kwa sheria zetu.

Lakini iwapo kama kesi itakwenda vyenginevyo tutawafungulia mashtaka mengine ya kijeshi ili kuwapa adhabu zinazostahiki.

(b) Mhe. Spika, kweli sisi ni marafiki wa damu kabisa na ndugu zetu wa China na tutaendelea kuthamini juhudi na michango wanayotupatia wezetu au ndugu zetu wa China ili kuhakikisha kwamba urafiki na misaada hii na mikopo saa nyengine ili iweze kwenda kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nam. 103

Mgawanyo wa Mapato yanayotokana na usimamizi wa Soko la Mwanakwerekwe na Soko la Mombasa

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza**:**

Soko la Mwanakwerekwe na soko la Mboga Mboga Mombasa yanasimamiwa na Manispaa ya Mjini lakini masoko hayo yapo Manispaa ya Magharibi "B"

Kwa kuwa Masoko hayo yapo Magharibi "B", lakini yanasimamiwa na Manispaa ya Mjini, Je, Wizara imetazama vipi juu ya mgawano wa mapato.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo swali lake Nam. 103 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kuwa soko la Mwanakwerekwe na lile la mboga liliopo Mombasa yanaendelea kusimamiwa na Baraza la Manispaa la Mjini pamoja na kwamba kiutawala masoko hayo yapo katika Manispaa ya Magharibi B. Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka zote mbili zinafaidika na uwepo wa masoko hayo kimapato, Mabaraza hayo mawili yamekubaliana namna bora ya ukusanyaji wa mapato katika masoko hayo.

Mhe. Spika, chini ya makubaliano hayo, Baraza la Manispaa – Mjini ambalo ndio mmiliki wa masoko hayo kisheria linakusanya mapato yatokanayo na ada ya usafi wa ndani ya soko na kodi ya maduka yaliomo ndani ya masoko hayo. Baraza la Manispaa la Magharibi “B” kwa upande wake linakusanya mapato yatokanayo na shughuli zinazoendeshwa nje ya soko zikiwemo za maegesho ya vyombo vya moto.

Utaratibu huu unaendelea kuheshimiwa na Mabaraza yote mawili kwa kuwa unaonekana kunufaisha pande zote mbili. Hata hivyo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inaandaa Agizo la Kiutawala *Administrative Order*

litakalotoa uamuzi kuhusu mgawanyo wa masoko hayo kwa Mabaraza ya Manispaa husika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali ya nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jibu lake zuri ambalo nahakikisha kwamba wenyewe wanaohusika wamesikia. Lakini kwa kuwa mimi naishi katika Magharibi "B" na matatizo ya usafi wa maeneo yetu mengi yanatanzwa kutokana na ukosefu wa Fedha.

Je, kwa kuwa wenzetu wa Manispaa ya Mjini wana uwezo kwa asilimia 80 au 90 na ukija kwetu Magharibi "B" Manispaa yetu ina asilimia kama 15 au 20. Mhe. Waziri ana mpango gani wa kushauri katika Manispaa mbili hizi wakatuongezea nguvu ya magari ya kusombea takataka katika maeneo yetu mbali mbali hasa maeneo ya Taveta pahala pachafu na panahatarisha usalama wakati wa mvua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kama nilivyosema ofisi yangu inaandaa utaratibu wa agizo la kiutawala kwa ajili ya mgawanyo wa mali. Lakini suala lilikluwa linahusu masoko. Ninachotaka kumhakikishia Mheshimiwa Mjumbe mali ni pamoja na magari na mambo mengine. Kwa hiyo, utakapokuwa tayari hiyo agizo la kiutawala limekamilika nadhani suala lake litakuwa limetekelezeka kwa kuwapatia wenzetu wa Manispaa ya Magharibi "A" na "B" kuwapatia magari na vifaa vyengine vya kusafishia ili waweze kuetekeleza majukumu yao vizuri.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii naomba nimuliize Mhe. Waziri.

Masoko ya Mwanakwerekwe pamoja na Mombasa yako chini ya usimamizi wa Manispaa ya Mjini na kwa sababu fedha zeto zinazokusanywa zinaingia kwenye mfuko mkuu wa serikali.

(a) Je. haoni masoko haya wakakabidhiwa Manispaa ya Magharibi "B" ili wakaweza kuyaendesha.

(b) Je, ni lini watu wa Manispaa ya Magharibi "B" makusanyo yao wanakusanya nje ya soko ni lini wataweza kuruhusiwa na ndani ya soko wakaweza kukusanya Manispaa ya Magharibi "B" ili wakapata kufaidika na matunda haya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Masoud Abrahman Masoud swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza kama jibu langu mama nilivyosema kwamba sasa hivi tuko katika maandalizi na matayarisho ya mwisho kwa ajili ya kutoa agizo la kiutawala kuweza kuyagawanya masoko haya kwa Manispaa ya Magharibi "B" na Mjini. Hivyo, tayari serikali imeshafanya maamuzi ya kufanya hilo jambo. Lakini utaratibu uliowekwa nadhani Mhe. Masoud Abrahman anauelewa toka yeye mwenyewe akiwa Mwenyekiti wa Halmashauri. Kwa sababu masoko yalikuwa yanamilikiwa kihalali na Manispaa ya Mjini ijapokuwa yapo katika mipaka au maeneo ya Magharibi walikubaliana kimsingi kwamba waweze kukusanya mapato ya nje yawe ni ya Manispaa ya Magharibi kwa wakati ule na sasa yamerithiwa na Magharibi "B".

Lakini kwa ndani yaendelee kukusanywa na wenyewe watu wa Manispaa ya Mjini. Hivyo utaratibu kama nilivyosema mwanzo utaratibu huu utakapokamilika mambo yote haya yatakuwa yamepata ufumbuzi.

Hata hivyo, fedha zinazokusanywa na Manispaa zote haziingii katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Ni fedha ambazo wanabaki nazo wenyewe kwa ajili ya kufanyia kazi ya kutoa huduma bora kwa wananchi na haziendi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Isipokuwa serikali inaendelea kutoa ruzuku kwa vyombo hivi kwa ajili ya kuongeza ufanisi mzuri zaidi ili vyombo hivi viweze kutoa huduma nzuri. Ahsante sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri na nimpongeze wizara yake kutengeneza masoko katika mji wetu.

Mhe. Waziri kwa kuwa kuna agizo la Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohd Shein la kutokutaka kuona ng'ombe wakizaa ndani ya miji.

(a) Kwa nini soko lako la Mava Mbarouk pale Michakaeni Chake Chake linafanywa mnada wa ng'ombe ambao ni sehemu ya mji.

(b) Je, kwa nini unashindwa kuchukua hatua ya kumuwajibisha yule ambaye bado hajataka kufuata agizo la Mhe. Rais. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kama nilivyokuwa natoa maelezo ya kila siku kuhusu jambo hili la ng'ombe mijini bado msimamo na maamuzi ya serikali yapo pale pale kwamba ng'ombe hawaruhusiki kuingia katika maeneo ya mji au kuzurura katika maeneo ya mjini. Taratibu na sheria ziko wazi sasa kama kuna mtumishi ambaye hawajibika na anaendelea kufanyakazi kwa mazoea basi taratibu za hatua za kinidhamu zitaendelea ili kuona uwajibikaji wake huo kama unafaa kwa wakati huu au haufai kwa wakati huu. Ahsante sana.

Msikiti mpya Uliojengwa kwa Msaada wa Serikali ya Oman

Mhe. Jaku Hashim Ayoub– Aliuliza**:**

Serikali ya Watu wa Oman inastahili pongezi kwa mashirikiano yake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika sekta mbali mbali za maendeleo ambapo hivi karibuni Oman imesaidia kujengwa kwa Msikiti Mkubwa eneo la Mazizini karibu na Chuo cha Kiislamu ambao umeshamalizika.

(a) Je, ni lini Msikiti huo utafunguliwa baada kukamilika ujenzi wake na sababu gani zimepelekea Msikiti huo kuchelewa kufunguliwa.

(b) Je, Msikiti huo unategemewa kuitwa jina gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 75 lenye vipengele (a) na **(**b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Serikali ya Zanzibar inaishukuru Serikali ya Oman kwa kutujengea Msikiti mkubwa na wa kileo. Msikiti huo tayari umeshafunguliwa tarehe 22/09/2017. Msikiti huu ulichelewa kufunguliwa kutokana na sababu za kiutawala na ikiwemo makabidhiano.

(b) Mhe. Spika, Msikiti huo unaitwa Jaamiu Zinjibaar. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali madogo sana ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kuna taarifa au harufu kwamba kuchelewa kufunguliwa kwa Msikiti ule kulikuwa kuna mvutano, kati ya kutia jina Msikiti ule na kuendesha Msikiti ule kwa gharama.

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri taarifa hizi unaweza kutuambia ni kweli au si kweli.

(b) Kama ni kweli je, ni nani msimamizi wa Msikiti ule, ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, au Serikali ya Oman. Tusije tukafika mahali tukajakushuhudia kama Msikiti wa Mwembeshauri. Ulijengwa Msikiti mkubwa na hali yake tunauona hivi sasa.

Lakini sisi wengi humu ndani ni Waislamu, kuna mambo matatu yakishakufika kama ni Muislamu hayataki kuwekwa. Maiti ikishakufika inataka ikazikwe la kwanza. Mtu akishakufika umri wa kuolewa au kuowa basi aozeshwe, la tatu swala haicheleweshwi.

Je, kucheleweshwa kwa kufunguliwa Msikiti ule hamuoni mmemnyima fadhila aliyejenga Msikiti ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba.....

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tusikilizane. Tunaomba utulivu kidogo, msikilizeni Mhe. Naibu Waziri akitoa majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama (a), sababu ambazo zilizosababisha Msikiti huo kuchelewa ni sababu za kiutawala ikiwemo pia masuala ya makabidhiano.

Mhe. Spika, sio suala la kwamba kulikuwa kuna mvutano, Msikiti kupewa jina na nini hapana. Ni sababu za kiutawala na naamini Mhe. Jaku Hashim utakubaliana na hilo.

Pia uliuliza katika swali lako (a) kuwa ni nani mmiliki wa Msikiti huo, kwa sababu unahofia kwamba isijekuwa hapo mbele tukajakuvutana Mmiliki huyu au huyu. Mhe. Spika, kwa taarifa tu mmiliki wa Msikiti huu ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hapana Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Dogo tu.

Mhe. Spika: Hapana, hapana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwanza niishukuru Serikali ya Oman kwa kuweza kutujengea Msikiti mkubwa kama huu kwa Waislam wa nchi mbali mbali wanaweza kuutumia. Lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, wakati wa ufunguzi wa Msikiti huu ilielezwa kwamba utakuwa unatoa mafunzo mbali mbali yatapatikana pale katika Msikiti ule. Je, mafunzo hayo ni ya aina gani na lini yataanza kutolewa mafunzo katika Msikiti huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, ni kweli mafunzo ya aina mbali mbali yatatolewa pale katika Msikiti ule, yakiwemo mafunzo ya dini ya Kiislamu. Nashukuru.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, napenda kumuuliza swali moja dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo. Je, ni kiasi gani cha gharama kilichotumika kuujenga Msikiti huo, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Yussuf Hassan swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, gharama ya Msikiti ule ni shilingi bilioni 17, bilioni 3 miongoni mwa hizo ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia msamaha wa kodi. Ahsante.

Nam. 40

Uwiano wa Kufunga Skuli na Vyuo vya Qur-ani

Mhe. Suleiman Sarhan Said - Aliuliza:-

Nashukuru Mhe. Spika, na mimi awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema mwenye kurehemu, aliyeumba Mbingu na ardhi na vilivyomo vyote na tumtakie heri na Mtume wetu Mohammad (SAW). Mhe. Spika, naomba swali langu namba 40 lijibiwe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kumekuwa na tatizo la kukosekana kwa uwiano katika tarehe za ufungaji na skuli na vyuo vya Qur-ani na hivyo kusababisha usumbufu kwa wazazi na wanafunzi wengine.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na tarehe zinazowiana katika ufungaji wa skuli na vyuo vya Qur-an ili kupunguza usumbufu unaojitokeza.

(b) Je, Serikali haioni baadhi ya wakati wazazi huwa wanasumbuka kwa kutokupanga likizo za mapumziko.

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukaa pamoja baina ya skuli za Serikali na Skuli za binafsi (*Private*) na Vyuo vya Qur-ani ili kuweka msimamo mmoja wa kufunga na kufungua.

Mhe. Naibu Waziri wa Eimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu inajua kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwapatia mapumziko watoto kulingana na mgawanyo wa siku zao za masomo. Kwa kuzingatia hilo, wizara imeanza na itaendelea na juhudi za kukutana na walimu wa vyuo vya Kur-an na Ofisi ya Mufti ambao ndio wanaovisajili vyuo vyote nchini, ili kulizungumzia suala hili na kupata ufumbuzi stahiki ili kuwaondolea usumbufu watoto pamoja na wazazi au walezi.

Mhe. Spika, **w**izara yangu kwa kawaida inazungumza na wadau hawa wote katika kuona watoto na wazazi tunawasaidia, hasa katika suala zima la kufungwa na kufunguliwa kwa skuli kupitia vikao na mikutano mbali mbali. Kwa kuliona hili katika kupanga ratiba za kufunga na kufungua skuli mwaka 2017, wizara pia imezishirikisha kikamilifu skuli za binafsi katika kupanga ratiba hii ili iwe ya wote. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini kwa kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ndio wenye majukumu ya elimu katika Zanzibar. Lakini suala la vyuo vya Qur-ani, inaonesha kwamba havina *registration* maalum na wala walimu wake hawalipwi na serikali.

(a) Je, serikali inawezaje kuviingilia vyuo kikatiba na kuweza kuvipa amri?
Serikali ilipiga marufuku baadhi ya *tuition* zilizokuwa hazina usalama, au hazina vituo maalum, lakini bado suala hili ni kitendawili.

(b) Je, serikali imechukua hatua gani katika suala hili la *tuition* zilizokuwa hazina uhakika?

Mhe. Naibu Waziri wa Eimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye sehemu mbili kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi lazima afahamu kwamba vyuo vya Qur-ani navyo pia vinafanyakazi zake kwa mujibu wa taratibu za kiserikali na kwa maana hiyo vinapaswa kusajiliwa na Ofisi ya Mufti. Ofisi ya Mufti ndiyo inayovisajili vyuo hivi.

Kwa upande mwengine ni kwamba katika mfumo wa elimu, tuna mifumo mitatu mikubwa. Kuna mfumo ambao tunauita *formal*, kuna *informal* na *nonformal*. Sasa vyuo hivi vya Qur-ani vinaingia katika mfumo wa *informal* na kwa maana hiyo vina namna fulani ya kuendesha shughuli zake, lakini pia hii haiondoi serikali kuingilia katika suala zima la elimu ya taifa, tunaita *National Education*. Kwa hivyo, serikali ina mkono wake katika masuala haya.

Mhe. Spika, kwa upande wa *tuition*. Suala hili tumelizungumza kwa urefu, ni kwamba kwa sasa tunajaribu kuzichunguza kwa makini ili kujua faida yake na hasara zake. Baada ya uchunguzi kukamilika serikali itatoa kauli juu ya *tuition*.

Mhe. Spika, lakini hata hivyo kwa sasa ni kwamba tunazifuatilia kwa karibu, ili kuona nani anasomesha, wakati gani na wanalipana kiasi gani na mambo mengineyo, tena haya tunayafuata kwa karibu ili kuona kwamba kila mtu anastahiki kupata haki hiyo. Kwa maana hiyo tumewaeleza walimu kuwa wakati wanapokuwa na madarasa ya *tuition*, wahakikishe kwamba hawamtengi mwanafunzi hata mmoja, aliyelipa asiyelipa ni lazima ashirikishwe. Huo ndio msimamo juu ya masuala haya, lakini niseme tu kwamba uchunguzi wa kina tunaufuata. Hata sisi tunaanza kushughulika kidogo na utaratibu huu. Ninaposema sisi kama serikali ni kwamba tunalichunguza kwa makini. Ahsante sana.

Nam. 49

Upungufu wa Vyoo katika Skuli ya Msingi Jadida, Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Kwa kuwa skuli ya msingi Jadida iliopo katikati ya mji na yenye wanafunzi wasiopungua 1000 ina vyoo (7) ambavyo hutumika kwa wanafunzi wa kike na kiume jambo ambalo ni tatizo kubwa skulini hapo.

(a) Je, Wizara hailijui tatizo hili la upungufu wa vyoo kwa skuli ya Jadida.

(b) Kama inalifahamu, hatua gani za dharura ambazo Wizara imezichukuwa ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa vyoo kwa skuli hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye vipengele (a) na (b) kama hivi ifuatavyo: -

(a) Wizara inalielewa tatizo hilo la upungufu wa vyoo kwa skuli ya msingi ya Jadida. Skuli ya Jadida ina wanafunzi 1917 na ilikuwa na vyoo saba kama ilivyoelezwa. Hii inaonesha upungufu mkubwa wa vyoo kwa wanafunzi.

(b) Kwa kuelewa ukubwa wa tatizo la upungufu wa vyoo katika Skuli ya msingi ya Jadida, wizara imechukua juhudi ya kujenga vyoo vipya 14 ambapo vyoo saba vitatumika na wanafunzi wanawake na vyoo saba vitatumiwa na wanafunzi wanaume. Hii imepunguza changamoto ya vyoo, na hata hivyo wizara inaendelea na jitihada za kujenga vyoo zaidi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa kumekuwa na tabia tunapojenga vyoo huwa tunawaangalia zaidi wanafunzi. Wanafunzi sio wanaokaa pale skuli peke yao, na walimu wao huwa wanahitaji hizi huduma. Sasa nataka nijuwe katika ujenzi wa vyoo mlioufanya kwenye skuli ya Jadida.

Je, kuna vyoo ambavyo vimejengwa kwa ajili ya walimu na kama vimejengwa ni vingapi kwa ajili ya walimu wanaume na vingapi vimewekwa kwa ajili ya walimu wanawake. Pamoja na kutoa pongezi kwa wizara kwa kujenga hivyo vyoo, lakini nilitaka nijuwe swali langu hili ili roho yangu iridhike. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, katika ujenzi wa vyoo ni wajibu wa skuli kuvigawa vyoo hivyo kwa mujibu wa mahitaji waliyonayo, haina maana kusema vyoo vya wanafunzi vina sifa maalum ambavyo haviwezi kuwa vya walimu.

Kwa hivyo, inawezekana skuli katika vyoo hivyo 14, viwili vinaweza pia vikatengwa kwa walimu, kimoja kwa walimu wa kike na kimoja walimu wanaume, huo ndio

utaratibu uliopo. Hakuna utaratibu maalum wa kusema hivi leo tunajenga vyoo vya walimu tu, hapana ni vyoo vya kawaida katika skuli, halafu tunavigawa kwa mujibu wa mahitaji ya skuli. Ahsante.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Labda niulize tu kwa kuwa tumeona katika ujenzi wetu wa kujenga barabara zetu tunakuwa tuna kampuni yetu wenyewe ya UUB ambayo inasimamia kujenga barabara.

Mhe. Spika, napenda niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa upande wa wizara na serikali kwa jumla, tumekuwa tunatumia fedha nyingi sana katika ujenzi, lakini mahitaji kwenye ujenzi hasa katika maskuli yetu pamoja na vyoo yamekuwa yanaongezeka.

Je, wizara haioni kwa kushirikiana na Shirika la Nyumba kuanzisha utaratibu wa kuwa na kampuni ndogo ambayo itakuwa inapeleka kasi ya ujenzi wa vyoo na hasa katika kuboresha maskuli yetu, ili kupunguza gharama na kuleta ufanisi kwa pamoja ndani ya serikali, maskuli yetu pamoja na maeneo tofauti. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, mara nyingi ujenzi huu wa vyoo katika skuli, tunaweza kusema ni miradi midogo, kwa maana hiyo yanajengwa zaidi katika misingi ya skuli. Pengine vyoo 14, 16,17 lakini pia vinajengwa wakati mwengine na nguvu za wananchi. Kwa hivyo, kwa maana hiyo hatuoni kwamba kuna haja kwa sasa.

Mhe. Spika, pale ambapo kutakuwa na miradi mikubwa ya fedha nyingi, nadhani itakuwepo haja ya kuzungumza na Shirika la Nyumba na wahisani wengine. Lakini hata hivyo kuna utaratibu mwengine wa kiserikali, kwamba katika miradi mikubwa inatangazwa *tender* na kwa maana hiyo inawezekana kwamba kila mwenye uwezo ataomba *tender* hiyo, likiwemo Shirika la Nyumba, ahsante sana.

Nam. 115

Kutatuliwa Changamoto za Biashara Tanzania Bara na Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hivi karibuni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilifanya mazungumzo na Serikali ya Kenya kutatuwa changamoto za kibiashara baina ya nchi hizo na mazungumzo hayo yamekuwa ya mafanikio kwa kuwa changamoto kubwa za kupitisha bidhaa baina ya Kenya na Tanzania zimetatuliwa. Kwa upande wa Zanzibar na Tanzania bara kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto za wafanyabiashara wa Zanzibar kufanya biashara bila ya bughdha Tanzania Bara, licha ya jambo hilo kuwa la muda mrefu bado changamoto hizo zipo.

Je, kwanini Tanzania Bara na Kenya wameweza kumaliza changamoto hizo za biashara lakini kwa upande wa Zanzibar na Bara changamoto hizo zinaendelea kwa miaka mingi wakati nchi zetu hizi zina uhusiano wa kindugu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 115 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba kueleza kidogo kuhusu vikwazo vya biashara vilivyotokea baina ya Kenya na Tanzania kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, Kenya iliiwekea vikwazo Tanzania katika bidhaa ya unga na bidhaa ya gesi na hivyo kusababisha usumbufu wa biashara kwa upande wa Tanzania. Tanzania nayo iliiwekea vikwazo Kenya katika bidhaa za maziwa na sigara kuingia ndani ya soko la Tanzania. Baada ya jambo hili kupelekwa ngazi za juu, viongozi wakuu wa nchi hizi mbili wamekubaliana kuondolewa kwa vikwazo baina ya nchi hizo mbili na makubaliano hayo yalifikiwa katika mkutano uliofanyika tarehe 8 Septemba 2017.

Kwa upande wa vikwazo vya kibiashara baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, wizara yangu inaendelea kufanya mazungumzo na watendaji wa taasisi za Bara ili kuondosha vikwazo vya kibiashara baina ya pande hizi mbili. Hivi karibuni wizara yangu ilikuwa na kikao na Wizara ya Viwanda na Uwekezaji ya Tanzania, ili kuangalia matatizo yanayowakabili wafanyabiashara.

Aidha, kupitia Kamati ya Kusimamia Masuala ya Vikwazo vya Biashara Visivyokuwa vya Kiushuru, Kamati ndogo imeundwa ili kufuatilia changamoto hizi ili hatimae kuendelea kuzitafutia ufumbuzi muafaka.

Vile vile, suala la vikwazo vya kibiashara baina yetu litazungumzwa kwenye vikao vya mashirikiano baina ya SMT na SMZ vinavyofuata.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa na kwa huzuni kubwa hili swali halikujibika. Halikujibika kabisa, lakini hichi nilichokiandika ni Kiswahili, liangalie mwenyewe Mhe. Spika, kwa uzito na Waheshimiwa Wajumbe nisaidieni.

Mhe. Spika, nilichotaka mimi ni kuhusu Tanzania, nini kero za wafanyabiashara kwa Zanzibar litamalizika. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alikuwa Waziri wa Fedha kwa kipindi hicho, haya mateso yaliyokuwa yakiendelea kabisa hakunitajia. Kukaa na wenzetu tarehe 08 Septemba limepata utatuzi, hili swali halikujibika hata sijui niulize nini. Nilichouliza mimi changamoto hizi kero.

Mhe. Spika, leo mfanyabiashara kachukua mivao ya kanga mitatu kafika pale kanyang'anywa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, uliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hapa swali la nyongeza Mhe. Spika, labda nipeleke tu, lakini ukweli namuonea huruma Mhe. Waziri, yeye alikuwa ni Waziri wa Fedha. Utakubaliana na mimi Mhe. Waziri ndugu zetu hawana nia nzuri na Zanzibar. Mifano ipo hai tulitaka kukatiwa umeme sisi, kama sio uwezo wetu....

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe usituhutubie *please*, uliza swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, sina nia mbaya na Muungano, Muungano wetu huu tunauhitaji. Mimi mmoja ninauhitaji Muungano huu, isije ikafika pahali nikaja nikahukumiwa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, sio suala la nia mbaya, hapa sio pahala pake pa kutuhutubia, uliza swali la nyongeza ukae.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hapa hapauliziki swali la nyongeza, swali halijajibiwa, nitauliza vipi swali la nyongeza.

Mhe. Spika: Basi naomba ukae. Mhe. Simai Mohamed Said swali la nyongeza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Lakini wacha niendelee hivyo hivyo mheshimiwa, nitaendelea hivyo hivyo.

Mhe. Spika: Mhe. Jaku.....

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi niulize swalia dogo tu la nyongeza pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa.

Mimi suala langu ni hivi Mhe. Spika, kwa kuwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba tumekuwa katika harakati kwa miaka mingi sana tukitegemea biashara kihistoria.

a) Je, Wizara hii inatumia utaratibu gani wa kukuza biashara baina ya kisiwa cha Unguja pamoja na udugu uliokuwepo kwa upande wa Kenya hasa kwa kupitia eneo la Mombasa.

b) Tumekuwa tuna Ofisi yetu ndogo kwa upande wa Dar es Salaam ambayo inaratibu masuala yote ya Zanzibar kwa upande wa Bara, Je, Ofisi ya Zanzibar iliyokuwepo hapo Dar es Salaam imetumia bidii gani kwa kushirikiana na Wizara yake ili kuhakikisha hizi kero ndogo ndogo hasa kwa upande wa bandari juu ya wafanyabiashara wanaoteseka kila kukicha wakati wanakuwa na mizigo yao midogo wanapofika Dar es Salaam, hasa katika boti zetu za kawaida za usafiri wa baharini.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kujibu swali lake la nyongeza Mheshimiwa Simai Mohammed Said Mwakilishi kama ifuatavyo.

Naomba nitoe ufafanuzi kwa sababu mazungumzo yaliyozungumzwa yameingizwa masuala ya kisiasa na mengine yamepotoshwa, Mhe. Spika, lazima tukiri kwamba Tanzania ni nchi moja na suala la biashara kila upande tunafanya biashara zetu kwa

mujibu wa taratibu na sheria tulizokuwa nazo. Lakini Umoja wa Mataifa limekuwa limeweka neno kwamba vikwazo visivyokuwa vya kiushuru au vikwazo vya biashara wameweka kwa maana yao kwamba. Kwenye biashara kunatokea matatizo ya kutokufahamiana na hasa unapokuwa unashughulikia biashara ukiwa na vyombo vingi ambavyo vinashughulikia kusimamia kuratibu suala zima la biashara.

Mhe. Spika, ningeomba kufafanua kuweka tofauti baina ya Tanzania na Kenya. Tanzania na Kenya ni nchi mbili tofauti na utaratibu wao wa kuzungumza lazima upitie katika utaratibu tofauti, Zanzibar na Serikali ya Muungano taratibu zetu kama nilivyozieleza lazima tupitie katika utaratibu ambao tumejiwekea wenyewe kuzungumza Mawizara, watendaji mpaka tukafika ngazi ya juu ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na jambo hili ambalo tunalifanya. Kwa hivyo mimi sioni kama kuna tatizo kubwa kuna ugumu au kuna chuki baina ya Serikali hizi mbili, ni taratibu za kibiashara zinatokea katika nchi mbali mbali.

Lakini ni kweli wafanyabiashara wa Zanzibar wengi wao wanapata vikwazo ambavyo vinawasababisha bidhaa zao zisiweze kwenda vizuri kule upande wa bara, na hiyo si kwamba Serikali inawapa maagizo watendaji kule bara hapana ni maofisa wanaohusika na watu mbali mbali wanaohusika katika utaratibu mzima ndio hao wanaosababisha wakati mwengine kutofahamu vizuri sheria na Kanuni zilivyo za kibiashara.

Kuhusu kutumia Pemba au Unguja kupitia Mombasa ni wazo zuri kwa kweli kwa sababu kweli ukiangalia Pemba hasa Kaskazini Pemba wao wako karibu sana na Mombasa, karibu sana na Tanga tulifanya utafiti mdogo tu ikaonekana kwamba biashara nyingi wanazofanya wenzetu walioko Pemba wanafanya kupitia Mombasa na Tanga, suala hili tunalifanyia kazi kuona kiasi gani tutaitumia bandari ya Tanga na vile vile iwe bandari ya Tanga kupitia pale kwenda Mombasa kwa bidhaa zetu ambazo zaidi zinazalishwa Pemba na zile ambazo zinatoka Unguja kwa ajili ya kuongeza biashara.

Kuhusu ofisi yetu ya uratibu kuwapa kazi ya kufanya masuala ya biashara hiyo kazi mpaka sasa hivi Ofisi ya utaribu hawajapewa na kweli tutakua tunawapa kazi nzito, kwa sababu masuala ya biashara kama mlivyoona nyie wenyewe ni masuala amabayo ni mazito. Kwa bahati nzuri Mhe. Spika, katika suala la biashara kwa mfano vyombo vikubwa ambavyo vinasimamia mambo ya biashara ukiangalia *TRA* ni chombo cha Muungano, *TRA* iko Zanzibar na *TRA* iko Bara na *TRA* unakokwenda popote pale ipo *TRA* kwa hivyo mlango wa kwanza wanaoingia wafanyabiashara ni kupitia *TRA*.

Kwa hivyo si busara kwa Afisi yetu iliyoko Dar es Salaam kuacha kushughulikia masuala mengine ya msingi yakiweko ya siasa na mambo mengine ya kufuatilia Wizara kwa Wizara, kwa kuwa kuna vyombo maalum vinavyoshughulikia biashara ndio maana Afisi hii haijakabidhiwa suala hili. Lakini panapotokea jambo kwa mfano bidhaa imekaa pale imekwama tunataka kupata uamuzi wa haraka katika vyombo ambavyo viko pale kwa mfano kama Afisi ya Makamu wa Rais bado tunaweza kutumia chombo hichi kwa ajili ya kurahisisha yale maamuzi. Lakini tunawashauri wafanyabiashara wetu wafuate vyombo viliopo pale ambavyo vipo hapa Zanzibar na vile vile Afisi yetu ambayo Wizara yetu tunafanya kazi na Wizara wenzetu Wizara ya Biashara wataweza kupatiwa mambo ambayo wanahitaji.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mimi nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri ambayo yamenipa faraja na mimi mtu wa Kaskazini Pemba, lakini pamoja na majibu hayo nilikuwa na swali dogo nataka niulize.

Kwa kuwa Wenzetu wa Tanzania Bara wameshafanya mazungumzo na watu wa Serikali ya Kenya na wameelekea mwelekeo mzuri mpaka wenzetu wale wameweza kufaidika na mazungumzo hayo, na kwa sababu sisi Kaskazini Pemba tunaitumia zaidi bandari ya Shimoni na Bandari za Mombasa kuingiza bidhaa zetu na kumekuwa na changamoto ndogo ndogo ambazo zinasababishwa na wafanyabiashara na Serikali kwa upande ule wa wenzetu wa Kenya.

Je, Wizara ya Biashara ina mpango gani wa kwenda Mombasa kule ikakaa na Serikali ya kule na watu wa *TRA* wakazungumza ili kutatua hizi changamoto ndogo ndogo ambazo zipo zinazowakabili wafanyabiashara wetu wanaotoa bidhaa kutoka Mombasa kuja Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza Wizara yetu hatujapokea changamoto yoyote ya mfanyabiashara anayefanya biashara Shimoni, changamoto tunayoiona sisi Wizara ya Biashara kwamba wanaofanya biashara kutoka Pemba kwenda Shimoni wanafanya kwa njia za magendo na tumeshakamata mali nyingi ambazo zinatoka Shimoni kuja Pemba kwa njia za magendo. Lakini pia huko nyuma karafuu walikuwa wakichukua wafanyabiashara walanguzi mbali mbali yaani hawa watu wa magendo kutoka Pemba wakipeleka Shimoni wakibadilishana wakifanya kama inaitwa *batter trade* wakichukua kule sabuni na vitu vyengine vyengine sukari na kuleta Pemba changamoto iliyopo ndio hiyo.

Lakini kama kuna changamoto ya wafanyabiashara kama wanapata vikwazo bidhaa zoa hawawezi kununua wakaleta huku Zanzibar kwa njia rasmi Wizara yetu iko tayari kwenda kuzungumza kwa kupitia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kama ni changamoto kubwa, tutaizungumza bila ya wasiwasi na tutaipatia ufumbuzi. Ninachoomba niseme tu kwa upande wa Pemba wafanya biashara wa Pemba wasitumie visiwa vile kwenda kufanya biashara za magendo na wakaficha kunako visiwa, waende rasmi inaruhusiwa na wakati mwengine biashara sisi na Kenya wala hulipishwi ushuru, kwa sababu ushuru unaolipishwa wewe ni wa kutoka nje, kwa sababu ushuru sisi na wa nje ni mkubwa ukileta kitu kutoka nje ya Zanzibar unalipa ushuru mkubwa na ukenda nao Kenya utalipa ushuru mkubwa.

Lakini baina ya Tanzania na Kenya taratibu zilioko sio za kumfanya mtu kumshtua na kumtisha wafuate taratibu na sisi kama tulivyosema tutafanya utafiti kuona tunatumia Tanga ili iwe ndio *base* ya wafanya biashara wa Pemba kwa kuingia Kenya na kupata faida.

Nam. 136

Utekelezaji wa Ulipaji wa Viwango vya Mshahara

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:

Kwa kuzingatia kuwa Serikali imeweka viwango vipya vya mishahara kwa watumishi wa umma na wale wa sekta binafsi vikiwemo viwango watakavyolipwa vibarua.

(a) Je, viwango hivyo vipya vya mishahara hasa kwa vibarua vitatumika katika miradi mikubwa ikiwemo miradi ya ujenzi ya Serikali kama barabara na miradi mengine.

(b) Ni lini Serikali katika utekelezaji wa miradi yake mikubwa itaanza kulipa viwango vipya hasa cha kutoka 7,000/- kwenda 25,000/-

(c) Je, Serikali haioni kuwa kutimiza utekelezaji huu wa nyongeza kuathiri miradi mikubwa kutokana na fedha nyingi kutumika katika kulipa vibarua au "*daily workers*"

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nianze kwa kumtanguliza Mwenyezi Mungu *Allah Subhana Wataala* ambae nae anaendelea kutupa pumzi zake na tukaweza kukutana asubuhi hii katika Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 136 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu inapanga mishahara kwa Sekta binafsi tu, mishahara kwa Taasisi za Umma inapangwa na Wizara inayohusika na masuala ya utumishi wa Umma. Hivyo, ikiwa Miradi mikubwa ya Serikali itafanywa kwa Kampuni za Binafsi viwango hivyo vipya vya mishahara kwa Sekta binafsi vitatumika. Kampuni hizo za Binafsi zitalazimika kuwalipa wafanyakazi wake viwango vilivyowekwa kwa Taasisi binafsi bila kujali ukubwa au udogo wa mradi. Na ikiwa Kampuni hizo ni za Serikali basi zitapaswa kufuata Sheria na taratibu za Serikali ambazo zinasimamiwa na Wizara inayohusika na masuala ya Utumishi wa Umma.

(b) Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa uwezo alionao kwa mujibu wa kifungu cha 97(1), cha Sheria ya Ajira, nambari 11, 2005, alitangaza kima cha chini cha mishahara kwa sekta binafsi tarehe 30 Juni, 2017 *(Legal notice – nambari 68, 2017).* Tangazo hilo limechapishwa katika gazeti rasmi la Serikali *Vol. CXXVI No. 6660* la tarehe 21 Julai, 2017. Hivyo Taasisi zote husika za sekta binafsi zimetakiwa kutekeleza toleo hilo kuanzia mwezi Julai, 2017.

c) Serikali kutimiza utekelezaji huu wa nyongeza hakuathiri miradi mikubwa hasa kutokana na aina yenyewe ya ajira inayozungumzwa (vibarua). Kwa muda mrefu wafanyakazi wa vibarua wamekuwa wakilipwa kiwango cha chini sana cha malipo

ukiliganisha na kazi wanazozifanya. Pia, aina ya kazi hizo ni za muda mfupi na sio za muda mrefu na huwa ni za msimu, hivyo kiwango wanacholipwa pia kimezingatia hilo. Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nambari 11, 2005 mfanyakazi aliye katika ajira ya kibarua, afanye kazi katika hali hiyo si zaidi ya kipindi cha miezi sita. Iwapo muajiri anataka kuendelea nae na bado kazi hiyo ipo inaendelea (mradi mkubwa) mwajiri anapaswa kumuajiri mfanyakazi huyo kwa mkataba wa muda maalum au wa kudumu kutokana na mahitaji ya muajiri na kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja dogo la nyongeza.

a) Mhe. Spika, kama alivyotangulia kusema katika majibu yake ya juu ya tangazo alilolitangaza Tarehe 30 Juni, 2017 swali langu liko hivi ni dhahiri kwamba baada ya tangazo hili kutangazwa kumekuwa na changamoto nyingi katika sekta tofauti hasa ambazo zinazoingiza fedha au pia kuwa tegemeo la uchumi wetu hapa Zanzibar. Ni utaratibu upi sasa hivi Wizara yake imechukua ili kukabili changamoto zilizojitokeza juu ya tangazo hili hasa katika sekta ya utalii pamoja na sekta ya ujenzi ili kuleta unafuu wa wananchi pamoja na wawekezaji katika visiwa vyetu.

b) Mhe. Spika, tuna miradi mingi mkubwa Zanzibar ambayo ilikuwa tayari imeshaanza kujengwa hasa mradi wa Mzee Bakhresa ambaye ni muwekezaji mzalendo ambae tayari ameshakopa fedha nyingi sana kujipanga na mradi wake, sasa viwango hivi vilivyopangwa kutoka shilingi elfu saba kwenda elfu ishirini na tano kwa *unskilled labour* vimeleta ugumu wa utekelezaji wake.

Je, Wizara yake anatumia utaratibu upi wa kisheria ili kuleta msamaha au kuhakikisha kwamba hili jambo halitaleta ugumu katika utekelezaji wake na kulinda maslahi ya vibarua au hawa *unskilled labour* pamoja na uchumi na mwekezaji mwenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Simai swali lake la nyongeza lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:

a) Amesema ni unafuu upi au utaratibu upi tunaotumia katika kiwango hichi cha mishahara kwenye taasisi za binafsi.

Naomba nimjibu kwamba taratibu tunazozitumia ni lile tangazo ambalo Mhe. Waziri amelitamka la kwamba wafanyakazi wa taasisi binafsi walipwe kutokana kiwango ambacho Serikali kimepanga, kwa hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi ajue kwamba tangazo lile lilotolewa ni halali kwa hivyo tunawataka wafanyakazi wa binafsi hawa walipwe kiwango cha mishahara ya chini ambacho wafanyakazi hawa wamepangiwa.

Mhe. Spika, swali la pili naomba alirudie tena.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, kwa nia njema kabisa hata hilo swali la kwanza niliilouliza majibu niliyopewa siyo, sasa naomba nirudie suala la kwanza niliilouliza ili nipate majibu.

Mhe. Spika: La pili Mheshimiwa Simai.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Spika, suala la pili ni kwamba changamoto zilizojitokeza ni nyingi sana katika sekta tofauti, wapo wawekezaji kama Mwekezaji Mzee Bakhresa ambaye ni mwekezaji mzalendo tayari yeye ameshachukua mkopo katika mabenki na kujipanga katika ujenzi huu.

Je. Wizara yake inachukua utaratibu gani kuhakikisha kwamba unamlinda maslahi ya huyu muwekezaji ili ahakikishe kwamba anaweza kuendelea na mradi wenyewe kwa sababu viwango ambavyo vimetajwa vimekuja njiani wakati huyu muwekezaji ameshaanza ujenzi wake. Sasa ni utaratibu upi wa kisheria anasimamia kwa sababu sheria ya kazi haimpi nafasi Waziri kutoa msamaha. Sasa ni utaratibu upi wa kisheria atautumia Waziri ili kuhakikisha kwamba anamlinda maslahi ya Mzee Bakhresa na biashara yake hii ya uwekezaji hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naona hili suala lina *conflict of interest* ndani yake, lakini pia nahisi kabisa kwamba tumeshajibu si mara moja wala si mara mbili suala hili juzi tu tumeliongeza. Lakini napenda kumhakikishia tena kwamba Mheshimiwa sijui kama amekuja kwa ajili ya kumwakilisha Bakhresa kwa sababu suala hili analolizungumza linazungumzia Mhe. Bakhresa, kuna wafanyabiashara ni wengi sana na bahati nzuri kati ya wafanyakazi wazuri tunaowaheshimu na wanafanya kazi nzuri sana katika hii nchi yetu na wameongeza ajira nyingi sana katika hii nchi yetu ni pamoja na Mhe. Bakhresa na tunakwenda nae vizuri.

Sasa kama kuna masuala mengine zaidi ni vyema akapita ofisini tupate kumfafanulia vyema, lakini pia kanuni zipo na nimesema juzi kwamba kanuni zimeshaandaliwa zinangoja kutiwa sahihi na Mhe. Mwanasheria Mkuu naomba awe na subira kwa sababu yeye ni mwakilishi kwa kadri atakavyokuwa anasema ataweza kuwapotosha wananchi wakakosa kuwa na moyo wa kwamba Wizara haifanyi ipasavyo. Naomba tuendelee kushirikiana na yeye kama ni muajiri mmoja wapo awe ni mfano wa kuweza kufanya vizuri ili tuendelee kuweza kufanya kazi vizuri. Kwa sababu wanachama wetu tumekaa muda mrefu tumewakandamiza kama mtu yoyote anakuja kuleta mradi katika nchi yetu lazima ajipange kwamba anakuja kuleta mradi na afuate sheria za kulima vipimo ambavyo vimewekwa na Serikali. Ni kitu ambacho kimefanyiwa kazi na kimefanya kazi na kinafanya na wale wote ambao hawajaanza kulipa kuanzia sasa kwa kupitia Baraza lako Mhe. Spika, ni kwamba wale wote kuanzia Julai, kama hawajalipa itabidi walipe *arrears* ambazo walipaswa waanze kulipa.

Naomba tusianze kusema maneno mengi isipokuwa tutekeleze kwa uzalendo na kupenda wananchi wetu ambao wako katika hali ya mazingira magumu. Ahsante.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri suali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali yake vizuri na kwa ufanisi zaidi, Mhe. Naibu Waziri nikuulize swali moja la nyongeza.

Je. Mhe. Naibu Waziri ni taasisi ngapi ambazo zimetekeleza agizo hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bihindi Hamad Khamis swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Katika taasisi ambazo tulipangiwa kuzipitia mara hii ni taasisi 205 lakini kati ya taasisi hizo ambazo zimetekeleza agizo la hili ni taasisi 138.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar inaelekeza kwamba madhumuni ya kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kujali na kulinda maslahi ya watu wa Zanzibar, na kwa kuwa vibarua nao ni wananchi wa Zanzibar.

Je, Serikali itaimarisha vipi mishahara yao na kutokuwatenga na kuangalia upande mmoja wa waajiri, yaani Serikali itawajali vipi vibarua hawa nao kama inavyopandishwa mishahara ya Serikali na wao wawe wanapandishwa mishahara ili kulinda maslahi ya wananchi hao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mheshimiwa Spika, suala hili la mishahara nafurahi kusema kwamba kuna wengine wanawaonea huruma na waendelee kuwa na hali hiyo ni kwamba wana vigezo vyao, na mambo yote haya tunapofanya tunapitisha kwenye Bodi ya mishahara ambayo inakua na utata, hati ya muajiri vyama vya wafanyakazi na serikali. Kwa hiyo masuala yote haya yanapitiwa katika utaratibu unaofaa na ambao unazidi kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata maslahi yake ipasavyo:-

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. swali linalofuata ambalo pia limefanana na hili linaulizwa tena na Mhe. Simai Mohammed Said, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Tunguu.

Nam. 137

Viwango vya Mishahara Sekta Binafsi

Mhe. Simai Mohamed Said - Aliuliza:-

Je, utaratibu upi umetumika kushirikisha Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo hasa katika sekta ya Utalii katika kupanga viwango vipya vya mishahara kwa sekta binafsi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto naomba kumjibu tena Mhe. Simai Mohammed Said, Mwakilishi wa Jimbo la wananchi Tunguu swali lake Nam. 137 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005, chini ya Kifungu cha 93 cha Sheria hiyo upangaji wa kima cha mishahara kwa sekta binafsi hutangazwa na Mhe. Waziri anaehusika na masuala ya kazi baada ya kupokea ushauri wa Bodi ya Mishahara.

Mhe. Spika, Bodi hiyo iko katika mundo wa UTATU (TRIPARTITE +) yenye kuwashirikisha Serikali, Jumuiya ya Waajiri, Shirikisho la Vyama huru vya Wafanyakazi na Jumuiya ya wafanyakazi, Biashara na Viwanda na Wataalamu wa kujitegemea wanaoteuliwa na Mhe. Waziri anaeshughulikia masuala ya kazi. Kwa upande wa Serikali wahusika wakuu ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kutokana na unyeti wa suala hilo Mhe. Waziri wa Kazi mbali na kupokea ushauri wa Bodi husika, pia hupata Muongozo wa Serikali ili kusaidia na kufanikisha hatua zinazohitajika kulinda maslahi ya taifa letu. Kwa kuwa Serikali kupitia vyombo vyake vya juu hushirikisha Wizara zote, hivyo, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ilishirikishwa kikamilifu katika jambo hilo, hasa tukizingatia mchakato wa suala hili ulianza mwezi Agosti, 2016 na taarifa zake kuwasilishwa na kujadiliwa katika vikao hivyo kila hatua ilivyokuwa ikitekelezwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana swali la nyongeza kama huna naomba ukae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Sawa ahsante, Mhe. Spika, nitakwenda kwenye nyongeza tu. Mhe. Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Naibu Waziri, nimthibitishie tu kwamba Wizara ya Utalii katika hili halikushirikishwa kwa sababu barua ninayo hapa inayotoka Kamisheni ya Utalii, inasema kwamba Kamisheni yaUtalii haikushirikishwa katika zoezi la kuweka viwango vipya vya mshahara katika mahoteli..

Mhe. Spika: Naomba usisome sema tu kwamba unayo barua na kuuliza swali lako.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu aliyotoa Mhe. Waziri ya ambayo si ya kweli kwamba Wizara ya Utalii kwa upande wa Kamisheni ambacho ndio taasisi ambayo inayosimamia suala zima la sekta ya utalii upande wa Zanzibar. Je, Mhe. Waziri kwa upande wako ikithibitika kwamba sio kweli juu ya suala hili zima utachukua maamuzi gani kwamba sekta ya utalii ambayo sasa mahoteli mengi wafanyakazi wamekuwa wanapunguzwa na sekta hii haikushirikishwa na majibu haya hayakwenda sambamba pamoja na hali nzima ya hiyo utatu je, unachukua hatua gani hivi sasa ili

kulinda sekta hii mama ili kuhakikisha kwamba uchumi wa Zanzibar unaendelea na unaimarika.

Mhe. Spika: Ahsante naomba suala hilo ajibu Waziri anayehusika na utalii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwanza na mimi nichukuwe fursa hii ya kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana Wanawake na Watoto kwa majibu yake mazuri kabisa aliyoyajibu.

Lakini napenda vile vile kuweza kutoa ufahamu kidogo kwa Waheshimiwa namuuliza swali Mhe. Mwakilishi Simai Mohammed wa Jimbo la Tunguu.

Kwanza wizara yetu si wizara ya utalii, inaitwa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, anaposema wizara imeshirikishwa aelewe kwamba Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nayo imeshirikishwa kikamilifu kwa hili napenda niweke wazi kwamba Wizara ya Habari imeshiriki mikutano mpaka vikao vyote vya serikali ambavyo vimejadili suala hili, Wizara ya Habari ipo na mimi ndiye Waziri nimeshiriki na tumelijadili suala hili kwa kikamilifu.

Maamuzi yaliyotolewa na serikali yapo pamoja na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, kuhusiana na Kamisheni kama kuna Kamisheni kuna watu waliosema hawakushirikishwa labda aieleze ni Bodi. Hili lalamiko hili liko kubwa sana, walianza kusema hawakushirikishwa katika kuchaguliwa kwenye Bodi ya Makamisheni, wako wamesema hawakushirikishwa katika kuundwa ile Kamisheni ya Utalii Sheria vitu kama hivyo. Lakini wizara wenyewe imeshiriki kikamilifu napenda suala hili wananchi walielewe wazi kwamba Wizara imeshiriki katika mchakato huu kiserikali na serikali imefanya suala hili kikamilifu. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nam. 27

Ukosefu wa Kituo cha Kununulia Umeme wa Tukuza

Mhe. Machano Othman Said - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibiwe swali langu Nam. 27 pamoja na marekebisho yake katika para ya mwisho sio baadhi bali ni hadhi ya Manispaa.

Katika kupeleka huduma za jamii karibu na wananchi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Wilaya Mpya za Magharibi ‘A’ na Magharibi ‘B’ ambazo tangu kuanzishwa kwake, Wilaya ya Magharibi ‘A’ ina ukosefu wa huduma muhimu za jamii, hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi wa Wilaya hiyo. Miongoni mwa huduma hizo ni ukosefu wa kituo cha kununulia umeme.

Je, lini Serikali itaamua kuanzisha kituo cha kununulia umeme kwa Wilaya hiyo ambayo ina hadhi ya Manispaa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said wa Mfenesini swali lake Nam. 27 pamoja na marekebisho yake kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa hivi sasa Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme haioni haja ya kuongeza vituo vipya vya mauzo ya umeme zaidi ya vilivyokuwepo, kwa vile huduma hiyo ya kuuza umeme inapatikana kwa kutumia mtandao wa simu wa Zantel. Hata hivyo, Wizara yangu inaendelea na uratibu wa kutanua wigo wa huduma hiyo ya uuzaji wa umeme kwa kutumia wakala ambao utaenea na kuwafikia wananchi hadi mitaani.

Mhe. Spika, huduma hii ya kutumia wakala ilitarajiwa kuanza kazi rasmi mnamo mwezi wa Agosti 2017, lakini kutokana na sababu za kiufundi katika mifumo ya kompyuta huduma hiyo imechelewa. Hata hivyo Wizara yangu kupitia Shirika la Umeme inaendelea na juhudi za kuhakikisha huduma hiyo inaanza kutolewa kabla ya kumalizika kwa mwaka huu wa 2017. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niulize suala moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, wilaya ya Magharibi (A) yenye majimbo 6 ya uchaguzi na wananchi wasiopungua laki mbili (2,000,000) ina wananchi wengi wengine wako vijijini mfano Bumbwisudi, Mwachealale, Mfenesini na kadhalika. Hivyo kusema kwamba Serikali haianzishi vituo vipya vya kununua umeme na kuwakosesha wananchi wa wilaya ile huduma muhimu ya jamii. Suala langu lipo hapa.

(a) Kwa kuwa katika wilaya ya mjini kuna vituo vitatu Gulioni, Michezani na Malindi na Manispaa ya Magharibi (B) kuna vituo viwili vya Mazizini na Mwanakwerekwe haoni kwamba kuki *shift* kituo kimoja cha mjini na kukipeleka katika manispaa ya Magharibi (A) ili wananchi wa Magharibi (A) wameze kupata huduma hizo.

(b) Kwa kuwa huduma za ununuzi wa ZANTEL huwa zina matatizo mara kwa mara hata hizo huduma za uwakala hakuna risiti ambayo inatolewa kwa wakala je haoni wananchi wa wilaya hii wataendelea kuteseka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni vyema tukastahamili mpaka ukamilishaji wa haya tuliyokuwa tumeyasema kukamilika, na tumesema kwamba ndani ya mwaka 2017 yatafanyakazi na tutafika mpaka kwenye maeneo, si sahihi kuondosha tatizo pahala pamoja lakini kupeleka tatizo kwengine itakuwa si utatuzi mzuri, mjini kuna idadi ya wengi zaidi ya wakaazi lakini busara zaidi kwa vile tuna mpaka kwenye *petroleum station* na kule zipo *petroleum station* umeme utapatikana kwa wakati. Ahsante sana.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri. Kwa kuwa Wilaya ya Micheweni ni sehemu moja wapo

ambao kuwa ilikuwa na mahitaji ya kupata vituo vya kuuzia umeme pamoja kulipia maji, na hadi sasa vituo hivyo havijakuwepo je, ni lini sehemu hizo zitaweza kuwekewa vituo vya kuuzia umeme na kulipia maji katika Wilaya ya Micheweni Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli vituo vyetu Pemba ni Chake Chake, Wete na Mkoani pana haja ya kufikiria Micheweni na tayari lilikuwa nimezungumza kwamba nitafika, kuona namna gani tunaweza tukaanzisha *post* pale pana haja hiyo ni jambo la msingi na nitakapokwenda nitakujulisha *inshaallah*.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Waziri, wananchi wa Wesha na Ndagoni wafuata huduma ya umeme Chake Chake je huoni ipo haja kupitia Shirika la Umeme kuweka kituo cha umeme maeneo ya Wesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza kama nilivyokuwa nimejibu, katika suala la msingi kwamba ile huduma itakuwa inapatikana vizuri lakini pia ZANTEL wanasaidia sana hii huduma ipatikane. Kwa hivyo kukamilika kwa mradi ule maana yake utanufaisha Unguja na Pemba na si busara kila pahala tukaweka vituo, tofauti aliyozungumza na ile ya Micheweni. Micheweni ni hoja ya msingi kutokana na *geography* yake ilivyo, lakini niseme kwamba hivi baada ya kukamilika kwa haya makubaliano tuliyonayo wananchi watapata nafuu sana kwa huduma hii ya umeme. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 36

Kukosa Umeme Kupitia Majenereta ya Akiba

Mhe. Suleiman Sarhan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada za kutafuta chanzo mbadala cha umeme, ilipata majenereta ya akiba lakini majenereta hayo kwa muda mrefu toka yalipoletwa hayatumiki.

(a) Ni Sababu zipi zilizosababisha majenereta hayo kushindwa kutumika na hivyo kupelekea hasara kwa nchi.

(b) Kama majenereta hayo yamepitwa na wakati na hayana vipuri na hayawezi kutusaidia wakati wa matatizo, kwa nini yanaendelea kuwekwa na kututia hasara.

(c) Je, majenereta hayo yanafanyiwa ukarabati (*service*) mara ngapi kwa mwaka na gharama yake ni kiasi gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako na naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarhan Said wa Chake Chake kabla ya kumjibu Mhe. Mheshimiwa naomba nianze kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Ni vyema ifahamike kuwa ununuzi wa majenereta 32 ya dharura yaliyoko Mtoni ulifanyika kufuatia kisiwa cha Unguja kukosa huduma ya umeme kwa zaidi ya miezi mitatu, hali iliyosababishwa na hitilafu katika waya wa baharini mnamo mwaka 2008/2009, katika kipindi cha awali majenereta hayo yalikuwa yanatumika kwa kuondosha mgao wa umeme, uliotokana na kuzidiwa uwezo kwa waya wa baharini uliokuwepo.

Uendeshaji huo wa majenereta ulidumu hadi kupatikana kwa waja mpya wa baharini wenye uwezo wa magawati 100 ambao ndio unaotumika hadi hivi sasa. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 36 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sababu kubwa iliyopelekea majenereta hayo kusita kutumika kwa hivi sasa katika wakati wa kukosekana umeme kutoka TANESCO ni kutokana na gharama kubwa za uendeshaji ambazo zinaweza kupelekea kuongezeka kwa bei ya umeme itakayosababisha mzigo kwa wananchi.

Aidha, kwa mujibu wa rasimu ya makubaliano ya matengenezo na kampuni ya MANTRAC ambayo ni wakala wa majenereta hayo inatakiwa kufanywa kila baada ya muda maalumu wa uendeshaji ambapo gharama yake ni jumla ya dola za kimarekani 761, 864.75/= ahsante.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini suala la umeme kwa Zanzibar ni suala lina upeo mkubwa sana tukiangalia kwanza suala la umeme, linatoka mbali sana na linapita chini ya bahari na sasa hivi, kwa matatizo ya tabia za nchi mara bahari inachafuka na miundo mbinu inaweza ikaharibika na matengenezo yake yanaweza yakatimia miezi au zaidi kama hatujajitayarisha.

(a) Sasa Serikali ina mpango gani wa kutafuta umeme mbadala wa uhakika wa kuweza kukidhi haja pale patakapotokea matatizo yoyote, kutokana na hali ambayo sasa hivi Zanzibar kila kitu mpaka *blander* lazima utumie kwa umeme, kwa hivyo serikali imejipangaje kuhusu suala hilo.

(b) Serikali haioni umuhimu wa kutafuta ugatuzi wa kimkoa ili kuweza kuchukua umeme wa kimkoa kabla ya kuingia katika *grid* ya taifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Serikali inafanya jitihada mbali mbali za kuhakikisha tunapata umeme mbadala na yeye kama Mjumbe wa Kamati anafahamu vizuri labda kauliza kwa niaba ya wananchi, anafahamu mpaka hatua ambayo tumefikia na tuko vizuri tu kwa mujibu kwa data ambazo Serikali inayo. Ahsante sana.

Nam. 30

Usambazaji wa Taarifa Kupitia Mitandao Kuhusu Utumiaji wa Vyakula Visivyo salama kwa Afya za Wananchi

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na tabia ya kuzusha taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii inayoelekeza kutofaa kwa baadhi ya vyakula kwa matumizi ya binadamu lakini hatusikii Serikali ikikanusha taarifa hizo.

(a) Je, Serikali huwa hawavioni vitu hivyo vinavyorushwa kwenye mitandao kuonyesha baadhi ya vyakula, dawa na vipodozi kuwa sio salama kwa afya zetu.

(b) Je, kama vitu hivyo vinavyooneshwa kwenye mitandao kuwa ni kweli au si kweli kwanini Serikali haitoi tamko.

(c) Je, kipo kitengo maalum cha Wizara ya Afya kinachofuatilia taarifa kama hizo na zinazotolewa kwenye mitandao hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake Nam. 30 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii, kulieleza Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, inafanya kila juhudi ili kuwalinda wananchi wake kiafya, na kuweka mazingira mazuri katika hali ya usalama na ubora wa maisha yao.

Mhe. Spika, ni kweli kwamba kumeibuka mitandao mingi ya kijamii, ambayo inaitumia fursa ya “UTANDAWAZI”, kutoa taarifa mbali mbali zikiwemo zinazohusu ubora wa vyakula tunavyotumia, taarifa hizo huwa wanazitoa bila ya kufanya uchunguzi.

Mhe. Spika, kupitia mitandao hiyo, hivi karibuni zilisambazwa taarifa za uwepo wa vyakula vya watoto, visivyo na ubora, vinavyojulikana kwa jina la chama, pia uwepo wa mchele wa Plastik katika soko la Zanzibar.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Bodi ya Chakula, Dawa na Vipondozi, ilifuatilia kwa kina taarifa hiyo pamoja na kufanya uchunguzi juu ya uwepo na jinsi vilivyoingizwa katika soko la Zanzibar, na tuligundua kwamba taarifa hizo sio za kweli ni taarifa ambazo ziliokotwa kutoka sehemu tofauti nje ya Zanzibar, na kutengenezwa, kurushwa kwa wananchi wa Zanzibar kama kwamba zipo Zanzibar kwa lengo la kuleta mtafaruku kwa wananchi.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Bodi ya Chakula, Dawa na Vipondozi baada ya kukamilisha uchunguzi juu ya taarifa hizo ilichukua hatua ya kuwatuliza wananchi kufuatia uongo huo kwa kutoa tamko la kuukana na kuwaeleza wananchi ukweli na uimara wa Serikali yao kupitia Bodi hii ya Chakula, Dawa na Vipodozi, kwa kuwathibitishia kwamba vyakula vyote vilivyomo katika soko la Zanzibar ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Bodi hii hii ilitoa tamko hili kwa vyombo vya habari mbali mbali kwa vipindi tofauti kama ifuatavyo:-

Kipindi cha Redio katika ZBC 22/07/2017.

Kipindi cha ZBC TV 31/07/2017.

Ufafanuzi katika mialiko ya vipindi mbali mbali vya Radio Binafsi kama *Coconut FM*, *Hits FM*, Chuchu *FM*, Mwenge *FM*, Bahari *FM* na Assalam *FM*.

Tulitoa taarifa kupitia Gazeti la Zanzibar Leo na katika mitandao (Tovuti ya wakala wa *TFDA (WWW.ZFDB.GO.TZ*) na katika ukurasa wake wa *Facebook* tarehe 14/07/2017.

Mhe. Spika, tunawashukuru sana wananchi wa Zanzibar kwani baada ya kupata taarifa zetu kupitia vyombo mbali mbali tulivyovitaja, waliondosha hofu na kuendelea na shughuli zao za maendeleo, kama kawaida.

Mhe. Spika, Kitengo cha Bodi cha Chakula, Dawa na Vipodozi ndio chenye jukumu la kufuatilia taarifa na kujibu hoja zote zihusuzo usalama na ubora wa Chakula dawa na vipodozi. Ahsante.

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Nashukuru Mhe. Spika na mimi nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake makubwa sana tena mazuri lakini kwa kuwa tatizo hili la kupotesha taarifa imekuwa ni kama tabia kwa watu ambao pengine ama kwa bahati mbaya ama kwa wengine wasioipendelea mema Zanzibar na watu wake, je Serikali huwachukulia hatua gani watu hawa ili kutokurudia tena katika masuala ambayo hayana uhakika.

Lakini swali la pili kwa sababu ya vitu kama chakula na vipodozi ni vitu vinavyotumika moja kwa moja na baada ya kutumika mtu yule ambaye ametumia inawezekana akapata

madhara. Lakini vitu hivi kwa msimamo tulionao ni kwamba vinakaguliwa nje ya nchi na ndani ya nchi katika kuingia pamoja na mletaji ambapo vitakuwa na *record* je, pale inapotokezea mtu au vile vitu vikawa vinaonekana vimeleta madhara kwa wananchi wetu hatua gani za kisheria zinachukuliwa kuanzia mkaguzi wa nje wa ndani pamoja na aliyeleta vitu hivyo ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, kuhusu suala lake yeye ni hatua gani ambazo Serikali zitachukua kwa kweli Wizara ya Afya haihusiki na hatua ambazo zitachukuliwa kwa wale ambao wanarusha mitandao hiyoi naona ipo Idara maalum au chombo maalum ambacho kinadhibiti hali ya usalama wa nchi yetu na ina haki ya kufanya kazi hii.

Lakini kuhusu swali la pili namuomba mheshimiwa arudie.

Mhe. Spika: Naomba urudie swali (b) mheshimiwa

Mhe. Suleiman Sarhan Said: Waheshimiwa kwasababu swali la kwanza ameshalijibu wizara haina uwezo wa kudhibiti hali na swali la pili linaenda hukohuko.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar: Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri pia naomba nijibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo yaliyoloulizwa na Mhe. Suleiman Sarhan.

Mheshimiwa vyombo vinavyohusika kwa mujibu wa sheria vipo ikiwemo Jeshi la Polisi na huwa vinafanya kazi hiyo pale inapothibitika kwamba zipo bidhaa zilizoingizwa kinyume na utaratibu wa sheria baada Taasisi husika kuthibitisha kufanya hivyo na wale wote waokwenda kinyume na utaratibu wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na kupitia Baraza hili Tufuku napenda tena nitowe wito kwa Jeshi la Polisi kuongeza kasi na bidii katika kufuatilia wale wote wanaofanya uhalifu wa aina hiyo.

Vile vile na wale wanaotoa uvumi kinyume na taratibu za nchi wapo watu wanaojitokeza kutoa uvumi mbali mbali ambao ni kinyume kabisa kwa nia ya kugombanisha wananchi na Serikali yao. Kwa hivyo na wao wote watachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria wale wote wanaotoa uvumi wa ovyo nataka niwahakikishie kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein na wale wanaojisemea maneno ambayo ni kinyume na taratibu watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 69

Matumizi ya Jenereta la Dharura Hospitali ya Mnazimmoja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Hivi karibuni kulifanyika matengenezo ya umeme Tanzania bara ambayo kwa Zanzibar ilihusu kuzimwa kwa nishati hiyo kuanzia asubuhi hadi jioni na taarifa ya kuzimwa huko ilitolewa siku moja kabla lakini jambo la kushangaza, Hospitali ya M/Mmoja ilishindwa kufanya matayarisho ya kuwasha jenereta kwa madai ya gharama kubwa mpaka Mheshimiwa Waziri alipoingilia kati.

(a) Je, jenereta hilo ni la kazi gani kama ikitokea dharura ya kukatwa umeme halitumiwi mpaka itoke amri kutoka juu.

(b) Je, kwanini Uongozi wa Hospitali haukufanya matayarisho ya mapema kuwasha jenereta hilo wakati tangazo la kuzimwa umeme limetolewa mapema.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kuendesha majenereta hayo endapo dharura inatokezea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Paje swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa swali hili lina marekebisho katika kifungu cha cha (c) nitayasoma wakati ukifika.

Mhe. Spika, kwa sasa Hospitali ya Mnazimmoja inayo majenereta 6, ambayo yanatumika kuleta umeme wakati wa dharura tu, kati ya majenereta hayo yapo ambayo yanajiwasha wenyewe wakati umeme ukiondoka yaani *(Automatic)*, majenereta haya yanatoa huduma katika sehemu ya mashine ya MRI, Wodi ya Watoto, Wodi ya Wazazi na n.k.

Pia yapo majenereta ambayo, ikitokea dharura ya kukosa umeme hayawaki hadi tuyawashe.

Mhe. Spika, ni kweli tulipokea matangazo juu ya matengenezo ya umeme Tanzania Bara ambapo Zanzibar ilihusika na kukosa huduma hiyo kwa wananchi na taasisi ikiwemo Hospitali ya Mnazimmoja. Uongozi wa hospitali ya Mnazimmoja baada ya kupata taarifa ya kutokuwepo kwa umeme kwa muda mrefu, na kwa sababu tunafahamu uwezo wa kila jenereta, tuliamua kufanya *service* ya dharura kwa baadhi ya majenereta ili kuweza kuwa na uhakika wa jenereta zote kuweza kutoa huduma za umeme kwa muda uliopangwa na bila ya kusitisha huduma ambazo zitahitaji umeme.

Mhe. Spika, kati ya jenereta ambazo tulizifanyia *service* ya dharura ziko ambazo kwa maumbile yake zilifanya kazi, mara baada ya kufanyiwa *service* na zipo ambazo zilihitaji zipumzishwe kwa muda maalum, baada ya *service* na ndipo ziweze kufanya kazi.

Ni kweli, baada ya huduma ya umeme kuondoka katika Hospitali kama tangazo tulivyolipokea, jenereta ambazo ni *automatic* zilifanya wajibu wake, na zile ambazo zilihitaji kuwashwa ziliwashwa, isipokuwa jenereta moja ambalo lilihitaji lipumzishwe kwa muda baada ya *sevice* tulilazimika kutokuliwasha kwanza ili kumalizia muda, uliosalia.

Mhe. Spika, hapo na ndipo tulipopokea simu na agizo kutoka kwa Mhe. Waziri kututaka kuwasha jenereta hiyo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala ni lile ambalo niliomba kwamba nitalifanyia marekebisho kidogo naomba nilisome, kuhusu suala ni kiasi gani cha fedha, kinachohitajika kuendeshea majenereta hayo, ni kwamba kila jenereta hutumia lita 40 za disel kwa saa, kwa jenereta 6 ni sawa na kutumia Shs. laki tano na nne (500,004/=) kwa matumizi ya saa moja.

Kabla ya jawabu hili la laki tano Mheshimiwa tulikosea kidogo *typing error* iliingia tukaandika milioni moja na laki mbili (1,200,000/=) Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri namuonea huruma sana tena sana lakini namuomba sana kabla ya kuja kujibu swali hili ajaribu kufanya utafiti kwanza wasije wakamuuliza mbuzi kwenye gunia. Jenereta hili lilokuwepo ni moja tu na linatosha hospitali nzima na miongoni mwa waliopiga kelele jenereta likafungwa ni mmimi mmoja na sote baadhi ya wajumbe ni shahidi tumepata msaada wa jenereta moja kubwa linaweza kuendesha hospitali yote nzima wacha sita, matano, manne na limefungwa baada ya kelele za waheshimiwa wawakilishi miongoni nikiwemo mimi.

Nimuulize swali dogo sana la nyongeza Mhe. Naibu Waziri hivi kweli siku zote tunaanza kupiga kelele *generator* lipo mpaka apige simu Waziri ndio likafunguliwe jenereta kama hayupo Waziri, Naibu Waziri ndio kweli tunataka kuwahudumia wananchi wetu kisawasawa kweli hivi. Ni lini usumbufu huu mtauondoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku mwakilishi makini wa Jimbo la Paje swali lake la nyongeza kama ifutavyo:

Mheshimiwa ni kweli hilo *generator* unalolisemea kwamba lina uwezo kutumika Hospitali nzima peke yake lakini kutokana na kwamba tunayo ma-*generator* ya kutosha hatuona sababu ya kuli-*overload generator* moja hali ya kuwa ma-*generator* mengine yapo na yamefungwa kufanya *service* katika sehemu tofauti, ni kweli nakiri kwamba lipo *generator* ambalo lina uwezo huo.

Lakini nilisema katika jawabu langu la msingi Mheshimiwa kwamba tuliliwacha lisiwake kutokana na *service* ambazo tulizifanyia na tulihitaji lipumzike. Mhe. Waziri kweli alipiga simu alipokea simu kutoka kwa watu kwamba generator halijawashwa hatupati taa na kweli alipoagiza liwashwe *generator* liliwashwa likiwa limebakia na dakika chache kukamilisha ule muda ule ambao tulikuwa tunalipumzisha.

Mhe. Jaku naomba uridhie na nitafata maelezo yako ukifatilia zile sehemu ambazo unanielekeza. ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kutoa maelezo ya ziada kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Serikali itahakikisha kwa kuwa ma-*generator* yale yamenunuliwa kwa nia ya kutoa huduma bora katika hospitali yetu kuu ya Mnazimmoja yatahakikisha majenereta hayo yanatoa huduma hiyo na wale wote ambao kwa njia moja au nyengine watafanya *sabotage* kwa makusudi ili majenereta hayo yasitumike ipasavyo hatua za kisheria zitachukuliwa.

Lakini napenda sana niungane na Mhe. Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia shughuli hii na naamini pale ambapo ma-*generator* yatahitajika kufanya basi majenereta hayo yatafanya kazi na yeyote yule ataekwenda kinyume na utaratibu huu basi hatua muwafaka zinachukuliwa za kiserikali ili kuhakikisha wanatiwa adhabu ipasayo na majenereta hayo yawe yanafanya kazi kama ilivyokusudiwa. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 10

Ongezeko la Makosa ya Barabarani

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma (Kny. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis): - Aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la makosa ya ajali za barabarani zinazosababishwa na uzembe unaofanywa na madereva na kupelekea vifo pamoja na ongezeko kubwa la ulemavu wa viungo.

(a) Je, Serikali inachukuwa hatua gani za ziada ili kuona hali hii inapungua au kuondoka kabisa.

(b) Je, ni lini Serikali itaweka utaratibu mzuri wa malipo kwa wanaobainika na makosa na kuondoa urasimu uliopo hivi sasa unaosababishwa na watendaji waliopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis Mwakilishi Nafasi za Wanawake Mkoa wa Kusini Unguja swali lake Nam. 10 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inachukua hatua zifuatazo ili kuona hali ya ogezeko la ajali inapungua au kuondoka kabisa.

- Kufanya ukaguzi wa ajali kila inapotokezea ajali ili kubaini chanzo kinachosababisha ajali pamoja na kuangalia uhalali wa dereva anayesababisha ajali.

- Kumfungulia mashtaka kila dereva aliesababisha ajali.

- Kuweka alama za barabarani kila inapojengwa barabara.

- Kuangalia uzima wa vyombo *(road worthless)* vyote vinavyotumia barabara kabla ya kuviruhusu kutembea barabarani.

(b) Wanaobainika na makosa wanapelekwa mahakamani na faini hulipwa huko kwa utaratibu mpya wa malipo yote ya Serikali kulipiwa kupitia Benki, kwa kuondoa changamoto zilizopatikana katika kuliendesha zoezi hili, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imo katika hatua za mwisho za kuondoa urasimu wa malipo kwa kutumia miamala ya malipo ya fedha kwa kutumia njia za Kieletroniki pamoja na malipo ya fedha kwa kutumia simu za mkononi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri na katika hatua alizozichukuwa Serikali kuweka alama barabarani kwa zile barabara ambazo zinajengwa. Je, ni hatua gani wanazozichukua kwa zile barabara ambazo zimeshajengwa na hazina alama barabarani na zinasababisha ajali za mara kwa mara ikiwemo barabara kuanzia Matofalini kupitia Mitondooni, Kisauni hadi Fumba ni hatua gani Mhe. Waziri unachukua. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wza Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Mwanaasha swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli nilizungumza pia jana suala hili kwamba kuna tatizo hivi sasa ambalo ni changamoto kwetu baada ya kuziweka hizi alama kuna watu wanazichukua zile alama kuziondosha au madereva nao kuzigonga. Mimi nitamuomba sana Mhe. Mwakilishi na Wawakilishi wote kwa jumla tuendelee kutoa elimu kwa watu wetu kuwa zile alama zinatusaidia sana katika kuepusha ajali barabarani na vile vile kuwachukulia hatua madereva ambao wanoendesha kwa mwendo wa kasi au wanaendesha bila ya uangalifu.

Kwa hivyo mimi nataka kusema kwamba Mfuko wa Barabara wamekuwa wanatenga kila mwaka pesa na sisi tutahakikisha kwamba zile pesa zinazotengewa kwa ajili ya kuweka alama barabarani tutahakikisha kwamba zile sehemu ambazo alama tunazirejesha ili wananchi wapate kuzijua na vile vile madereva wasipate sababu kufanya makosa. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 99

Usafiri wa Boti na Meli Za Kisasa

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Shirika la Meli Zanzibar linahitaji kupatiwa meli za kisasa, au Boti za kisasa kwa ajili ya usafiri wa haraka, kati ya Unguja – Pemba, Unguja Dar es Salaam, ili Shirika liweze kujiendesha kibiashara. Kwa kuwa Shirika la Meli la Zanzibar ni chombo muhimu kwa kutoa huduma kwa wananchi, kwa kutumia usafiri wa meli.

Je, Wizara ina mpango gani wa kupata meli au boti kwa ajili ya Shirika hilo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukuwa nafasi hii kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi Wananchi Jimbo la Kijitoupele swali lake Nam. 99 kama ifuatavyo:-

Wizara kwa kushirikiana na Serikali Kuu hivi karibuni imelifanyia mageuzi Shirika la Meli ili liweze kuimarika pamoja na kujiendesha kibiashara.

Mageuzi hayo yamehusisha mpango wa kulipatia Shirika la Meli, Meli mpya na za kisasa ili kufanikisha lengo hilo.

Kwa kuanzia mnamo mwaka 2015 Serikali imelipatia Shirika la Meli, Meli mpya na ya kisasa ya MV. Mapinduzi II na katika muendelezo wa azma hii, katika bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2017/18, Serikali tayari imetenga jumla ya T.shs.18 bilioni kwa ajili ya ununuzi wa meli nyengine mbili ikiwemo meli ya mafuta na nyengine ya abiria na mizigo kwa lengo la kuliimarisha Shirika la Meli na vile vile kutekeleza Ilani ya Uchaguzi CCM ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafiri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa azma kuu ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapata meli mbili ili kusaidia usafiri wa hapa na pale katika nchi yetu jee kwa kuzingatia umuhimu wa meli yetu ya usafiri tuliokuwa nayo ya MV Mapinduzi II Wizara haioni kuharakisha hili tukatafuta meli moja tu ya usafiri kwanza halafu ya mafuta ikaja baadaye.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kijitoupele swali lake la nyongeza ni kama ifuatavyo.

Kama tulivyosema tunaona umuhimu na hasa pale meli yetu ya MV Mapinduzi II inapokuwa inapata matatizo ya kiufundi kwa hivyo tunaendelea na mchakato na karibuni tutatoa taarifa kuhusiana namna gani tulipofika mpaka tutakapofanikisha hili swali ambalo ni muhimu katika kuendeleza sekta hii ya usafiri baharini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe wakati wa maswali umekwisha na tangazo la wageni Waheshimiwa Wajumbe wageni wetu wa leo ni wageni wa Mhe. Mwanaasha Khamis Juma Mwenyekiti wetu wa Baraza na Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chukwani wanatoka Baraza la Vijana Shehia ya Tomondo ambao wako saba, Waongozwa na Ndugu Salama Hassan Mussa ambaye ni Makamo Mwenyekiti naomba asimame wamuone, pia yupo Katibu ambaye ni Ndugu Juma Rashid Kombo naye naomba asimame wengine ni Ndugu Abdu Ali Iddi, Ndugu Ridhiwana Rashid, Ndugu A. Mpelembe, Ndugu Rajab Muhidin na Ndugu Fatma Juma Hamad karibuni sana Baraza la Wawakilishi.

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Spika: Naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ili aje awasilishe Ripoti ya Wizara yake.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima kwanza kabisa napenda kumshukru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutujaalia afya njema, hekima na kutuweza kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa rehema, nguvu na uwezo ili tuweze kutekeleza vyema mipango na malengo tuliyojipangia kwa manufaa ya wananchi wote.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuongoza vyema katika kupanga na kutekeleza mikakati ya kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu, uongozi wake mahiri, thabiti, makini unaendelea kuwa dira katika utekelezaji wa kazi zetu...

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Waziri naomba nimpishe Mwenyekiti aje achukuwe nafasi. Mhe. Mwenyekiti karibu.

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar)alikalia kiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri endelea

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: pia napenda Mhe. Mwenyekiti,pia naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, nachukua na fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, Zubeir Ali Maulid na Naibu Spika, Mgeni Hassan Juma pamoja na wasaidizi wako wote

wakiwemo Wenyeviti na Katibu wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kwa hekima, busara na uadilifu. Umahiri wako katika kuliendeleza Baraza hili umewezesha kuwepo na mijadala makini ambayo imesaidia sana kuimarisha utekelezaji na majukumu yetu ya ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kuchukua fursa hii kuushukuru uongozi wote wa wizara yangu, nikianza na Naibu Waziri, Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, Katibu Mkuu ndugu Fatma Gharib Bilal, Manaibu Makatibu Wakuu, Mauwa M. Rajab na Hassan Khamis Hassan, Kamishna wa Kazi, Katibu wa Mtendaji Baraza la Vijana, Wakurugenzi Watendaji wote kwa mashirikiano wanayonipa katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba kuchukua fursa hii adhimu kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, Utalii ambayo ilifanya kazi zake za kawaida kwa mwaka 2016/2017 kwa kutembelea taasisi mbali mbali za Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na kupitia Ripoti ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kama ilivyojipangia katika mpango wa kazi wa fedha wa mwaka 2016/2017. Pia namshukuru na kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) pamoja na wajumbe wake wote kama wafuatao.

1.	Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	-	Makamo Mwenyekiti
2.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
3.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Mjumbe
4.	Mhe. Maryam Thani Juma	-	Mjumbe
5.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Mjumbe
6.	Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Mjumbe
7.	Ndg. Himid Haji Choko	-	Katibu
8.	Ndg. Mussa Issa Mussa	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefanya kazi nzuri sana na wizara yangu na imeonesha umahiri mkubwa na moyo wa kujituma katika kuhakikisha kuwa wizara inafanikiwa kukamilisha utekelezaji wa majukumu yake kwa lengo la kuimarisha na kustawisha maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Aidha, kamati hii imekuwa mstari wa mbele kuishauri wizara pale ambapo zinajitokeza changamoto za kiutendaji, kamati hii huwa inatoa ushauri wa namna ya kuzikabili changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nichukue fursa hii nitoe muhtasari wa utekelezaji wa ushauri wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kama ifuatavyo:

Sekta ya Kazi

Ushauri Nam.1.Kamati inataka wizara kufatilia kwa ukaribu zaidi suala la wafanyakazi walio katika sekta binafsi ili kuhakikisha wanapatiwa mikataba ya ajira.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi nchini ni la Kamisheni ya Kazi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira Nam.11 ya 2005. Katika kusimamia jukumu hilo ipasavyo Kamisheni ya Kazi hufanya ukaguzi kazi ili kuhakikisha sekta binafsi zinatekeleza sheria za kazi na inasimamia na kuhakiki mikataba ya wafanyakazi wa sekta binafsi nchini.

Wizara imeendelea kufatilia kwa karibu zaidi suala la wafanyakazi walio katika sekta binafsi ili kuhakikisha wanapatiwa mikataba ya kazi. Jumla ya taasisi 240 (Unguja 156 na Pemba 84) zilifanyiwa ukaguzi ikiwemo kuangalia mikataba ya wafanyakazi ambapo tuligundua taasisi hizo zina wafanyakazi 5,611, kati ya hao wafanyakazi wapya waliokuwa hawana mikataba ni 2,301. Wizara ilizitaka taasisi husika kuwapa wafanyakazi wao mikataba kama sheria za kazi zinavyoelekeza. Hivyo, wizara kwa kipindi cha 2016/2017 imethibitisha jumla ya mikataba ya kazi 2,301 (Unguja 1,939 na Pemba 362) kwa wafanyakazi wa sekta binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza kufatilia suala hili ukaguzi wa kazi kwa taasisi binafsi unafanywa mara kwa mara ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria za kazi kwa 2016/2017 jumla ya taasisi binafsi 240 (Unguja 156 na Pemba 84) zimefanyiwa ukaguzi kazi ili kuhakikisha zinatekeleza ipasavyo sheria ya kazi ikiwemo kuwapatia wafanyakazi wao mikataba ya kazi inayokubalika kwa mujibu wa sheria. Endapo itagunduliwa kuwa taasisi hazitelezi ipasavyo sheria za kazi hupewa muda maalum (wiki mbili) wa kutekeleza sheria hizo. Jumla ya taasisi 20 zilipewa notisi na hatimae kurekebisha kasoro zilizobainika wakati wa ukaguzi ikiwemo kuwapa wafanyakazi wao mikataba ya kazi inayozingatia sheria.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua nyengine ni kufatilia suala hili kwa mwaka wa fedha 2016/2017, jamii imeelimisha juu ya sheria ya kazi ambapo jumla ya vipindi 29 (18 vya redio na 11 vya TV) vilirushwa kwa taasisi 29 za sekta binafsi zilipatiwa elimu ya sheria za kazi. Miongoni mwa elimu hiyo iliyotolewa ilikuwa ni kuelimisha wafanyakazi, waajiri na jamii kwa ujumla juu ya mikataba ya kazi, aina ya mikataba hiyo na umuhimu wake kama sekta inavyojielekeza.

Ushauri Nam.2. Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kupitia Idara ya Usalama na Afya Kazini, ihakikishe kwamba wafanyakazi wanapatiwa vifaa vya kujikinga na madhara wakati wa kazi, lakini pia kuwataka waajiri kuwasimiamia wafanyakazi waweze kutimiza wajibu wao huo. Hili litawezekana kwa kuhakikisha kuwa kuna kanuni maalum zinazowabana waajiri ili waweze kulisimamia suala hili pamoja na kuajiri wataalamu wa kutosha kwa ajili ya kufanya ukaguzi huo.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Idara ya Usalama na Afya Kazini inaendelea kufanya ukaguzi kwenye sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanafanya kazi katika hali ya usalama na inasimamia kuona kuwa mfanyakazi anapatiwa vifaa vya kinga kulingana na kazi anayoifanya. Katika kusimamia suala hili kwa ufanisi zaidi idara imetayarisha rasimu za kanuni zitakazowabana zaidi wahusika (wafanyakazi na waajiri)

kutekeleza suala hili kwa mujibu wa kifungu cha Sheria cha 116 (1) na (2) cha Sheria ya Usalama na Afya kazini, Nam.8 ya mwaka 2005. Rasimu za Kanuni tatu za usalama na afya kazini kwenye umeme, ujenzi na adhabu kwa makosa mbali mbali ziko katika hatua ya kupitiwa na Mwanasheria wa Wizara kabla ya kupelekwa kwa Uongozi wa Wizara na Wahusika wa Utatu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imefanya Ukaguzi wa Usalama na Afya Kazini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 katika taasisi 139 (Unguja 89 na Pemba 50) ikiwemo Viwanda, taasisi za Ujenzi, Mahoteli na Vituo vya Mafuta. Kila taasisi ilielekezwa vifaa vya kununua kwa kuwakinga wafanyakazi wake kwa mujibu wa kazi wanazozifanya. Mfano, Kiwanda cha Bakhresa cha Unga walitakiwa wawanunulie wafanyakazi wao '*safety boots'*, '*mask'*, '*dust coats'* pamoja na '*reflectors*.'

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa Idara inapata wataalamu wa kutosha imepanga kuajiri wataalamu wanane (8) wa fani ya (Sheria, Ukaguzi na Afya kazini kwenye mitambo, ujenzi, afya na mazingira ya kazi (*hygiene*) ambapo watapatiwa mafunzo maalum ya Usalama na Afya Kazini. Mpaka hivi sasa, wafanyakazi wawili wamepatiwa mafunzo ya Usalama na Afya Kazini katika kiwango cha Shahada ya Pili (*Masters*) na "*Post Graduate Diploma*". Pia, wafanyakazi wote wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi kuhusu Usalama na Afya Kazini.

Pia, Idara imeweka katika bajeti yake ya mwaka huu, ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufanya vipimo vya sauti, mwangaza, umeme, hali ya joto na baridi na hali ya unyevu wakati wa ukaguzi kwenye sehemu za kazi.

Ushauri Nam.3

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuhakikisha suala la kuwapatia bima ya afya wafanyakazi wote wa Sekta ya Umma linafanyiwa kazi kwa haraka iwezekanavyo.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, suala la Bima ya Afya hivi sasa linashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Afya. Hata hivyo, wizara imefanya mawasiliano nao ni kwamba andiko la nadharia '*Concept Note'* ya kuanzishwa Bima ya Afya tayari imeshapitishwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi. Hatua inayofuata ni kutayarisha Sheria ya Bima ya Afya ambapo Mswada wa Sheria ya kuanzisha Bima ya Afya Zanzibar tayari umepitishwa kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na umeshapitishwa na Baraza la Mapinduzi na sasa Mswada huo upo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kufanyiwa Marekebisho yanayostahiki na hatimae kuwasilishwa kwenye Baraza lako tukufu la Wawakilishi.

Ushauri Nam.4. Serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana,Wanawake na Watoto iandae '*data base'* ya Mahoteli yaliopo Unguja na Pemba ambayo itaonesha idadi ya Wafanyakazi waliopo katika hoteli hizo pamoja na asili yao, huduma wanazopatiwa. Kwa mfano, *ZSSF*, bima ya afya, kuwepo kwa mkataba wa ajira au na

kadhalika. '*Database*' hii inaweza kutumika katika kurahisisha ufuatiliaji wa maslahi ya wafanyakazi hao kwa ukaribu zaidi.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza ushauri huo, wizara kupitia Kamisheni ya Kazi ipo katika hatua ya kuanzisha *database* inayosimamia masuala ya kazi ikiwemo takwimu za Mahoteli. Hadi sasa hatua zifuatazo zimeshachukuliwa:-

- Imeshateua afisa maalumu atakaehusika na uwekaji wa takwimu zikiwemo taarifa za idadi ya hoteli zilizopo nchini; idadi ya wafanyakazi; aina ya mikataba kwa wafanyakazi na taarifa nyengine muhimu zitakazohitajika.

- Imetoa mafunzo ya ukusanyaji na uwekaji wa takwimu kwa maofisa walengwa ili kuweza kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

- Imenunua vitendea kazi ikiwemo kompyuta kwa ajili ya utunzaji wa takwimu hizo. Haya yote ni maandalizi ya kuanzishwa kwa *database* ya taasisi za kazi yakiwemo mahoteli.

Mhe. Mwenyekiti, pia wizara ipo katika hatua ya kukiimarisha kitengo cha Takwimu cha Kamisheni ya Kazi ili kiweze kuweka taarifa zote muhimu zinazohitajika kwa Kamisheni ya Kazi ikiwemo takwimu za taasisi za kazi na mahoteli. Hivi sasa inaangalia uwezekano wa kufanya tathmini ya Mahoteli yote yaliyopo Unguja na Pemba na kuzihifadhi takwimu hizo kwa njia ya '*Excel'* hadi hapo *database* hiyo itakapokuwa tayari.

Sekta ya Ustawi.

Ushauri Nam.1. Kamati inaishauri Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuhakikisha fedha zinazotumika kwa ajili ya kulipa pensheni jamii kwa wazee zinawekwa kumbukumbu sahihi zenye kuonesha matumizi halisi, ikiwemo idadi ya wazee waliosajiliwa, waliolipwa na ambao wamefariki. Utaratibu huu uwe unafanyika kila mwezi.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaishukuru kamati na watendaji wote kwa ushauri mnaotupa katika kuimarisha utekelezaji wa zoezi la Pensheni Jamii. Wizara inatumia utaratibu kama uliotajwa hapo juu ambapo taarifa zote hizo zipo na zinahifadhiwa ili kupata takwimu sahihi za matumizi halisi, wazee waliosajiliwa na waliofariki.

Mfano, katika Mwezi wa Julai 2017, Fedha iliyotengwa ni Tshs. 564,535,000 (Unguja 355,937,000 na Pemba 208,598,000). Wazee wote Unguja ni 17,289 (waliolipwa 16,170 na wasiolipwa ni 1,119) na Pemba 10,022 (waliolipwa 9,358 na wasiolipwa 664). Gharama za Uendeshaji ni 16,015,000 (Unguja 10,157,000 na Pemba 5,858,000). Wazee wapya waliojiunga na mpango ni 251 (Unguja 159 na Pemba 92) na wazee waliofariki ni

136 (Unguja 100 na Pemba 36). Huu ni mfano tu wa namna Wizara inavyohifadhi takwimu za pensheni.

Ushauri Nam.2. Kamati imepata taarifa kwamba kuna ukaguzi unafanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Pensheni Jamii. Hivyo, kamati inaitaka serikali kuharakisha ukaguzi huo na ripoti yake iletwe ndani ya Baraza la Wawakilishi. Vile vile endapo itabainika kwamba kuna watu wamehusika katika kufanya ubadhirifu wa fedha hizo hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itakapokamilika itawasilishwa kwa mujibu wa taratibu.

Sekta ya Uwezeshaji

Ushauri Nam.1

Kamati inaiagiza Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuandaa '*database'* ambayo itakuwa na orodha halisi ya wahusika wanaopatiwa mikopo, sehemu wanazofanyia kazi, maeneo wanayoishi, taarifa za malipo ya mikopo kwa kila mwezi, na kadhalika.'*Database*' hii itawezesha kutumika katika kuwafuatilia wadaiwa wakati wa kurejesha mikopo, pia kujua biashara inayofanyika baada ya kupatiwa mkopo, lakini pia kuweza kujua hali ya urejeshaji mikopo. Ambapo hii itasaidia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuwajua wadaiwa sugu na kuweza kuwaepuka wanapotaka kupatiwa mikopo kwa mara nyengine.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuthibitisha kuwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi una utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za waombaji na waliochukua mikopo kwa mujibu wa taratibu za taasisi za mikopo midogo midogo. Kumbukumbu tunazoweka ni katika madaftari maalum, mafaili na Maleja (*Hard copies*) pamoja na kopi laini (*Soft copies*) katika kompyuta. Aidha, wateja wetu nao wanapatiwa vitabu ambavyo vinaonesha mikopo waliyochukua, viwango wanavyotakiwa kulipa kila mwezi, marejesho waliyokwisha kuyafanya na kiasi cha fedha kilichobakia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ofisi, Mfuko una kumbukumbu za wateja wake wote, tarehe walioleta maombi, kiasi cha mikopo waliyoiomba, siku waliyofanyiwa tathmini na maafisa mikopo, siku kikao kilipokutana na kuyainisha maombi ya mikopo yao, viwango vilivyopitishwa na kamati ya mikopo, tarehe waliyopewa mikopo, namba za akaunti ambazo fedha hizo zimeingizwa, pamoja na kopi za mikataba ya wateja. Aidha, kwa sasa wizara inazidi kukiimarisha kitengo cha takwimu cha wizara ili kuweza kuweka taarifa zake zote sahihi. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 maombi 504 yalipokelewa ambapo kati ya hayo jumla ya mikopo 341 ilitolewa yenye thamani ya shilingi milioni 600 kwa watu 3,486 (Wanawake 1,944 na Wanaume 1,542) katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa za mikopo zinahuishwa (*up dated*) kila mwezi kwa maana ya kwamba mwisho wa mwezi kila mdaiwa wa Mfuko anaingiziwa ingizo lake ili kujua kiasi ambacho anadaiwa kufikia mwezi husika. Katika kumbukumbu tunazoziweka anaonekana kila mteja na jina lake, Shehia yake, Wilaya yake, mkopo aliochukua, kiasi anachotakiwa kulipa kila mwezi, jumla ya fedha aliyokwisha kuilipa, kiasi alicholipa mwezi husika na fedha anazodaiwa.

Ushauri Nam.2. Kamati inaitaka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kutoa mafunzo kwa wanaotaka kupewa mikopo kabla ya kutoa mikopo hiyo ili kuwapa muongozo sahihi wa jinsi ya kutumia fedha za mkopo kwa lengo la kupata faida na kuweza kurejesha mkopo.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa mafunzo kabla ya kuwapatia wananchi mkopo ni kuwa Muongozo wa Mfuko umeweka wazi kuwa kabla ya wakopaji kupatiwa mikopo, na mara tu mikopo yao inapoidhinishwa, basi mafunzo maalum hutolewa. Mafunzo hayo yanaitwa "*PRE LOAN Training*"- maana ni mafunzo kabla ya kupatiwa mikopo. Mafunzo haya kwa mwaka 2016/2017 yalitolewa kwa wakopaji 739 kati ya waliyoomba mikopo 1,000. Mafunzo hayo hujikita zaidi katika utaratibu wa kufanya malipo, umuhimu wa kuweka akiba, umuhimu wa kuweka kumbukumbu za mahesabu na udhibiti mzuri wa fedha. Pia wakopeshwaji wanapatiwa elimu ya masuala ya biashara mfano, masuala ya mitaji, masuala ya uendeshaji biashara, masuala ya masoko na masuala ya kujua faida na hsara.

Sekta ya Vijana

Usauri Nam. 1. Kamati inaiomba serikali kuhakikisha katika mwaka wa fedha 2017/2018 itenge bajeti maalumu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mabaraza ya Vjana.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2017/2018, serikali imetekeleza agizo hilo kwa kupitia Baraza la Vijana ruzuku ya shilingi 100 milioni ambapo zitatumika kwa shughuli za Baraza la Vijana Unguja na Pemba. Fedha hizo zitatumika kwa kutoa mafunzo na kuimarisha Mabaraza, kuyaunganisha Mabaraza na fursa mbali mbali zikiwemo za mikopo, ujasiriamali, ushiriki pamoja na kuanzisha miradi ya maendeleo.

Ushauri Nam. 2. Kamati inaitaka serikali kuitengea fedha Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, ili iweze kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi liliopo Mwanakwerekwe, ili Baraza la Vijana la Taifa liweze kupata ofisi ya kudumu na ya kutosheleza.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara ipo katika hatua ya kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi. Wizara imewasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango katika ukamilishaji wa ghorofa ya pili. Pindi litakapokamilika Baraza la Vijana nalo litapatiwa ofisi hapo.

Ushauri Nam. 3. Kwa kuwa idadi ya Mabaraza imekuwa kubwa sana, Kamati inaishauri serikali kufanya marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar, ili kuwa na Mabaraza ya idadi maalumu katika kila wilaya, kuliko kuwa na Mabaraza katika kila shehia. Hii itarahisisha ufanisi wa kuyaratibu hayo Mabaraza. Vile vile marekebisho hayo yazingatie changamoto nyengine zilizoonekana kama zilivyoainishwa hapo juu.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa na Mabaraza kidogo kutafanikisha utaratibu mzuri wa Mabaraza hayo, lakini kutakwaza ushiriki wa vijana wengi ambao wapo katika ngazi za shehia. Lengo la kuanzisha Mabaraza ya Vijana ni kuimarisha ushiriki wao katika nyanja mbali mbali za kimaendeleo kuanzia ngazi za shehia hadi taifa. Vijana wanaweza kupata fursa zaidi kwenye shehia zao kuliko katika ngazi za juu na ukizingatia hivi sasa serikali inatekeleza Sera ya Ugatuzi ambapo jamii inatakiwa kushirki kikamilifu katika fursa za kimaendeleo kuanzia ngazi za chini. Hivyo, mfumo huu wa Mabaraza unaenda sambamba na Sera ya Ugatuzi ya Serikali.

Sheria ya kuanzisha Baraza la Vijana Zanzibar ndio kwanza inaanza kutekelezwa hivyo, nadhani ni vyema tukaendelea kuitekeleza ili kuangalia kama kutajitokeza changamoto zozote nyengine tuweze kuzifanyia kazi kwa pamoja.

Ushauri Nam. 4. Ili kutatua changamoto za masoko, kamati inaishauri serikali kuandaa mkakati maalumu utakaowataka wawekezaji hasa katika sekta ya mahoteli ya kitalii kutokuingiza baadhi ya bidhaa kutoka nje ya Zanzibar, ambazo upatikanaji wake ni rahisi ndani ya Zanzibar. Kwa mfano, bidhaa ya kilimo na mifugo.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, sera na miongozo ya uwekezaji wa Zanzibar umeweka zuwio kwa wawekezaji kutoingiza bidhaa ambazo zinapatikana hapa Zanzibar ikiwemo bidhaa za kilimo na mifugo. Changamoto iliyojitokeza ni kwa kuwa bidhaa zinazozalishwa hapa kwetu zina changamoto ya kufikia viwango vya kimataifa vinavyohitajika katika mahoteli hayo, kwani wao wanatoa huduma kwa wageni zaidi, ni wafanyabiashara wachache tu wanaofikia viwango hivyo na kuweza kuuza katika mahoteli. Hata hivyo, serkali inaendela kuwashajihisha wananchi kufuata vigezo na viwango vinavyotakiwa ili kwenda sambamba na soko.

Ushauri Nam. 5. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuanzisha utaratibu ambao utatoa fursa kwa Mabaraza ya Vijana kuweza kupatiwa mikopo ili wajiendeleze na shughuli zao za kimaendeleo.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uzoefu tulionao katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, unaosimamiwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto unawapatia mikopo vijana wote wa Zanzibar na wizara inaahidi kuwa wale wote waliopo katika Mabaraza wanaohitaji mikopo na watakidhi vigezo vinavyohitajika, watapatiwa mikopo hiyo. Wizara inawaomba vijana wote wahamasike kuanzisha miradi yao ili waweze kupata fursa za mikopo.

Ushauri Namba 6. Kamati inaitaka serikali kuanzisha Sera na Sheria ambayo itawalazimisha wawekezaji katika sekta binafsi, kuweka asilimia maalum ya ajira kwa wazawa.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia wizara yangu imeupokea ushauri huo wa Kamati wa kuanzisha Sera na Sheria na itakaa na watendaji wa taasisi mbali mbali zinazohusiana na masuala ya Vijana na Ajira, Uwekezaji, Utalii, Taasisi za Sheria na Mamlaka nyengine za Umma na Binafsi ambazo zina wajibu mkubwa wa kukuza ajira kwa wazalendo ili kuangalia namna ya kuanzisha Sera na Sheria hiyo. Katika hatua ya awali, wizara inaendelea kusimamia programu ya mafunzo kazi kwa wanagenzi yenye lengo la kukuza ujuzi kwa vijana ili kuweza kuajirika, kujiajiri na kutengeneza fursa za ajira. Aidha, wizara itaendelea kushajiisha jamii juu ya kubadili tabia ili kuweza kuingia katika soko la ajira hasa katika sekta ya utalii ambayo inazalisha ajira kwa wingi hapa Zanzibar. Ili iweze kufanikiwa, kunahitajika umakini na mashirikiano makubwa baina ya taasisi mbali mbali za umma na binafsi ili kuwepo makubaliano ya pamoja katika uandaaji na upitishaji wa Sera na Sheria hiyo.

Sekta ya Wazee

Ushauri Nam. 1. Kamati inaitaka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuandaa utaratibu maalumu, ambao utakuwa na usawa wa huduma zinazotolewa kwa nyumba hizi, katika ubora, ili kuondoa dhana ya utofauti, hasa ukizingatia kwamba wazee hawa wote wana haki sawa mbele ya jamii.

Majibu

Wizara inalipokea shauri hilo la kuhakikisha kuna uwiano katika utoaji wa huduma kwa wazee na tayari imeanza kulifanyia kazi kwa kuwataka waratibu/wasimamizi wa nyumba hizo kuainisha gharama za mahitaji yote yanayotakiwa kwa mwezi na mwaka kwa mujibu wa idadi ya wazee waliopo katika kila makaazi ya wazee, ili wakati wa kupanga bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, kuwepo na bajeti yenye uhalisia kwa mujibu wa mahitaji.

Ushauri Nam. 2. Kamati inaitaka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuwapatia huduma wazee zinazoendana na gharama ya fedha zinazotolewa na serikali.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara inahakikisha kuwa inaimarisha huduma zinazotolewa katika nyumba zote za wazee zinazosimamiwa na serikali na huduma hizo zinaendana na gharama ya fedha zinazotolewa na serikali na kwa ubora unaotakiwa.

Ushauri Nam. 3. Kamati inaitaka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuhakikisha kwamba nyumba ya Limbani inawekewa uzio, ili kuwaweka wazee hao katika mazingira yaliyo salama.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, nyumba ya wazee Limbani tayari imeshawekewa Uzio.

Sekta ya Wanawake na Watoto

Ushauri Nam. 1. Kamati inaitaka serikali kufanya utaratibu wa haraka, ili kuwezesha kupatikana kwa mashine ya '*DNA'*, ingawa suala hili linajulikanwa kuwepo katika mradi wa *'Legal Sector Reform',* ambao '*DNA'* imepangwa kununuliwa katika awamu ya pili ya mradi huo, lakini Kamati inaona ipo haja ya kutafuta njia mbadala na ya haraka kwa sababu kwa sasa hali ni mbaya na inazidi kuwa mbaya. Kamati inapendekeza katika mwaka wa fedha 2017/2018 serikali kutenga fungu maalumu la kununulia kifaa hiki, ikishindikana njia hii basi serikali ipunguze baadhi ya vifungu vya fedha za bajeti kwa kila wizara ili kifaa hiki kiweze kununuliwa kwa haraka zaidi.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, serikali kwa kuona umuhimu wa kupatikana kipimo hicho, kupitia Wizara ya Afya imetenga fedha maalum kwa mwaka wa fedha 2017/2018, kwa ajili ya kununua mashine ya kupimia vinasaba (*DNA*) katika fedha za Mradi wa Maendeleo. Chumba kwa ajili ya kuwekea mashine hiyo tayari kimeshatayarishwa.

Ushauri Nam. 2. Kamati inaitaka serikali kuhakikisha kwamba wale wote wanaokiuka maadili yao ya kazi katika kulishughulikia suala la udhalilishaji wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

Majibu

Serikali kupitia taasisi zake mbali mbali zikiwemo za kisheria, inalifanyia kazi suala hili kwa kuhakikisha inaweka mifumo imara ya kuondosha mianya inayotumika ikiwa ni pamoja na kuzifanyia marekebisho sheria zilizopitwa na wakati kama vile Sheria ya Mahkama ya Kadhi, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Nam. 7 ya mwaka 2004, Sheria ya Ushahidi na Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004 ambapo sheria mbili za mwisho tayari zimeshapitishwa**.** Pia, serikali haitamvumilia mtendaji yeyote atakaebainika anakwenda kinyume na maadili yake ya kazi katika kulishughulikia suala hili kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na hayo, serikali imeanzisha operesheni maalumu kuanzia mwezi Machi, 2017 ya kusimamia uharakishaji wa usikilizaji wa kesi za udhalilishaji ambapo jumla ya kesi 139 zimesikilizwa na kati ya hizo kesi 28 zimetiwa hatiani. Pia, operesheni hiyo imekubaliana kuondoa dhamana kwa makosa yote ya udhalilishaji.

Ushauri Nam. 3. Kamati inaitaka Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, iandae programu maalumu ya kuwawezesha wazee pamoja na jamii kwa ujumla ni jinsi gani jamii itajikinga na matatizo ya udhalilishaji badala ya kuwaelekeza kuyatibu baada ya kwisha kutokea. Vivutio vingi ambavyo vimeanzishwa, vina lengo la kutibu tatizo hili badala ya kulikinga. Kwa mfano, Maafisa wa Ustawi wa Jamii, Vituo vya Mkono kwa Mkono, kuweko kwa simu za kuripoti matukio haya yanapotokea na kadhalika. Sheria, Kanuni na Taratibu zianzishwe kuwachukulia hatua wazee wanaowaacha watoto wao kushiriki katika starehe za usiku, wanaovaa mavazi yasiokuwa na staha na kadhalika.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara inakubaliana na Kamati kuwa, kwa muda mrefu kumekuwa na jitihada za kutibu au kushughulikia matukio ya udhalilishaji zaidi kuliko kuzuia. Kwa kuliona hili wizara imeandaa mpango wa miaka 5 wa kupinga vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto uliozinduliwa hivi karibuni ambao umejikita zaidi katika kukinga matukio yasiendelee kutokea. Hivyo, Mpango kazi huo katika maeneo yake makuu matatu kuna eneo mahsusi la uzuiaji (*Prevention*).

Ushauri Nam. 4. Kamati inaitaka serikali kuyafungia maeneo yote ya starehe ambayo yanaruhusu kushiriki watoto ambao wana umri mdogo na ambao bado ni wanafunzi.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaupokea ushauri uliotolewa pia itashirikiana na Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Jeshi la Polisi katika kulisimamia suala hili. Aidha, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja kulisimamia suala hili katika eneo lake na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inafuatilia suala hili kwa karibu sana.

Ushauri Nam. 5. Kamati inalitaka Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua za kinidhamu askari amoja na mzee yeyote atakayehusika na kuchukua hatua za kufuta kesi ya udhalilishaji. Kwa sababu kesi ya jinai ni kesi ya serikali, hivyo hakuna mtu mwenye mamlaka ya kuifuta kesi hiyo kinyume na utaratibu wa kisheria.

Majibu

Mhe Mwenyekiti, wizara inalifanyia kazi suala hili kupitia vikao vyake mbali mbali vya uratibu vinavyojumuisha Jeshi la Polisi kwa kukemea vitendo vya Jeshi la Polisi kuhusika na usuluhishi katika kuharibu ushahidi na kufuta kesi hizi. Jeshi la Polisi katika uzinduzi wa Mpango Kazi wa Miaka Mitano wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji lilitoa ahadi ya kuwawajibisha watendaji wa Jeshi la Polisi wote

watakaokwenda kinyume na maadili na viapo vya kazi zao kwa mujibu wa sheria. Pia, wizara inaiunga mkono hoja hiyo pamoja na kusisitiza mashirikiano baina ya taasisi za sheria, Jeshi la Polisi na wizara yataimarishwa katika kusimamia utekelezaji wa kesi hizo na inatoa wito kwa jamii kuripoti haraka matukio ya udhalilishaji na ukatili pamoja na kuwa tayari kutoa ushahidi kwani ndio muarobaini pekee wa kuharakisha uendeshaji wa kesi hizi.

Maswali ya jumla yaliyojitokeza

Kuhamishwa kwa bi Sada Abubakar Abdi

Ushauri Nam. 1. Kamati haikuridhishwa na hatua hiyo iliyochukuliwa na Katibu Mkuu wa izara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na inaiagiza Wizara kumrejesha mama huyo katika eneo lake la kazi kama kawaida.

Majibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba kufanya Marekebisho ya jina kwamba si Bi Salama bali ni Bi Sada Abubakar Abdi. Napenda kukuhakikishia kuwa uhamisho wa Bi Sada Abubakar ulikua ni wa kawaida wenye lengo la kuongeza ufanisi katika maeneo yetu ya kazi. Pia, tunapenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, wizara haijawahi kumuandikia barua za shutuma mfanyakazi huyo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Maryam Thani Juma (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kusoma hotuba ya maoni ya kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati kwa mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru tena Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu aliyeumba Mbingu na Ardhi, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu, tukitekeleza majukumu yetu mbali mbali ya kuwatumikia wananchi wetu ambapo leo tuko ukingoni kuhitimisha kujadili Ripoti za Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati zako kwa Mawizara.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kusoma maoni ya kamati kuhusiana na hoja iliyopo mbele yetu hivi sasa, kwa ruhusa yako naomba unistahamilie kidogo na uniruhusu nielezee hisia za kamati kutokana na kuendelea kwa wimbi na ishara za vitendo viovu katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, bila shaka wengi wetu tumesikia habari mbaya kabisa zilizozagaa katika kipindi hiki hasa vitendo vya ukatili, udhalilishaji wa wanawake na watoto,

mapenzi ya jinsia moja na matumizi ya dawa za kulevya. Kitendo cha kutekwa na hatimae kusababisha kifo cha kutatanisha cha mtoto Arman Hassan Mohammed huko Fuoni Meli Tano, mwanzoni mwa wiki iliyopita ni muendelezo wa vitendo viovu na vya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, hali inazidi kusikitisha zaidi baada ya kusikia habari za kukamatwa kwa watu waliokua katika sherehe "*Birthday*" ya Mashoga huko Fuoni pamoja na nyengine katika Ukumbi wa Wazee Sebleni. Mhe. Mwenyekiti, ni hatari na jambo la kufedhehesha kabisa kuona kwamba vitendo kama hivi sasa vinaanza kutendeka katika Taasisi za Serikali.

Kamati yangu inaamini kwamba vitendo hivi vimeshamiri katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, hivyo sote kwa pamoja tuunganishe nguvu zetu kuvipiga vita na hatimae kuvitokomeza kabisa vitendo hivi ambavyo kwa kiasi kikubwa vinachangia katika suala zima la udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inashauri kuangaliwa upya na hatimae kuikata kabisa misingi ya udhalilishaji na vitendo hivi vya udhalilishaji vikiwemo:-

- Kuongezeka kwa kasi kubwa kwa kumbi za starehe katika maeneo yetu,
- Baa za mitaani,
- Mitandao ya kijamii isiyodhibitiwa,
- Kumon'gonyoka kwa maadili,
- Visingizio vya sherehe mbalimbali zisizodhibitiwa kama vile *"Day Out*" , "*Birthday'* na 'Kibuki' nakadhalika.

Aidha, Kamati yangu inatoa wito kwa jamii kuwa waangalifu na kuwa makini na mialiko ya sherehe wanayopewa hasa kwa watoto kwani miongoni mwa mialiko hiyo, mambo yanayofanyika si mazuri hata kidogo katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Baada ya kilio hicho cha kamati, sasa turudi kwenye hoja iliyombele yetu ambapo kwa mujibu wa maelekezo ya Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2016 naomba tena kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi imepitia Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yetu ya Mwaka 2016/2017 kwa wizara yake nyengine inayoisimamaia ambayo ni Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii adhimu kumpongeza sana Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Vijana Wanawake na Watoto pamoja na Naibu Waziri Waziri ndugu Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Wakurugezi wote, Kamishna wa Kazi pamoja na Wafanyakazi wote wa wizara kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa katika kupitia kazi zetu za kamati.

Aidha nichukuwe fursa hii kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa mashirikiano yao mazuri waliyotupa mwanzo hadi mwisho na kupitia maagizo haya kwa wizara hii. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1.	Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	Mwenyekiti
2.	Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Maryam Thani Juma	Mjumbe
4.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
5.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mjumbe
6.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7.	Mhe. Mussa Foum Mussa	Mjumbe
8.	Ndg. Himid Haji Choko	Katibu
9.	Ndg. Mussa Issa Mussa	Katibu
10.	Ndg. Amina Abeid	Mkalimani

Mhe. Mwenyekiti, katika kazi za Kamati Mwaka 2016/2017, Kamati yangu ilitoa maagizo takriban (23) kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ambapo kwa ujumla, kamati imeridhika na Utekelezaji wa Maagizo hayo. Hata hivyo, juhudi zaidi zinahitajika ili kupunguza changamoto mbali mbali zinazoikabili wizara hii.

SEKTA YA KAZI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu iliiagiza wizara kufuatilia kwa karibu suala la upatikanaji wa Mikataba ya kazi hasa katika sekta binafsi. Kamati inaipongeza wizara kupitia Kamisheni ya Kazi kwa kuhakikisha inafuatilia kwa karibu agizo hili na hatimae jumla ya Mikataba ya kazi 2,301 katika sekta binafsi imethibitishwa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017.

Hata hivyo, Kamati inaamini kwamba bado kuna maeneo mengi Kamisheni ya kazi inashidwa kuyafikia kwa ajili ya ukaguzi kazi, hivyo Kamati inadhani kuna umuhimu wa kuongezewa Bajeti kwa Kamisheni hii ili iweze kufikia taasisi nyingi zaidi na hatimae kuweza kutekeleza kwa ufanisi mkubwa agizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu agizo linalohusiana na Usalama wa Afya Kazini, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii inazidi kuishauri Wizara na Serikali kwa Ujumla kwamba, Rasimu ya Kanuni za Usalama na Afya Kazini alizozieleza Mhe. Waziri ziharakishwe ili ziweze kukamilika kwa haraka kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji sehemu za kazi.

Aidha, Kamati inakubaliana na Mpango wa Idara ya Usalama na Afya Kazini kwa kutaka kuajiri wataalamu zaidi wa fani tofauti watakaopatiwa mafunzo maalum ya Usalama na Afya Kazini, hatua ambayo ikikamilika inaweza kuleta mafanikio makubwa na kuhakikisha wafanyakazi wetu wanafanya kazi katika mazingira mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuangalia Suala la Usalama na Afya Kazini, sasa naingia katika Suala la Bima ya Afya kwa wafanyakazi wetu. Kwa kweli suala hili ni la muda mrefu, hivyo Kamati yangu inaziomba wizara zote zinazohusika na suala hili zishirikiane na zikae pamoja na hatimae waweze kulikamilisha ili wafanyakazi wetu katika sekta za umma na binafsi waweze kufaidika na bima hii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na *Database* itakayoonesha idadi ya Hoteli na Wafanyakazi wao, Kamati inaishauri wizara kuongeza kasi ya maandalizi hayo ili iweze kufikia katika hatua kubwa zaidi. Kwa kweli *Database* hiyo itasaidia katika kurahisisha upatikanaji wa taarifa kama vile idadi ya mahoteli, idadi ya wafanyakazi na sehemu wanakotokea, mikataba ya Ajira na huduma wanazozichangia kama vile *ZSSF* na Bima ya Afya na mengineyo.

SEKTA YA USTAWI

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru na kuipongoza sana wizara kwa kuwa sikivu kwa kufuata ushauri wanapopewa hasa katika masuala ya malipo ya Pencheni Jamii. Hata hivyo, Kamati yangu inaiomba sana wizara kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kuhakikisha kwamba inaharakisha ukamilishwaji wa Ripoti ya *CAG* kuhusu Pencheni Jamii na hatimae iweze kuletwa katika Baraza lako tukufu kwa kujadiliwa.

SEKTA YA UWEZESHAJI

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imeridhia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yangu ya Mwaka 2016/2017 kuhusu Kumbukumbu za Mikopo pamoja na utoaji wa mafunzo kabla ya utoaji wa Mikopo kama alivyoeleza Mhe. Waziri kwa Sekta hii hivi punde. Aidha, Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeridhika juu ya Utekelezaji wa Maagizo yote ndani ya Sekta ya Wazee.

SEKTA YA VIJANA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imefurahishwa na hatua ya wizara kwa kutekeleza maagizo tunayowapa kwa asilimia kubwa katika sekta hii ya vijana, Suala la Bajeti pamoja na Utekelezaji wa Sheria ya Baraza la Vijana pamoja na Mikopo, linaonekana kuangaliwa kwa jicho la rehma na wizara.

Hivyo, tunaipongeza serikali kwa hili na tunatowa wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi wenzetu, pamoja na Viongozi wengine ngazi ya Mkoa, Wilaya, Jimbo na Shehia kuzidi kuwahamasisha vijana wetu kuibua na kuwa na mipango thabiti ya miradi yao ili kuzichangamkia fedha zinazotengwa kwa ajili ya maendeleo ya vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya soko kwa wajasiriamali wetu, Kamati inazidi kusisitiza kutekelezwa kwa sera inayoweka zuio kwa kutoagiza bidhaa ambazo zinapatikana hapa Zanzibar, ikiwemo bidhaa za kilimo na mifugo.

Aidha wizara ijitahidi kutoa taaluma kwa wazalishaji ili kuhakikiasha bidha zao zinakua za viwango na vinasindikwa vizuri ili vikidhi soko liliopo.

SEKTA YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inapongeza serikali kwa jitihada inazozifanya katika kuhakikisha mashine ya *DNA* inapatikana pamoja na kuweka mikakati ya kuondosha mianya inayotumika katika kuwabana wanaohusika na vitendo vya udhalilishaji hapa nchini.

Kamati inazidi kuzihimiza taasisi zote zinazoshughulikia masuala hayo zizidishe mashirikiano ili hatimae tuweze kutokomeza kabisa vitendo vya udhalilishaji katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia hotuba yangu Kamati yangu inazidi kusisitiza kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuzidi kushirikiana na Kamati yangu ili kufanikisha vizuri majukumu tuliyopewa na Baraza letu tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa kamati ya Wanawake, Habari na Utalii naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaanza na tunaendelea na mchagiaji wetu wa mwazo atakuwa ni Mhe. Simai Mohamed Said na atafuatiwa na Mhe. Ame Haji Ali ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata fursa hii leo kuweza kutoa mawazo yangu. Nimekuwa na hamu sana nikisubri ripoti ya hii kamati ambapo inagusa maeneo makubwa huku nikitambua kwamba ni moja katika wizara ambayo inawagusa wananchi wengi wetu katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba hasa kwa upande wa vijana ambao imekuwa ni kimbilio lao.

Lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa ripoti yake nzuri kusoma leo maagizo ni mengi amejaribu kufafanua kwa upande mwingi sana na nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati aliyesoma ripoti kwa niaba ya kamati yao. Kamati hii wamekuwa wanahangaika sana wanafanyakazi nzuri kwa mujibu wa taratibu na kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukuwe nafasi hii kukupongeza wewe kwa umahiri wako katika kipindi chote hichi sasa tumeanza kuona sasa uzoefu wako unazidi kupanda na Mwenyezi Mungu akujaalie *inshaallah* kwenye kitu hicho iko siku utakuja kuwa pia kuliko zaidi ya hapo, pengine kwa majina yale ambayo kama tunaita Mhe. Spika wetu *inshaallah*.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na Kamisheni ya Kazi. Kamisheni ya Kazi hii ndio yenye majukumu ya kisheria ya kusimamia maslahi ya wafanyakazi kwa upande wa Sekta Binafsi kwa upande wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kumeibuka mawazo au fikra nyingi sana juu ya suala zima la Sekta Binafsi na jinsi gani tunaweza kuboresha kwa upande mmoja ili kwenda kwa dhana ile ambayo ya *Public Private Partnership* au kuleta ukaribu karibu kabisa baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma.

Nimpongeze sana Waziri wa Biashara baada karibuni kuleta ile sheria ya kuonesha Baraza la Biashara huku nikiamini kwamba hii itakuwa ndio nafasi kubwa sana la

kuwafanya wawekezaji kuwa karibu. Leo asubuhi Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na maswala mawili matatu ambayo yalihusiana na maswala ya kazi na maslahi ya Wazanzibari kwa ujumla pamoja na wawekezaji. Kwa kweli majibu ambayo yalitoka leo asubuhi sikuyatarajia ambapo yalivyoenda hasa kwa Mhe. Waziri pale aliponita mimi kuwa ni Wakala wa Mzee Bakhresa. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri inawezekana kuwa aliteleza na nimshukuru kwa busara za Spika sikutaka kutumia kanuni lakini si vibaya mimi nikiwa kama *backbencher* nimkumbushe kazi za Mwakilishi na nitaomba ninukuu Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar ibara 88 inasema hivi:

> "Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongozwa shughuli zake kutokana na vifungu vya katiba hii itafanyakazi kwa mambo yafuatayo ya utekelezaji".

(a) Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo unahitaji kuwepo kwa sheria hiyo.

(b) Kujadili shughuli za kila wizara wakati wa kikao cha mwaka wa bajeti katika Baraza la Wawakilishi.

(c) Kuuliza maswala mbali mbali kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.

(e) Kuidhinisha na kusimamia mipango ya maedeleo ya serikali katika njia ile ile ambayo bajeti ya mwaka inaidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mzalendo na ni mpenzi mkubwa wa maendeleo ya nchi yetu na nina thamini michango ambayo inayotolewa na wawekezaji. Naomba ninukuu pia hotuba ya Mhe. Rais alipokuja katika Baraza letu hili kuzindua kwenye ukurasa wa namba 15 alitamka hivi kwenye uwekezaji wa vitega uchumi alisema:-

"Mhe. Spika, katika kuendeleza juhudi za kuvutia uwekezaji katika maeneo huru ya Uchumi ya Fumba serikali imefunga Mkataba na *Bakhresa Group of Company* ili kujenga miundo mbinu katika eneo ambalo mpango mkuu wa uwekezaji umeidhinishwa katika kipindi cha miaka mitano".

Mhe. Mwenyekiti, sisi wengi tunafaidika na matunda ambayo Mzee Bakharesa amejenga katika bandari yetu na sasa hivi anaelekea kule Pemba na mji ambao ameujenga na boti nyingi ambazo anazo. Kwa hivyo, mimi sina budi nikiwa Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tunguu kuunga mkono juhudi za serikali na kipenzi chetu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jinsi ambavyo na ukarimu wake na kuweza kumpokea mzee Bakharesa kuja hapa. Malengo yangu haya nataka niseme kitu kimoja hata ukienda katika ripoti yake yeye namba 6 amemtaja Kampuni yake ya Bakhresa anasema kwamba kwenye ripoti yake ukurasa namba 6 anasema kwamba:

" Wamefanya ukaguzi wa usalama afya kazini kwenye kiwanda kama cha Bakhresa."

Sasa na mimi nimuulize na yeye je, ni wakala wa Bakhresa maana yake kuna viwanda vingi tu hapa Zanzibar mbona hatujaviona kuvipitia. Kwa hivyo, nimwambie tu kwamba wakati mwengine unapoteleza si vibaya lakini ni vizuri tukaheshimu wale wawekezaji ambao ni wazalendo.

Lengo langu mimi ni kusema hivi. Mimi namtetea mzee Bakhresa kwa vitu viwili.

1. Jinsi alivyo-*create* ajira.

Nakumbuka mara moja nilikuwa na mzungu mmoja ambaye alikuwa ni *consultant* wa Wizara Fedha nikamuuliza katika wawekezaji wote Afrika Mashariki ni nani unaempenda sana akasema hakuna kama mzee Bakhresa. Nikamuuliza kwa nini kasema kwenye suala la ajira tu.

Sasa mimi Mhe. Mwenyekiti, viwango ambavyo vimetangazwa na Mhe. Waziri bado vinaleta ukakasi katika sekta ya ujenzi, sekta ya uwekezaji pamoja na katika sekta ya Utalii na waziri mimi ningemshauri kitu kimoja tu hapa.

Hili lina sehemu mbili la kwanza anahitaji kutumia busara na kutumia nguvu na watu ambao wamo katika wizara yake ili kuunganisha nguvu pia kuangalia wapi pana kasoro tuweze kwenda nazo pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye ukurasa 142 inasema hivi:

Kuihamasisha jamii kushiriki katika utalii wa ndani na kutoa mafunzo kwa vijana 680 ili kuwawezesha kujiajiri wenyewe kupitia sekta ya utalii. Lakini pia kutengeneza ajira laki moja za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida ya sasa hivi palipo ni vigumu sana kwa wafanyabiashara au wawekezaji kuendelea kuwaingiza watu katika Sekta ya Utalii. Kwa sababu biashara hii ni ya msimu, mimi nimefanyakazi muda mrefu sana katika sekta hii lakini pia nimekaa katika Bodi na taasisi tafauti katika kushiriki mikutano mingi. Sasa waziri ninapompa ushauri anahisi namlenga yeye moja kwa moja.

Mimi napitia kwa kupitia mlango wa wizara kuishauri serikali ili kujenga hoja wapate kuagalia kwa upana ni nguvu zipi tunaweza kutumia kwa pamoja ili kuleta umakini katika jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi katika sekta ya utalii ukiangalia mahoteli ambayo ni makubwa na madogo, wanapomaliza katika mwezi wa Novemba, wale wanamaliza mikataba yao ambao walikuwa waingie katika mikataba ambayo ni ya *permanent* au ya kuongezwa muda inakuwa ni vigumu sana wale wale kurudi. Lakini na vibarua pia wale ambao ni *unskilled labour* walikuwa wanafanya kazi kwa masaa mawili wakilipwa shilingi 10,000 mpaka shilingi 15,000 wawekezaji sasa hivi wamelazimika wawalipe shilingi 25,000 na 30,000. Sasa wengi wao wamefekwa na wengi hawa wanatoka katika vijiji vyetu, lakini sisi tunapotaka kulenga tunasema hapa tunahitaji tutumie upeo wetu ili

kuweza kuishauri serikali kuhakikisha kwamba tunatimiza yale malengo ya ilani, lakini pia tunawasaidia vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama utasoma Mkuza na kama utaangalia vision 2020, yale yote ambayo tumeyataja na vijana ukiangalia na tangazo la waziri wa kazi kwa viwango wameviweka tarehe 30, inavunja moyo kuangalia yote yale ambayo tumeyakusudia badala ya kusonga mbele tunarudi hatua nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu au niseme vitu viwili, tunataka tutumie nguvu kwa Kizungu nasema damage control. Sasa ili pakufanya haya ni kuangalia kuunda kamati ya haraka kuchunguza, je bidii gani zinaweza kufanyika ili kuweza kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo hapa, pamoja na Mhe. Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Juma Ali Khatib, maana yake amekuwa msikilizaji sana makini, yeye na amekuwa anafuatilia masuala haya kwa nguvu kabisa.

Kwa hivyo, mimi ninachoshauri katika kuangalia haya masuala ya viwango vya fedha baina ya muajiri na muajiriwa, tuangalie viwango ndani ya sekta ya utalii. Maana yake unaposema sekta ya utalii basi unagusa mahoteli, kuna mikahawa na kuna maduka. Tuangalie pia katika sekta ya ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali ilivyo sasa hivi ili kukiendeleza Kisiwa chetu cha Pemba ni vigumu sana kwenda kuwekwa miradi, kwa sababu unapotaka kufanya *feasibility study*, kuna kitu kinaitwa *ROI*, yaani *Return On your Investment*. Sasa unapotaka kuwekeza kwa upande wa masuala mazima ya wawekezaji sasa hivi, ukiangalia ajira na vibarua ambavyo utakuja kuvileta inakuwa ni vigumu kuiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, leo ukiiangalia Pemba kwa *speed* ambayo tunataka Pemba iende. Tuna hoteli kubwa nne. Tuna ile Mantariff, tuna The Ayana, tuna Misali, pengine tuna Apikilago na nyengine ndogo ndogo, pamoja na Fundo Lagun. Sasa kwa kasi ambayo Pemba tunataka ikuwe na kwa viwango hivi tulivyoviweka tutapata ugumu sana ili kuyapeleka maendeleo Pemba. Mimi nitashukuru sana wawakilishi ambao wanatoka upande wa Pemba waweze kulisemea hili, kwa sababu moja kwa moja tunataka Pemba iendelee hasa katika suala zima la *Ecotourism.*

Mhe. Mwenyekiti, katika sekta ya utalii unasema *labour intensive,* yaani unahitaji watu wengi ili wafanyekazi kwa ufanisi. Sasa Zanzibar tumefika pahala tunashindana katika huduma na visiwa vyengine kama Seychelles, Mauritius na maeneo mengine. Tukiwapunguza wafanyakazi katika huduma tutashuka chini, tukishuka chini ile hamu ya mgeni anapokuja Zanzibar tunasema ni *experience* itapungua, ule uzuri ambao mgeni anaupata, kwa sababu itabidi katika huduma utakuwa huipati ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika sekta ya ujenzi. Leo ukiangalia makampuni ambayo ni ya ujenzi pamoja na makampuni ya ulinzi, wengi watu wameanza kuwapunguza na hili ni la ukweli kabisa. Kama utafanya utafiti wa uhakika sasa hivi, ukiwauliza hawa wawekezaji katika sekta ya utalii, huyu atakuambia kapunguza 40, huyu 30 na huyu 15 na huyu 20.

Sasa ukichukua kama tuna hoteli 300 Zanzibar uki-*multiply by* 10 tayari watu 3,000 wameshatoka.

Sasa hivi leo niwaulize Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hili, hivi vijana wetu ambao tunawatarajia waingie katika ajira hatujisikii vibaya sisi kuona kwamba watu wanatoka kwenye kazi zao, hatuna huruma. Kwa sababu bora tuwe na wengi wako katika ajira kuliko tukawa tuna wachache hawa wengi wanaingia mitaani, wanapoingia mitaani ndio yale ambayo tunayakimbia tunakuja kukutana nayo. Kwa hivyo, mimi nashauri aunde kamati kwa nia njema kabisa kuwaangalia katika kila sekta ambazo zilizokuwepo kuna athari gani, lakini pia tuna miradi mikubwa ambayo itatekelezwa na sekta binafsi ambayo ni ya serikali na fedha zao zimeshapangwa.

Mmoja ni Mradi wa *Terminal II Airport*, wa pili ni barabara pia kutoka Fuoni kwenda Tunguu, na nyengine zote ambazo zimepangwa ndani ya ilani. Sasa hawa vibarua wote itabidi badala ya kulipwa shilingi 7,000, shilingi 10,000, waanze kulipwa shilingi 25,000, lakini fedha hizi zimeshatengwa. Ndio maana nikasema katika Uwanja wa Mau, sasa hivi vibarua wanalipwa shilingi 10,000. Waziri anasema kwamba atatumia utaratibu, hakuna utaratibu wowote wa kisheria unaomruhusu yeye baada ya kutangaza kiwango cha chini, kila mmoja anatakiwa alipe, kama kutakuwa kuna msamaha, utakuwa ni msamaha wa Mhe. Rais. Mradi wa serikali ambao unatakiwa utekelezwe na kampuni binafsi ni lazima ufuate tangazo lake. Kwa hivyo, ili ku-*rest situation* na kuangalia upana anatakiwa afanye kazi kwa ukaribu na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na Waziri wa Habari, Utalii na Michezo waunde kamati ili kuangalia uwezekano wa ku- *rest situation*.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimshauri kwa upande mwengine mmoja juu ya suala la kwenye ushauri wake namba 4, nikitoka katika suala la ajira, juu ya Mabaraza ya Vijana. Mimi nimpongeze sana kwa fedha ambazo tumempangia ni milioni 100, lakini bado hazitoshi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimshauri Mhe. Waziri kwamba atumie programu tofauti na kujenga ukaribu na taasisi za kimataifa za vijana, ili kupata hizi *group study exchanges*, lakini pia kuleta umoja baina ya nchi tofauti. Kuna uwezekano mkubwa kujenga uhusiano na nchi za Uganda ndani ya *East African Community.* Tuna wajumbe wetu sisi kutoka Zanzibar ambao ni Mhe. Mariam na Mhe. Dk. Abdalla Hasnuu Makame, aongee nao ni katika upeo wa nchi zetu hizi tano au sita za ndani ya Afrika ya Mashariki kwa kushirikiana ndani ya *SADC* kuangalia makampuni au taasisi ambazo zinaweza kuwasaidia vijana. Kwa kutegemea bajeti ya serikali peke yake haitoshi kutaka kwenda kwa kasi ambayo tunayoitaka. Lakini pia sio vibaya kuwasiliana na taasisi za kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, vijana ili waendelee wanahitaji pia kufungua akili yao na kupata *exposure* na kuweza kupata usafiri. Mimi namshukuru sana na nampongeza Mhe. Waziri kwa kumchukua Mwenyekiti wetu wa kamati yetu hii pia kufanya safari naye kwenda Ethiopia ni jambo zuri sana ameweza kujionea mwenyewe juhudi hizi ziendelee ndani ya kamati yake na kujenga ukaribu, huu ndio mfano ambao tunautaka. Kwa hivyo, mambo kama haya ni kwa ajili ya kujenga ufahamu mkubwa kwa vijana wetu uendelee pia kwa kuwapatia nafasi na fursa kutoka nje ya visiwa vyetu na kwenda nchi za nje ikiwa ndani ya Afrika au mabara mengine pamoja na Asia.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumzie suala la udhalilishaji wa watoto. Mhe. Mwenyekiti, hakuna kitu kikubwa kama ulezi, na kitu kikubwa ambacho waziri anatakiwa akisimamie Mhe. Mwenyekiti, ni suala la *parental guidance*, ulezi kwa watoto. Leo tunawakuta watoto wanakuwepo nje.

Mhe. Mwenyekiti: (Hapa Mwenyekiti, kampa ishara mjumbe amalizie mchango wake).

Mhe. Simai Mohamed Said: Mm! nimekuona mheshimiwa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimekuona namalizia.

Utawakuta watoto wanatembea mpaka usiku. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kama wazee hawatatimiza majukumu yao ya kuwalea watoto wao, utawakuta vijana wapo nje muda wa saa. Kwa hivyo, mimi nashauri tuendelee kutoa vipindi maalum ili kuwasaidia watoto wetu na wazee ili kuhakikisha *parental guidance* inaendelea, pamoja pia aangalie uwezekano wa kwenye mitandao, watoto ambao wako chini ya umri wa miaka 18 wasitumie hizi *smartphones*, wazee walinde kwamba mtoto atumie simu za kawaida, kwa sababu ndani ya *smartphone* kuna mengi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo niliyotoa na ushauri wangu, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa. Mwenyezi Mungu akubariki wewe, nampongeza sana Mhe. Waziri, naomba tuendelee kufanyakazi kwa pamoja, tupendane, tujenge umoja kwa nchi yetu. Lakini pia pale ninapompa ushauri anione mimi kama kijana wake, mimi wala sina tatizo naye tutaendelea kushirikiana naye kwa pamoja. Niahidi pia mimi nafanya kazi yangu kwa utiifu, kwa mujibu wa kiapo nilichokula kuilinda katiba yetu ya Zanzibar na dini yangu ya Kiislamu.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa uliyonipa, ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Ame Haji Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi naomba nichangie machache sana katika hotuba hii ya leo. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuniamsha salama nikiwa mzima na kufika kuja kufanya kazi hii ya wananchi kwa niaba yao.

Mhe. Mwenyekiti, nianze tu kwa kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia wananchi wake wa nchi hii. Kipekee nimshukuru Mhe. Rais kwa maamuzi yake ya kuwaongezea wafanyakazi wetu kima cha chini cha mshahara ili hali zao ziwe bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, Naibu Waziri wake pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya katika kutimiza majukumu ya kuiongoza wizara. Ila na mimi nina mchango mdogo tu katika hotuba hii ambayo imewasilishwa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze pale kwenye ukurasa namba 3 kwenye lile shauri la kwanza. Kamati iliishauri wizara wafuatilie uwezekano wa kutizama mikataba hasa katika sekta binafsi, mimi nianze hapa. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi ya kipekee na wizara basi ni eneo hili. Bado wafanyakazi wetu wengi hasa katika sekta ya binafsi hawana mikataba na wanafanyakazi ngumu, lakini kwa kweli maendeleo yao ni mabaya kwa sababu imekuwa ni kawaida, leo yuko kazini kesho anafukuzwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sekta ya hoteli kwa sababu kwa bahati njema miongoni mwa maeneo ambayo yana hoteli nyingi ni jimbo langu. Kwa hivyo, haya nitakayokuwa nasema hapa nayasema kwa niaba ya kuwawakilisha zaidi wananchi wa Jimbo la Nungwi na Wilaya ya Kaskazini A, na wamenituma hasa nije niseme haya ambayo nataka kuyasema sasa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kwamba wafanyakazi wengi katika hoteli zilizonyingi hawafanyikazi na mikataba haipo. Lakini jambo la pili, hata juzi nilipokuwa namuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza kuhusiana na suala la utaratibu huu wa nyongeza za mishahara aliyoitangaza kwa sekta hizi binafsi, pamoja na takwimu nyingi ambazo alinipatia lakini leo nataka niseme tena. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nungwi wananyanyasika sana katika mahoteli hivi sasa. Wafanyakazi hawa imekuwa sasa hii sera au agizo la serikali la kuongeza mishahara ni manyanyaso kwao. Wafanyakazi hawa wanatolewa makazini kila uchao. Narudia, wafanyakazi hawa wanatolewa kazini kila usiku unaokucha. Nami kwa niaba yao nawasemea leo na wanisikie huko waliko kwamba naiambia serikali juu ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kigezo wanachokitumia waajiri hawa kwamba wao hawana uwezo wa kuongeza mishahara kima kilichotajwa. Sasa kama hawana uwezo wa kuongeza je, wana uwezo wa kuwanyanyasa tu. Sasa kinachotokea Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba nafasi ambayo ilikuwa ina watu kumi hoteli basi watano wanatolewa, bila sababu, bila maelezo wala bila malipo. Wakishakutolewa hawa watano maana yake katika hoteli hiyo sasa wanabaki watano katika nafasi ile, kilichopo ni manyanyaso kwa sababu kazi ya watu kumi sasa inalazimika ifanywe na watu watano.

Mhe. Mwenyekiti, hii kadhia kubwa serikali yetu imetangaza kima hichi kwa nia safi kwa kuwalinda na kuwanusuru wananchi hawa wasinyanyasike, badala yake imekuwa ni tofauti. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri kwa dhati kabisa, kwa imani na kwa moyo wangu wa kuwatumikia wananchi kama kazi yetu ilivyotuleta humu, twendeni katika sekta hizi tukawanusuru wananchi walioko busara zitumike.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi kila uchao wananipigia simu wanataka kuja, nawaambia tulieni. Mimi ninafanyakazi ya kuwasemea na nitawasemea hili na vyombo vinavyohusika vitafika katika maeneo yenu kuja kuwasaidia. Lakini Mhe. Waziri katika kufanya hili ni lazima busara zitumike. Maana yake tunaweza tukaenda katika nia ya kuwatetea kumbe tunakwenda kuwachongea kazi. Kwa hivyo, ndio nasema kwamba busara zitumike katika kuwanusuru waendelee kuwepo kazini, lakini busara zitumike katika kuwanusuru waendelee kufanyakazi zao vizuri. Haya ni maagizo ambayo nimesema leo niyaseme katika kikao hiki, kikao halali cha kuishauri serikali yangu kwa niaba ya wananchi walionituma kuja katika chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri naongoza kwa Zanzibar kwa kuwa na mahoteli mengi, ila nilitegemea niongoze pia kwa kuwa na waajiriwa wengi katika sekta hii, lakini imekuwa tofauti. Kwa hivyo, naiomba sana serikali ilichukuwe jambo hili, ilifuatilie kwa karibu jambo hili kwa nia safi ili tuwasaidie wananchi hawa waendelee kuishi kwa amani, utulivu na upendo katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka leo nisimame na kusimama yangu hasa nilitaka nilisemee jambo hili na katika eneo hili na kwa uzito wake ili lichukuliwe hatua kwa maslahi ya wananchi wote wa Zanzibar na sio Jimbo la Nungwi peke yake. Pale katika Jimbo la Nungwi kuna watu wanatoka katika mikoa yote ya nchi hii, wanatoka katika kila eneo kutoka Zanzibar, Tanzania na kila mahali kuja kwa ajili ya ajira ambazo ziko pale. Sasa serikali tuwatendee haki wananchi hawa wote kwa kuwatetea haki zao kama ulivyowajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nilisimama kusema hayo tu kwa niaba ya wana Nungwi na kwa niaba ya wana Zanzibar wote. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa mchango wako sio mbaya ni mzuri, ni majukumu ambayo umepewa. Sasa ninamwita Mhe. Nadiri Abdul-latif Yussuf, akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismi llahi rahmani rahim, ninamshukuru Mwenyezimungu kunijalia uzima na sisi hapa kufika hapa wazima, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia ripoti ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na watu wote duniani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwenye wizara hii nina mambo matano tu ya kuchangia sio mengi. Jambo la mwanzo nitazungumzia suala la vikundi. Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwamba wizara inajitahidi kusaidia masuala ya vikundi. Lakini tuangalie vikundi vile vina wanyonge, utakuta si chini ya kikundi kimoja kina watu zaidi ya kumi au kumi na tano, kuwasaidia laki tano au milioni moja bado hamjafanya kazi. Ni vyema kabisa vikundi vyote mkaviita mkasikiliza vinataka kufanya nini, mradi wao utagharimu shilingi ngapi na ni busara kabisa mkakisaidia kikundi chenye *capital* kubwa mkakisaidia *capital* kubwa, na chenye *capital* ndogo mkakisaidia *capital* ndogo, ili vikundi vile visiwe kila siku kazi yao kuomba, vifanye kazi ili viweze kukua na wao waje kusaidia wenzao siku za mbele. Lengo kuu ni kusaidia wanyonge wa nchi hii, wananchi wa nchi hii ambao wanataka kujituma wao wenyewe kuliko kutegemea ajira za serikali na za sehemu nyenginezo binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, ninachoiomba wizara ni kwamba wawache kusaidiasaidia vikundi kwa fedha ndogo hawafiki kokote. Kikundi kina watu 15 kusaidiwa milioni moja, au milioni mbili, tukii-*divide* hiyo fedha ni fedha ndogo sana hawawezi kufanya kitu. Ukiwaangalia katika hao wote wana watoto familia kubwa. Kwa hivyo, ningeomba sana vikundi vyote viwe vinasaidiwa kwa mujibu wa hali halisi ya maisha tuliyokuwa tunayo hapa Zanzibar. Lakini naamini kwamba wizara inachukua juhudi ya kukaa na vikundi hivi kuvisaidia ni jambo zuri, lakini waendelee kuwafikiria kwa kuwapa *capital*

kubwa na kuwapa elimu zaidi ya kufanya biashara kubwa na sio biashara ambazo zilizozoeleka za mikate, sijui za kufanya kitu gani ndogo ndogo za kupata *income* ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la ajira, suala hili niwapongeze wenzangu wote walioanza kuchangia kuhusu suala la ajira. Lengo na madhumuni tunazungumza kila siku kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiwezi kuajiri watu wote, inachukua jitihada za kutosha kuweza kuajiri kwa wale wanaoweza, lakini wasioweza ndio maana wizara yako ikapewa mzigo pamoja na wizara nyengine kuweza kuangalia vipi watawasaidia wananchi. Lengo la Mhe. Rais kuzidisha mshahara wa kima shilingi 300,000/- ni jambo la busara sana na ni jambo zuri sana kwa upande wa serikali. Lakini tutambuwe serikali itabaki kuwa kama serikali na *Private Sectors* zitabakia kuwa ni *Private Sectors*. Tusijaribu kuziingiza *Private Sectors* na serikali ikawa ni kitu kimoja, uwezo wa serikali ni mkubwa lakini uwezo wa watu binafsi ni mdogo. Sasa waliyozungumza wenzangu yote ni mambo ya muhimu sana na ndio yameshatokezea si kama tunazungumza hapa kwamba tunataka tuombe, haya mambo yameshatokezea walioathirika ni Wazanzibari sana kuliko jamii iliyobakia.

Sasa tungeomba Mhe. Waziri kauli yako uliyoitoa uifikirie sana mara mia kwa sababu wanaoangamia ni Wazanzibari, sisi sote tunataka Wazanzibari wapate mshahara hata laki nne lakini kwa mujibu wa hali tulizokuwa tunazo na hivi *Private Sectors* haziwezi zote kulipa hizo fedha ambazo mmependekeza nyinyi, kuweni Serikali pandisheni vizuri tunapenda. Lakini *Private Sector* ziko kubwa na ndogo zipo ambazo unazosema wewe zimesha-*support* kauli yenu ya kwamba ilipwe laki tatu washaanza kulipa, zile zitakuwa zina uwezo wa kulipa lakini kuna *Private Sectors* hazina uwezo wa kulipa, matokeo yake Wazanzibari ajira wameshakosa wengi na kwa kitendo hichi hata mimi kuajiri kwa fedha hiyo kama nilikuwa na wafanyakazi kumi nitawabakisha watano niwalipe laki tatu lakini wale watano nawatoa kwa kukufuateni nyinyi lakini kwa kuwaumiza wananchi.

Lengo la Mhe. Rais ni zuri liendelee kwa Serikalini kwa sababu Serikali ina uwezo na imeshaweka *target* yake lakini kwenye *Private Sectors target* hiyo haipo, tungeomba sana kauli hiyo Mhe. Waziri ukaitafakari Mhe. Rais anakusikia jambo zuri sana kafanya lakini kauli yako ijaribu kuiondosha msilazimishe *Private Sectors* kwamba walipe laki tatu, wananchi wataumia bora walipwe laki na nusu lakini wapate ajira japo pesa ya chakula wapate kuliko kuja kukosa kabisa wakaanza kuingia kwenye madawa ya kulevya na wakaanza kudhurura tu kwenye vijiji. Hii hali ipo hali inaumiza na kama unataka kushuhudia haya kakae kwenye TVZ pale kama wanavyokaa wenzako siku zote watu wapige simu usikie maneno utakayopewa, kaeni kwenye mdahalo wewe na Naibu Waziri wako na Katibu mkuu muone hili jambo linaathiri vipi halafu semeni watu wapige simu musikie hizo *complain* ziko vipi.

Kwa sababu nyinyi mkisha kukaa kwenye TV wakati mwengine mnatangaza *order* ambayo mmeiandaa nyinyi si vibaya, lakini na nyinyi sasa kakaeni kwenye TV musikilize wananchi watakwambieni nini. Mimi naamini Mhe. Waziri unaniangalia na napenda sana ukiniangalia suala hili wanaoathirika ni wanao ikiwa wa kiume ikiwa wa kike Wazanzibari wewe ni Mzanzibari mwenzetu lakini ujue kwamba Zanzibar sasa hivi imeshaumia watu ajira waliosema elfu tatu pia kidogo, ukifanya uchunguzi labda elfu tatu kwenye masuala ya hoteli. Lakini ukichukulia maduka na sehemu nyenginezo basi ni

zaidi ya wafanyakazi elfu tatu wa Zanzibari wameshakosa ajira hapa Unguja ndani ya muda huu ambao umetoa kauli wewe Mhe. Waziri kuwa watu walipwe laki tatu. Tungeomba kauli yako uitafakari na *Private Sectors* zisilazimishwe ziweze kutoa kwa mujibu wa uwezo wao watu wapate ajira hali ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakwenda kwenye suala la malezi ya wazee, suala hili sasa hivi tunajiona kwamba Zanzibar tunataka twende na wakati, wazee wengi wamekuwa wanapenda mambo ya kizungu haya ndio matokeo sasa ya jamii inapoenda kuharibika, Wazanzibari leo ndio maana tunakuta wanawake wengine wanabakwa wanaume huvutiwa na mavazi wanayovaa kwa sababu wazee wenyewe wa kiume na kike haya mambo mmeshayataka. Mnawaachilia watoto wanaangalia *TV* mambo ya *fashion* na mambo ya michezo ya maajabu ajabu mnataka kuiga mambo ya kizungu wakati sio maadili yetu huku ndio tunakopotea.

Mhe. Waziri mimi ningetoa wito kwako wewe tena uzidi kupiga vita hivi vitu kwenye *TV* na kuelimisha wazee, wale wazee ambao wanajisikia wanataka kuwa na mambo ya kizungu basi wakahamie London huko sio Unguja, haya mambo Unguja tuna maisha yetu, tuna maslahi yetu, tuna hekma zetu hatuwezi kwenda kama mambo ya kizungu zungu wananchi wakaharibikiwa. Wazee wote ambao wanataka mambo haya ya kijamii ya *Western Country* kufuata wapaleke watoto wao. Lakini hapa leo tunakuta Mzanzibari hata baibui keshalisahau ni mambo ya maajabu sana na ndio mambo haya yanajitokeza sana sasa hivi, kubakwa wanaume wanavutiwa ndio maana wanafanya hivyo vitendo wengine wanafanya makusudi lakini vinasababisha hivi hivi mtu anavaa nguo ndani yote anaonekana unategemea nini Mhe. Waziri. Mhe. Waziri tungeomba kwamba uzidi kupiga vita masuala haya ili twende vizuri.

Lakini vile vile Mhe. Waziri nitakwenda kwenye suala la pencheni mimi nampongeza Mhe. Rais tena Dkt. Ali Mohammed Shein na Mweyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutumia hekma zake ambazo hawa wezee walikuwa hata hawapati elfu ishirini lakini wamejitahidi yeye na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kutoa shilingi elfu ishirini kuwapatia wale wazee fedha ya soda. Lakini ninachotaka kuzungumza kwamba fedha hii kwa mujibu wa maisha yalivyo na wazee halisi shilingi elfu ishirini kwa awamu tuliyokuwa nayo naamini ni kubwa kwa sababu walikuwa hawapati Mhe. Rais kawaonea huruma.

Lakini ningeomba Serikali ikafikiria angalau wazee hawa waje wapewe laki moja kwa mwezi baada ya elfu ishirini siku za mbele, kwa sababu elfu ishirini tuiangalie kila siku mimi labda natumia kadi ya simu elfu thalasini, elfu ishirini anapata mzee kwa mwezi mzima watoto wake hawana kazi sikatai ni fedha nyingi elfu ishirini kwa mtu aliyekuwa hana, lakini kidogo sana kwa mujibu wa maisha ya sasa hivi ningemuomba Mhe. Rais kabla hajamaliza muda wake hili ni ombi basi ataweza kutafakari kuangalia mfuko wake wa Serikali uko vipi basi angalau ikafika elfu 50, tukenda 100,000 tukatoa mafuta baadae tukawapa hata laki tatu wazee hawa kwa mwezi sio tatizo kikiwepo. Kama walivyoanza elfu ishirini kizuri kikubwa lakini tuzidi kuwazidishia kwa sababu hali ya elfu ishirini kwa hali ya maisha sote tunashukuru lakini ndogo kwa wazee hawa kupewa elfu ishirini huu ndio ukweli haya ndio maisha ambayo tunakwenda nayo.

Lakini naamini Mhe. Rais kwa busara zake na hekima zake kama alivyoanza na elfu ishirini ambayo hata mwanzo walikuwa hawaipati hii basi atafika elfu hamsini, laki moja na kuendelea mbele.

Mhe. Mwenyekiti mimi nilisema nitazungumza mambo matano tu kwa sababu Wizara hii sina uzoefu nayo haya ambayo nimeongelea kwa ajili ya jamii yanafaa, lakini kwenye suala la ajira ndio muhimu kuliko yote, suala la ajira lifikirieni watu msiwalazimishe kulipa mnavyotaka nyinyi Wizara, muweza kuwaambia tu kwamba fikirieni kuajiri watu zaidi watu wapate ajira lakini kima cha laki tatu kwa *private sector* wengine ni kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wangu maamuzi yake mazuri, kupandisha mishahara Serikalini, Serikalini fedha zipo lakini ukija kwa kina Nadir pesa hizo hazipo, usilazimishe Mhe. Waziri tunaomba sana ukae kwenye *TV* kwenye mdahalo siku hiyo na sisi utwambie tupate tukusikilize watu watakwambia nini uendelee na majukumu mengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada zake anazochukua anafanya kazi nzuri anajitahidi lakini vitu vyengine visije kumuangusha mimi namuonea huruma kwa sababu siku nyengine tutambadilikia na sisi hatutaki hayo. Sasa leo tunakuomba Mhe. Waziri, tunakupenda sana na Baraza linakupenda haya mambo yachukue yafanyie kazi changamoto hizi kwa wananchi, hatutaki vijana wa Kizanzibari waingie kwenye madawa ya kulevya walewe, wakae vibarazani waongee maskani kwa sababu kazi tunataka tuone wanapata kazi hata kama mshahara mdogo kazi wanayo baadae tutaangalia mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na ripoti hii naikubali asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia kidogo ripoti ya kamati ya Wizara hii ya Wanawake na Watoto. Awali ya yote nimpongeze sana Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada zake za makusudi za kuweza kuwapatia wananchi wake makazi mema na huduma njema kwa wale wote ambao wengine naweza kusema, kwa mtandao huu ambao wameuweka katika wizara ya Wanawake ni kwamba wasiokuwa na nguvu au wasiojiweza ambao wanaweza wakapoteza haki zao kutokana na kushindwa tu kuweza kujieleza au kuitetea haki yao.

Lakini kwa huruma za Dkt. Ali Mohammed Shein akaweza kuwatengea Wizara ili kuhakikisha kwamba wananchi wanatafutiwa haki zao hata kwa yule mtoto mchanga ambae amezaliwa akawa hajui lolote, kwa hivyo hili nimpongeze sana na Mwenyezi Mungu atamlipa fungu lake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na kuzungumzia kwamba Wizara hii kwa kweli ni Wizara kubwa sana yenye mashaka makubwa sana, lawama haziwachi na haya mambo hayeshi lakini kwa kweli wizara inajitahidi kadri ya uwezo wake, lakini kwa sababu mambo haya yanagusa jamii kwa kweli yanakuwa hayatokwisha kulalamikiwa. Mhe. Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni na haki yake mpeni, lakini kwa kweli Wizara inajitahidi katika kutufafanulia na sisi tunatakiwa tusiivunje moyo tunatakiwa tuipe

nguvu na tumsaidie Waziri pale ambapo amekwama kama nasi ni viongozi ambao tumekuja kuwatetea wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hii Wizara ina idara zisizopungua karibu sita (6) ina Wizara ya Kazi, Wazee, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto, kila unaloliona ni suala la malalamiko kwa kweli ni lazima tutafune jongoo kwa meno kumsaidia Waziri katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, suala la sekta mbili ambazo ni sekta za kazi Mheshimiwa sekta ya Serikali kama Serikali inajitahidi kujivua wenyewe au inajitahidi kujisaidia wenyewe katika kuwapangia wananchi wake kazi au shughuli pamoja na mafao yao kwa vile ninavyoona mapato ya Serikali na kwa vile inafaa, lakini tumsaidieni Waziri katika sekta za wafanyakazi binafsi. Kwa kweli hata hawa wafanyakazi binafsi na wao ni moja ya fungu la wananchi wa Serikali maana yake wananchi wote waliomo katika Zanzibar ni wananchi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale wanaitegemea Serikali hata kama mtu anafanya kazi binafsi, lakini anaitegemea serikali katika kumsaidia katika kupata haki zake na Serikali imefanya mambo mengi moja sasa hivi ni kumpandishia mshahara kwa mtu ambae ana kipato cha chini.

Mimi naona kuna suala zuri sana hili la kuweza kukaa tukalitafakari kama juzi Waziri aliposema, naamini juzi Waziri alisema maneno ambayo niliona yana haja hiyo. Serikali ina nia njema ya kupandisha mishahara kwa nia ya kusaidia wananchi wake, lakini kuna baadhi ya sekta bado ni ngumu ukizikazia sheria ukasema kwamba lazima sheria hii ifanye kazi pahali pengine panaweza pakaleta matatizo. Naweza kusema kama wafanyakazi walioko Pemba tunajua Pemba katika maeneo ya Micheweni tunaita maeneo huru bado shilingi elfu kumi na elfu tani ni pesa kubwa sana, hatojenga nyumba pale zaidi ya vibanda vya mgongo kwa sababu ukimwita mfanyakazi wa kukujengea nyumba atakambia elfu ishirini na tano mie sina, labda elfu tano au elfu kumi na akishitaki anaweza akakushitaki kisheria.

Lakini Waziri alizungumza juzi kwamba maeneo mengine tunayafanyia jitihada za kuweza kuangalia tufanyeje, mimi nilimsikia hapo juzi maneno aliyokuwa akizungumza na hilo ni neno zuri. Lakini unapoweka sheria, sheria inatakiwa iwepo kwa sababu kuna maeneo mengine elfu ishirini na tano ni ndogo inatakiwa ata iwe arubaini au hamsini. Lakini kwa sababu imeona Serikali ina lengo moja basi tutizame pale na kule kutakokuwa kuna mazungumzo mambo mengi yana mazungumzo kwa hivyo tunaweza tukayatizama, lakini sio kila jambo tukazie sheria kuwa itakuwa hivyo kwa sababu kuna baadhi ya mambo tukiyakazia sheria tutaweza kuharibu mtandao mzima ambao unakwenda.

Mheshimiwa katika kitabu cha Mhe. Waziri, naweza kusema karibu ukurasa wa kwanza mpaka wa tisa inaelezea suala la wafanyakazi, ikiwemo mambo ya bima, ikiwemo ajali kazini, ikiwemo kama walivyosema wanzangu kufukuzwa kazi kiholela holela yote haya yanamkabili waziri ambayo yeye siwezi kusema ni *computer* au ni kitu gani kwamba kila jambo ataelewa. Lakini ni kweli hii sekta imekuwa ngumu watu wanafukuzwa kazi sasa hivi mtu mmoja atafanya kazi kama punda atafanya kazi za watu wawili au watatu kwa pesa hiyo hiyo ambayo kiwango kimelipwa. Sasa kuna haja tusiwatizame wafanyakazi watupu tuwatizame na wawekezaji, tuangalie hili suala kwamba vipi linakwenda kwa

sababu huwezi kumlazimisha mtu kusema kwamba atakuwa ana wafanyakazi wangapi lakini lazima tuweke sheria ambayo itaweza kumzuia yule bwana kutokufanya mambo ambayo atakuwa anajiamulia mikononi mwake.

Suala ambalo anafukuzwa mtu kisheria hakuna tatizo kwamba mfanyakazi ni mtovu wa nidhamu ni halali yake kufukuzwa, lakini mtu anafukuzwa wengine wanakaribia kiwango chao cha kupokea pesa au kuna kiwango chao chngine chochote anamtafutia sababu anafukuza, haya lazima yatizamwe pamoja na bima za afya ziangaliwe mtu akipata ajali kazini hatakiwi tena, kwa sababu bosi anataka kazi yake iende anamtafuta aliye mzima. Kwa hivyo kuna mambo ambayo nimeona kwenye kamati karibu kurasa tisa zinamsemea mfanyakazi hasa wa sekta binafsi, tunashukuru katika humu nimeona sekta ya serikali haikutajwa inaonekana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar wafanyakazi wake inawajali na kuwajengea uwezo na bima vizuri sana, ka hivyo niipongeze Serikali kwa hatua hiyo. Lakini pia niiombe Serikali kwamba itafute juhudi za makusudi pia kuwawekea mikataba maalum na mizuri katika kazi za binafsi hili ningeiomba serikali iendelee.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni kwamba kuna hizi pesa za pencheni za Rais ambazo sijui tunaitaje lakini ni pesa ambazo Rais wa Zanzibar amejitolea kuwasaidia wazee waliokwisha kufikia umri, kama walivyokwisha kusema wenzangu pia *amount* ni ndogo lakini kweli na uwezo wa nchi yetu tunaangalia, kwa hivyo ningemuomba Rais akaangalia tu kama kutakuwa na uwezo wa kuongezea akawaongezea.

Lakini pili tutizame na umri Mhe. Rais atizame umri wa sasa kwamba miaka 60 ndio tumeweka kiwango cha kuwa mtu ameshakuwa mtu mzima, sasa Mhe. Rais kama atakuwa mfuko wake unajitahidi ashushe umri kidogo waswahili wanasema uwache tawi kabla hujakamata tawi, kwa hivyo akiliacha tu lile tawi la Serikali au la kazi akamate tawi la Mhe. Rais limburure burure. Kwa hivyo ningeomba Mheshimiwa kidogo akashusha chini umri ili na wale kidogo kwanza wengine hata hatuzifiki hizo pesa za Mhe. Rais tukazionja kwa sababu umri wenyewe unakuwa mashaka mashaka. Kwa hivyo ningeomba kidogo Mheshimiwa atushushie umri ili tuweze kuonja pencheni yake.

Nimuombe Mhe. Rais sijui hii inakuwaje katika mikataba yake akiondoka yeye sijui itabakia au ndio itaondoka, Mhe. Rais labda atuwekee mikataba hii isiondoke maana yake hichi ni kitu chema mwengine asije akaondosha, kwa hivyo ningemuomba Rais kwa sababu atakuwa ameshatuzoesha na huyu ajae basi afuate nyayo zake Mhe. Rais ningemuomba na hilo.

Lakini pia huu mfuko wa uwezeshaji Mhe. Mwenyekiti, Waziri namsikia siku nyingi muda mwingi tunazungumza huu mfuko wa uwezeshaji naona matatizo yake aliyoandika wengine malipo yao yanakuwa tabu, lakini nimeona hata *database* zake zinaonekana kidogo tuliuvamia huu mfuko na fikiri kwa *speed* ya maendeleo tukawa hatujaweka vitu vizuri baadhi ya watu wengine ambao sio waaminifu wameanza kupiga chenga na ile mikopo hailipwi vizuri. Kwa hivyo ningeomba lifanyike hilo lakini kama nilivyoona katika kamati Mhe. Waziri namuomba kwamba atafute vikundi vilivyokuwa vimeshajijengea uwezo katika mazingira ya kuwa vinataka kazi, wengine hujikusanya kwa minajim ya kutaka ule mfuko halafu wakishaula wala hatuwezi kuwafanya kitu wale

ni wananchi wetu lakini lengo ni kuwaendeleza ili na wenzetu nao wapate mafanikio zaidi.

Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kila mmoja anatakiwa kupata huu mfuko lakini kwa yule aliyekuwa tayari wameshakubali kutaka kujiwekea katika mikopo hii ambayo midogo midogo ili na wenzake wapate, wafanye warudishe na wenzao wapate. Kwa hivyo hili nilikuwa naliomba Mhe. Waziri alifuatilie zaidi.

Lakini Mheshimiwa nataka nizungumzie hili suala la Baraza la Vijana wakati mwengine tunailaumu Wizara lakini hebu tutizame Shilingi milioni mia moja, mie mwenyewe peke yangu hainitoshi sikwambii mabaraza yote ya vijana, milioni mia moja kwa mabaraza ya vijana ni pesa ndogo sana, lakini humu katika ripoti ya kamati pamoja na majibu ya Wizara ya uwezeshaji wamelizungumza vizuri, kwamba hili neno sio kwamba zigawiwe pesa na vijana wote wapewe hizi pesa ni ufuatiliaji na mikakati ambayo itawafanya wale vijana kuwaweka pamoja na kuwashajihisha katika mambo mbali mbali ikiwemo kuwapa mafunzo na mambo mbali mbali ya kujipanga katika kujiwezesha.

Kwa hivyo tunaing'ang'ania kwamba milioni mia moja iko wapi, lakini milioni mia moja hii ikishakufanyiwa hayo mambo ya watu wa Zanzibar wote vijana milioni moja pesa ngapi lazima tuitizame tumtizame na Waziri tutampiga masuala ya shilingi milioni mia moja kama tunamuonea. Kwa hivyo ningeomba Serikali hii iwe kama walivyozungumza wenyewe kwamba inaonsha ni muundo wa kuweka vitu katika kuwashajihisha vijana katika kuweka karibu na kuweza kuwapangilia mipango ya maendeleo karibu. Lakini sio kwamba ni mipango ya mikopo na kuweza kuwapa maendeleo kamili.

Lakini nilikuwa nazungumza suala Mheshimiwa katika kila sekta nimeona sekta ya ugatuzi kila sekta nimeona ugatuzi hofu yangu ugatuzi huko mwisho utafikia wapi, maana yake kila kitu ni ugatuzi kinakwenda kwenye katika wizara. Sasa sijui hiyo wizara ya ugatuzi mwisho itakuwa vipi mimi naihofia sana kutokana na muundo huu hali sijui itakuwaje huko mbele. Lakini Mwenyezi Mungu atatusaidia. Lakini kwa kweli ugatuzi umekuwa mwingi wizara zimekuwa nyingi hatma yake hatuijui, lakini hili naliangalia sana.

Mheshimiwa pia nataka nizungumze hizi huduma za wazee na watoto. Mheshimiwa naizungumzia Serikali kwamba ina jukumu la wananchi wake wote wa Zanzibar, waliopo katika Zanzibar kutokana na kuwasaidia kwa kila hali.

Mhe. Waziri, kuna wazee wana hali mbaya katika majumba wana watoto wana watu wao, kama ndugu lakini wazee wale wahawapati huduma yoyote zaidi ya kuyanyaswa, lakini mzee yule hathubutu jirani kusema hathubutu, matokeo yake yule mzee anakufa kiofisa na tai shingoni. Kwa kweli tuna haja Serikali itumie nguvu ikague kague baadhi ya maeneo kwenda kuwachukua watu wale wazee wale kwa nguvu bila ya kusikiliza wazee wao na watu wao ambao kwa kweli hawatendei haki.

Ana haki ya kuwa ni mzazi ana haki ya kuwa ni baba ana haki, lakini hawatendewi haki wakiwemo walemavu, wakiwemo wale tunawaita sijui wenye mtitindigo wa akili baadhi ya watu wale hawatendewi haki. Serikali kwa kweli ina haki ya kuwabeba kwa nguvu

kwa sababu mtoto anakuwa ni mtoto wa mama akiwa tumboni, akimtoa mtoto ni wa Serikali. Kwa hivyo Serikali lazima iwe makini katika kulitetea suala hili kwamba wamfahamishe mtu huyu mtoto si wako huyu mtoto wa Serikali kwamba asimdhalilishe, asimfanye kila kitu ana haki katika nchi hii.

Kwa hiyo ningekuomba waziri katika masuala kama haya ….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. malizia muda wako.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. nakuja namalizia kidogo najua muda mdogo..

Mhe. Mwenyekiti: Nakupa dakika moja.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sawa Mheshimiwa katika suala hilo hivi sasa tayari kuna watoto wadogo wadogo wa kile wenye umri wa miaka kuanzia saba, mitano mpaka kumi usiku unawaona wako kwenye maeneo kama ya chips kama eneo gani wanaomba, wakikutana na kibaka mtoto yule atakwenda kufanywa nini wapo tena peleka askari wako wakaguwe. Nimewaona na nikasema hawa sasa balaa lina kuja kwetu, kesho asubuhi atabakwa, lakini tatizo sijui hawana wazazi wale watoto, sijui lakini matatizo haya yameanza nikasikia watu wanasema hapa watoto hivi, lakini watoto wameanza sijui ikoje. Kwa hivyo Mheshimiwa hilo ningeliomba ulifuatilie.

Lakini Mheshimiwa nakuja la mwisho, nataka nikwambie kitu kimoja kuna watoto ambao tunawaita nisiseme wa haramu watoto waliokuwa baba zao tuseme hawakuoa au mama hakuolewa. Watoto hawa kwa utaratibu ninaokwamba kwamba kwa lugha yetu yoyote hakuna mwana asiyekuwa na baba njoo nae. Kila mtoto ana baba yake, yoyote yule hata kama kazaliwa nje ya ndoa ana baba yake.

Mheshimiwa kutokana na utaratibu wetu baada ya mama ukeshampa ujauzito unamwambia utajijua, hakuna kujijua, walipanga wakazungumza wakaeka sawa, serikali lazima iangalie tusichukue kwa sababu ya dini kwamba huyo mtoto atakuwa na madhara, serikali ina haki yake ya kumbana mtoto huyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Muheshimiwa namalizia tu kidogo .

Mhe. Mwenyekiti: Malizia kwa ufupi kabisa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Basi namalizia kwa sababu watakuwa hawaifahamu hii tu.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia kwa ufupi kabisa muda wako umekwisha.

Mhe. Suleiman Saharah Said: Mheshimiwa tunaleta DNA mama yeyote atakayekuja akasema mwanangu huyu baba yake fulani akapimwe na atakuwa amshughulikie

hajaambiwa arithi mali lakini amshughulikie mtoto yule. Kwa hivyo Mheshimiwa ningekuomba sana, Mheshimiwa nakushukuru sana naunga mkono hoja asilimia 100. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana kwa mchango wako na maoni yako, anayefuata ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Paje na baadaye atafuata Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti nikushukuru sana nami sitochukua muda mkubwa sana kwa vile ni Mjumbe wa Kamati hii naomba ku-*declare interest* na niliyasema mapema huko juu katika Kamati yetu, nitakapofika huku Kamati sitokuwa nayo pamoja nimeeleza mapema na Mwenyezi Mungu shahidi nilipoyazungumza maneno hayo.

Mimi sitochangia sana hoja yangu kubwa itakuja katika ukurasa 23, mwisho mwisho huku masuali ya jumla yaliyojitokeza kuhamishwa kwa Bi. Saada Abubakar Abdi, Mheshimiwa hilo ni suala la muda mrefu na tupo hapa kwa niaba ya wananchi kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza la Wawakilishi.

Baraza la Wawakilishi ni moja ya muhimili mkuu wa nchi na ndio muhimili pekee wenye jukumu la kutunga sheria za nchi na kusimamia shughuli za Serikali, Baraza la Wawakilishi limepewa kazi ya uwezo wa kufanya kazi kwa mujibu wa kifungu cha 88 cha Katiba ya Zanzibar cha mwaka 1984 kama inavyofanya marekebisho sheria za haki na kinga ya fursa ya mjumbe.

Mheshimiwa hapa pana vichekesho, tena vichekesho na sisi sote kwa kosa la mtu mmoja na sisi wengine tukaja kuonekana humu aa mimi siwezi, vichekesho, vichekesho. Bi. Saada huyu kahamishwa kwa mtazamo na macho maana yake kama picha haiyoni basi hata kuona hatuoni, Bibi huyu kahamishwa baada ya kushirikiana na Kamati ambayo kaiunda Mhe. Spika, kisheria kuhusu mtoto nani Ibrahim Abdalla, sasa hatukusoma basi hili na hili hadi tuone. Kamati ikaagizwa vichekesho vya hali ya juu ni vitendo vya ajabu, leo baada ya kutoa mashirikiano bibi yule ikabidi kuondoshwa kupewa uhamisho aaa hii si haki.

Kakaa karibu miaka 7-8 hajapewa hata barua ya onyo kwa kafanya kosa hili, kamtoa mtoto kapelekwa wizarani mtoto hakurudi inaonekana mtihani kwake kashirikiana na Kamati aa mimi hili nitalisimamia mpaka dakika ya mwisho. Kiakili kimtazamo basi mrejesheni baada ya mitatu minne mumhamishe angalau amri ya Kamati mmeitekeleza, kiakili na mtazamo wameitwa mashehe wameitwa mapadri kwa kesi hii, sitaki kuingilia kesi iko mahakamani sitaki kugusa huko Kanuni zetu zinatukataza, lakini kimtazamo kaondoshwa huyu bibi kwa kushirikiana na Kamati, tusitafute mengine tukatafuka mchawi mrejesheni bibi mtueleze sababu gani za msingi, maelezo mlojibu humu hee.

Kamati haikuridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto na inaangiza Wizara kumrejesha mama huyu katika eneo lake la kazi za kawaida, hilo ndio agizo la Kamati, majibu Mhe. Mwenyekiti, naomba kufanya marekebisho hili jina hata saa 9.00 za usiku ukiniamsha nalijua bibi hapa limeandikwa Bi. Salama bali ni bi Saada Abubakar Abdi napenda

kuwaarifu kuwa uhamisho wa Bi. Saada Abubakar ulikuwa ni wa kawaida wenye lengo la kuongeza ufanisi katika maeneo yetu ya kazi.

Pia tunapenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba Wizara haijawahi kumuandikia barua ya shutma, kipi kilichozidi haya ni maonevu na ni dhambi sasa hatuwezi kufanya kazi za Kamati hizi, hatuwezi kufanya kazi Mhe. Mohammed Aboud, wewe ndie msimamizi mkuu wa Baraza hili, hatuwezi kufanya kazi kama hatukupata mashirikiano. Leo katoa mashirikiano katika kwenye Kamati bibi huyu kenda kuhamishwa, sasa ukweli tutaujua wapi uongo tutaujua wapi kilichokuwepo Waheshimiwa Wajumbe bibi huyu kapewa uhamisho baada ya kwenda kumtoa yule mtoto akapelekwa kule wizarani mtoto hakujulikana alipokwenda mpaka leo, yuko wapi hajulikani usalama wake hatujui mtoto uko wapi ukweli uko wapi.
(Makofi)

Nilisema miye kwenye Kamati mimi ni mjumbe, lakini hili sitoweza kukubali kwa Kanuni nchini tuwelezeni, mimi mchango wangu ulikuwa mkubwa ni huo mrejesheni japo miezi mitatu minne angalau hii Kamati muiheshimu hamuwezi kufanya kazi peke yenu. Hii Kamati nzito, sasa mkajifanya nyinyi ndio wakubwa kuliko wajumbe sifahamu na kwa mujibu wa Kanuni tuko sawa sawa humu hakuna mkubwa hakuna mdogo humu ndani sote ni waheshimiwa.

Hivi yule wamrejeshe hakuna jengine lolote huwezi kudharau mchango wa mwenzio humu ndani. Bibi yule mumrejeshe, tena mnajifunga wenyewe humu ndani hakuiba, hajafanya kosa wanatoa uhamisho wa kawaida mbona miaka sita yote hiyo aliyokuweko hamjampa uhamisho wa kawaida baada ya kutokea hili aa, haielekei. Hiki ni kitu cha ajabu mno Bi Saada arejeshwe tusije tukafika pahali mkamsingizia mwizi, kafanya hivi mbona huko kote haikufika hatua kama hiyo, hili *no*, hili lirejesheni bibi huyu kwa kesi ya Mtoto Ibrahim Abdalla kumchukuwa mkampeleka halafu hamkurejudisha mkampa uhamisho aa ni vichekesho mimi siwezi kukubaliana nalo. Hili arudishwe ipasavyo bibi yule, kakaa miaka saba, miaka sita haijafika hatua hiyo na mnasema hata barua ya onyo hamjampa sasa huku tupitishe nini, tukubali wapi.

Mimi hili no sikubaliani nalo kabisa kama tutaendelea mimi nitaendelea kulisimamia na unaambiwa ovu utumie mambo matatu, mdomo wako, pili mkono wako na tatu ulichukie. Kwa hivyo, mimi naendelea kutumia mdomo wangu, mkono wangu na mwisho nitalichukia ili kumuomba Mhe. Spika, anihamishe kwenye kamati hii ndio la mwisho. Siwezi kufanya kazi kwenye kamati namna hii hata siku moja.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri Nam. 4. Kamati inaitaka serikali kufanya maeneo yote ya starehe ambayo yanaruhusu kushiriki watoto ambao ni wa umri mdogo ambao bado ni wanafunzi.

Majibu ya wizara. Wizara imepokea ushauri huo uliotolewa, pia itashirikiana na Wakuu wa Mikoa kama kuna mtu anastahiki pongezi ni Mkuu wa Mkoa wa Mjini. Bwana Ayoub Mohammed kafanya kazi kubwa mno na nimuombee aendelee kufanya kazi, amefanya kazi kubwa ya Mwenyezi Mungu mbali ya kuwa ni wajibu wake lakini atalipwa na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na mchezo sasa hivi hizi kumbi zetu zinakodishwa kwa nia njema lakini matumizi yanakuwa mengine. Mjumbe wa Kamati limetokea tatizo Sebleni Nyuma za Wazee, sijui kumefanywa *birthday* matokeo yake shughuli iliyofanywa nyengine. Kumbi hizi zinatumiwa kwa njia nyengine kinyume na maadili yetu ya Wazanzibari. Mhe. Mkuu wa Mkoa kafanya kazi moja kubwa ya ziada na malipo yake atalipwa kwa Mwenyezi Mungu, haielekei haya mambo yashazidi mno sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 20. Pia serikali haitamvumilia mtendaji yeyote atakayebainika kuwa anakwenda kinyume na maadili yake. Wizara hii tunayoichangia sasa hivi watendaji wakiwemo Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu hebu wakajitathmini wenyewe.

Jana nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri hapa lakini hakufahamu Kiswahili nilichokizungumza, wamekaa wakajitizama wenyewe mle ndani, utendaji wao ukoje, uadilifu wenu ukoje hebu jichunguzeni wenyewe. Huwezi kuwasha taa nje kabla ya kuwasha ndani ya nyumba yako ni makosa, kwanza taa unawasha ndani ya nyumba ndipo uwashe nje, jichunguzeni, jitizameni, jihakikini mjielewe.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze wizara, hapo kusema kweli wapewe ukweli wao ukurasa wa 19. Kamati Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, kuhakikisha kwamba nyumba ya Limbani inawekwa uzio ili kuweka wazee hao katika mazingira yaliyo salama.

Nyumba ya majibu hayo nyumba ya wazee Limbani tayari imekwisha jambo la kupongeza niwapigie kofi Mheshimiwa na haya wangeyafanya kwa Bi. Saada yasingewakuta haya, wangefanya kwa Bi. Saada yasingetokea haya sasa tuseme walichokifanya kipi maana hata kuona hatuoni hata ile picha hatuioni tungeyafanya kama haya kwa Bi. Saada wala yasingetokea nitaendelea kulisimamia hili mpaka dakika ya mwisho mimi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi ni mjumbe wa Kamati hii na nilisema mchago wangu hatokuwa mkubwa sana hii leo, kesi yangu iwe moja nije katika Kamati yangu kuongezeka kwa kasi kubwa kwa kumbi za starehe katika maeneo yetu baa za mitaani, mitandao ya kijamii isiyodhibitiwa, kumon'gonyoka kwa maadili visingizio vya sherehe mbali mbali zisizothibitiwa kama *day out*, *birthday* na kibuki na kadhalika.

Hii ni changamoto kubwa hapa Serikali ikakae ikajipange iangalie, Mkuu wa Mkoa peke yake hatoshi kufanya kazi ana majukumu mengi. Ndio kwenye Mkoa wake lakini nyie wizara mna majukumu, Mkuu wa Mkoa huu tutamvunja mabega halali usiku anafanya kazi ni mtu wa kumpongeza sana. Wizara hii ni majukumu yenu si kila kitu afanye Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi nafikiri, nifikie hapa hapa nielezwe kesi ya Bi. Saada lini atarudishwa ili nisiwe na matatizo ya Kamati yangu. Mhe. Mwenyekiti baada ya maelezo hayo naomba nikomee hapa kwa muda huu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa ni zamu ya Mhe. Hidaya na Mhe. Hidaya nitakupa dakika tano na Mhe. Omar Seif na yeye nampa dakika tano ili tuweze kumpa Mhe. Waziri naye kuweza kufanya majumuisho tumalizie kipindi chetu hichi cha saa hizi. Mhe. Hidaya karibu sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. mwenyekiti kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia machache juu ya Hotuba hii ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, juu ya utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima, lakini pia nitowe salamu za rambi rambi kwa vijana wote wa Zanzibar kwa kuondokewa na kijana mwenzetu Hafidh ambaye ni kijana ambaye tulikuwa tunamtegemea na kijana wetu jembe letu, katika Mikoa yote ambayo anatuwakilisha ndani ya Kisiwandui Ofisi kuu basi niwambie kwamba tunatoa mkono wa pole vijana wote na mikoa yote kwa wazazi wake, Mwenye ezi Mungu ailaze mahali pema roho yake peponi – Amin.

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenda kwenye Sekta ya Vijana, Mhe. Mwenyekiti kama unavyoniona umri wangu ni kijana na nimeingia ndani ya Baraza hili kwa niaba ya hao hao vijana wa Mikoa yote, kwa hiyo nitakuwa makini kuwasimamia vijana na kuyazungumza yale yote ambayo yanawahusu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati niipongeze sana kwa kazi kubwa wanayoifanya kwa kushirikiana na Wizara asilimia mia moja, kwa kuhakikisha mambo yote yanakwenda sawa, lakini Kamati hapa ilitoa maoni juu ya mabaraza ya vijana na Kamati iliomba kwamba ipatiwe bajeti na mabaraza ya vijana yapatiwe bajeti yao, na naishukuru wizara kwa kulipitisha hili na mabaraza haya kayapitishiwa bajeti ndani ya baraza hili, niipongeze sana kwa juhudi hii wizara lakini pia, niipongeze sana wizara kwa kulisikiza tamko la Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kuhakikisha kwamba vijana hawakai tu bila ya kufanya kazi yoyote.

Kwa sababu tuanaona hali ya nchi yetu ilivyo haina uwezo wa kuwaajiri vijana wote, lakini kutokana na moyo wa Rais wetu akaona kwamba kuna haja ya kutengeneza haya mabaraza ya vijana, ili vijana waweze kujisaidia wenyewe na waweze kujikwamua na maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti nimuombe sana Waziri, bajeti tumeipitisha kwa moyo safi ili vijana waweze kufanya kazi lazima wawezeshwe, ili hii bajeti ifanye kazi na hawa vijana waendelee kufanya kazi na kunufaika na haya mabaraza ya vijana, basi ingeiomba sana Wizara ikalisimamia suala la bajeti ili hizi bajeti zikafika kwa walengwa na wakaweza kuzifanyia kazi.

Mimi nafikiri vijana hawako tayari kuidanganya wizara wala kuidanganya Serikali, wakati watakapopatiwa hizi bajeti zikafika kwa wakati basi vijana watafanya kazi kwa nia safi na kwa moyo bila ya kumkera mtu, kwa sababu wataona kweli umuhimu wa kujaliwa lakini pia ule umuhimu wa kuonesha moyo na Mhe. Rais wetu basi nina hakika vijana hawa hawatalalamika wala hawatasema mambo mengine kwamba wao wanadharauliwa au la vipi.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Naibu wake lakini pia na Katibu wetu Mkuu wa Wizara hii malalamiko ya vijana yamekuwa mengi wanajua kwamba bajeti ilipitishwa na tayari ilikuwa imeshaanza kutolewa baada tu ya kuipitisha hapa, lakini tu muda mfupi bajeti haijulikani vipi nimuulize tuu Mhe. Waziri kuna nini ndani yake kama kuna lolote basi wafahamisheni vijana ili waweze kujua ukweli wa hili suala kwasababu ni mwezi wa pili sasa hivi hii bajeti inakwenda *wrong wrong* haifahamiki.

Mhe. Mwenyekiti, ningekuomba sana Waziri akahakikisha swali hili analisimamia ili kuwapa moyo na nguvu mabaraza haya ya vijana kuzidi kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na muda umenipa dakika tano lakini pia ningependa kulizungumza swali hili la Kamati pia wameiomba Wizara kwamba kuna haja kweli labda haya Mabaraza ya Vijana moja kwa moja yaende kwenye Wilaya, kutokana na ule msongomano mkubwa ulioko ndani ya mashehia lakini pia vile vile huko huko ndani ya Mashehi ya mabaraza haya ambako yalianzishwa tunaona kwamba kuna changamoto kubwa ambayo hayo mabaraza mengine hayajafika ile kiukamilifu huko ndani ya Mashehia. Kwa hivyo tunauhakika kwamba shehia nyingi bado hazina muongozo maalum juu ya Mabaraza ya Vijana lakini huu moyo ambao tutaupelekea ndani ya Mawilaya ikawa Wilaya ndio wasimamizi wakuu wa Mabaraza ya Vijana basi tuoneshe kihaki lilahi ili yaweze kufanya kazi mabaraza haya kwa kutetea na kuwasadia vijana waliomo ndani ya mashehia yote.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako nilokupa umemaliza.

Mhe.Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe.Mwenyekiti naiunga mkoni hotuba hii asilimia mia moja

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa nimwite Mhe. Omar Seif nikuombe na wewe utumie dakika tano na baadaye atamalizia Mhe. Naibu Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, tukishamaliza kusema hizi dakika tano zishakwisha na hatujamaliza basi hatusemi hata ahsante hatupongezi hatufanyi chochote maana dakika tano tunachangia kitu gani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Waziri lakini nitakuwa mkosefu wa fadhila kama nitasahau kumshukuru na kumpongeza Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kama ninavyozungumza kila siku ni Rais wa kupigiwa mfano, wazee wetu leo wamenufaika na imani yao kubwa wameirejesha kwa Rais wakiwa na matumaini kwamba ni mkombozi wao hongera Dkt. Shein hongera kwa imani yako, hongera kwa kila kitu ambacho unatuonesha kwa dhati ya nafsi yako kwa wananchi unaowaongoza wa Zanzibar.

Nazungumza haya kwasababu mimi sasa hivi nina miaka hamsini na mbili au hamsini na tatu lakini Dkt. Shein kadiriki kuwapatia wananchi hawa wazee pencheni ya pesa elfu

20,000/= iwasaidie, miye sisemi kama ni jambo dogo nasema ni jambo kubwa sana nani miongoni mwetu aliyekuwa anaweza kudiriki kutoa alfu 20,000/= tuu akasema nitaenda kutoa kama sadaka kupeleka, msikitini tunapitishiwa kofia wengine tunapitisha kwa nyuma michango ya misikiti.

Lakini yeye kwa kuona umuhimu huu ameona achangie hili mimi nakupongeza sana Rais Mwenyezi Mungu akupe kila la kheri na *Inshaallah* atakulipa kwa imani yako, atakulipa tu Mwenyezi Mungu mwenyewe anasema *Inallaha* hakika ya Mwenyezi Mungu *Lanudhiu ajirani Muslina* hazuwi wala hapunguzi ujira wa mtu kufanya wema Mwenyezi Mungu atamlipa kwa imani yake lazima atamilipa.

Lakini mimi niko hapo hapo nilikuwa na mengi ninayotaka kuchangia lakini umenipa dakika tano na zote nishazitumia sasa nakwenda kwenye ukurasa wa 10 hapo penye hayo mafao ambapo Kamati walianza ukurusa wa 9 kwa kuzungumza kwamba, Kamati imeagiza Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kuzihakiki fedha zinazotumika kwa ajili ya kulipa pencheni ya wazee na kuziwekea kumbukumbu sahihi zenye kuonesha matumizi halisi ikiwemo idadi ya wazee waliosajiliwa, waliolipwa ambao wamefariki kwa utaratibu huu uwe unafanyika kwa kila mwezi. Wizara ikajibu ikasema kwamba inaishukuru kamati na watendaji wote kwa ushauri unaotupa katika kuimarisha utekelezaji wa zoezi la pencheni ya jamii.

Lakini wakatoa mfano ya mwezi wa Julai mwaka 2017 wakasema pesa zilizotengwa ni 564,535,000/= Unguja milioni 355,937,000/= na Pemba milioni 2,598,000/= wazee wote wa Unguja wakiwa elfu 17,289 waliolipwa elfu 16,170 na wasiolipwa 1,119 na kwa Pemba 10,022 waliolipwa 9,000 na wasililipwa 664 na gharma ya uendeshaji wakaitaja hapo. Jumla ya hao wote wazee wakaieleza hapo ukifanyia hesabu wanakuja wazee kama 27,216 lakini hesabu hiyo hiyo ya 27,211 ukiigawa kwa pesa hizo milioni 564,535,000/= inakuja kila mzee anapata shilingi elfu 20,746/= sasa hizi 746 ukizigawa kwa mwezi ukuzizidisha kwa mwezi mara mwaka unakuta ni pesa nyingi, wangetupa uchanganuzi wa hili kwa sababu kamati ilitaka rekodi na mimi kutokana na uwelewa wangu mdogo wa mambo ya hesabu pia niliomba nipewe mchanganuo nipewe mchanganuo Waziri akija atupe machanganuo katika kujumuisha kwake kwa hili inakuwa ni hivi.

Lakini pia wameweka gharama ya uendeshaji mfano wasiolipwa katika kipindi hiki ni watu kwenye mwezi huo ni watu 1,683 ukizidisha mara elfu 20,746/= utapata ni shilingi milioni 34,915,518 kwa mwezi naomba mchanganuo. Waziri atupe kwenye Baraza ili na siye tujuwe ni vizuri na siye tujuwe kwamba aha likitokea hivi tunafanya hivi sasa hesabu kama hii ukifanya mara mwaka ziko ngapi ziko nyingi.

Mhe. Mwenyekiti: malizia hoja yako uunge mkono.

Mhe. Omar Seif Abeid: Maelezo mazuri. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako unamaliza malizia hoja yako uunge mkono. Mhe. Waziri wa Fedha kwa vile muda wetu hautotosha kumalizia naomba utengue kanuni ya muda ili tuweze kupata muda kuendelea zaidi.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile shughuli zilivyopangwa kufanyika asubuhi hii bado hazijakamika naomba tuweke kando kanuni ya 23 ili tuweze kuruhusu shughuli zilizopangwa ziweze kukamilika naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Mnakubaliana na hoja hiyo ya kutengua waliokubali wameshinda. Mhe Naibu Waziri naomba uendelee na kuchangia.

Mhe. Naibu Waziri wa Uwezashaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana kuweza kunipatia nafasi angalau ya kuweza kujibu baadhi ya hoja na baadhi ya hoja atakuja kujibu mwenyewe Mhe. Waziri mwenyewe atakapofika. Lakini kwanza naomba nichukuwe fursa hii kutowa mkono wa pole kwa familia ya kijana wetu Hafidh ambaye Mwenyezi Mungu amemuhitaji mbele ya haki tumuombe Mwenyezi Mungu amepeleke salama huko anakokwenda na awape subra wazee wake katika kipindi hiki kifupi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kwanza nichukuwe fursa ya pekee kuishuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari, Utalii ya Baraza la Wawakilishi kwa jinsi wanavyotupa maelekezo yao katika utendaji wao wa kazi na kutufahamisha na kutuelekeza nachukua nafasi hii kuwaomba waendelee na moyo huu wa kutuelekeza pale ambapo wanahisi inafaa kuelekezwa kwani tukiamini binadamu wote hatukukamilika.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mimi kama nilivyosema nitajibu tuu baadhi ya hoja nienze na Mhe. Simai Mohammed Said kuhusu suala zima la kuhusiana na fedha ya Mabaraza ya Vijana, amesema kwamba fedha iliyotengwa tu na Serikali ni kidogo nakubaliana nao kwamba ni kidogo lakini amesema kwamba kuna njia mbali mbali za wafadhili ambao wanaweza tukashirikiana nao wakaweza kuwasaidia vijana wetu hao basi nimuombe Mhe. Simai wakati yeye ni mdau mkubwa wa biashara tushirikiane ili tuone vijana wetu hawa nao wanasonga mbele katika maslahi yao ambayo wamejipangia.

Vile vile Mhe. Simai alizungumzia suala la udhalilishaji watoto kuhusiana na vipindi viendelee kutolewa nimuhakikishie kwamba Mhe. Simai tunashirikiana na Wizara ya Habari kuendelea kutoa vipindi hivi na mambo mengine mengi mengi ambayo tunahisi yanaweza kutoa ujumbe kwa jamii kuelimisha juu ya suala hili zima la udhalilishaji.

Niendelee na Mhe. Ame Haji Ali wa Nungwi yeye amesema suala la mkataba kwenye taasisi binafsi Mhe. Mwenyekiti naomba nikiri kama ni kweli ikiwa mimi mwenyewe nimeshafanya ziara kwenye sehemu taasisi mbali mbali nikiwa na Kamishna wangu pamoja na jopo zima la maafisa wa kazi tumegundua kuna matatizo ya mikataba na mambo mengine lakini nimuhakikishe Mhe. Ame tutalifuatilia suala hili kwenye Jimbo lake la Nungwi kwa maslahi ya wananchi wetu hawa kama alivyosema yeye mwenyewe kwamba busara iutumike ili waendee na kazi zao hawa basi nimuhakikishe kwamba Wizara naye kuhakikisha haki ya wafanyakazi hao inapatikana.

Nikija kwa Mhe. Nadiri yeye amezungumzia mambo mengi lakini amezungumzia mambo mengi lakini amezungumzia suala zima la vikundi kuhusiana kwamba vikundi vinaweza kuchangwa watu 12 na fedha wanayopewa ni kidogo, naomba kumuhakikishia

Mhe. Nadir kwamba utaratibu wetu wa kikundi unakuwa kikundi kina watu watano lakini vile na utowaji wetu wa pesa inategemea lile ombi kikundi ambacho kimeomba pesa zile kwa ajili ya kufanyia mradi wao wanaotaka.

Ikiwa mradi wako umemanisha pale Mhe. Mwenyekiti huwezi ukapewa mapesa mengi lakini mradi wako unahitaji fedha nyingi basi hatusiti kukupa fedha zile wakati tumefika sisi pale kuja kukukagua wewe mwenyewe kwenye kikundi chako na kujiridhisha kwamba kweli huyu tutapompa fedha zetu anauwezo wa kuzirejesha.

Halafu niendelee na Mhe. Suleiman Sarhan nimshukru sana Mhe. samahani nije hapa kwza Mhe. Nadir kwanza amesema suala zima la pencheni kwa wazee kwamba wanalipwa elfu 20,000/= fedha ni kidogo, nikiri kuwambia kweli ni kidogo lakini kwanza inapaswa nichukuwe fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa muono wake huo mtazamo wake huu wa kuona kwamba iko haja ya kuweza kuwawezesha wazee wetu hawa kila mwezi kupewa elfu 20,000/= sio jambo dogo ni na kushukuriwa na kumuombea hekima na busara na maisha marefu azidi kuwa na afya njema ili aweze kufikia yale malengo yake.

Lakini nimuombe Mhe. Nadir kwamba nimfahamishe kwamba Mhe. Rais ana nia njema na wazee hawa lakini vile vile na sisi kama wawakilishi inapaswa tusimamie suala zima la kodi yetu na mapato yetu ya nchi, tutakaposaidiana na Serikali katika kuziba ile mianya ya kupotea kwa kodi zetu hizi ma kushirikia sote kwa pamoja basi mapato yetu ya nchi yatakavyokuwa mazuri naamini Mhe. Rais ataendelea kuongeza fedha hii.

Niendelee na Mhe. Sarahan tunampongeza sana maana mengi aliyozunguza yeye ametuelekeza Wizara tunamshukuru sana lakini amezungumzia ombi la watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kuhusu huduma. Nimuhakikishie Mhe. Suleiman kwamba tutalichukua hili tutaliangalia na tutalifanyia kazi ili kama ulivyosema hakuna mtoto asiyekuwa na baba, isipokuwa hapa panakosekana mambo fulani, tutahakikisha kwamba wale watoto ambao wamezaliwa nje ya ndoa wazee wao ambao hawatoi huduma basi na wao wanastahiki kuwatunza watoto wale.

Nikitoka hapo naenda na Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye amesema suala zima la uhamisho mfanyakazi Bi Saada kwanza nataka nimuhakikishie Mhe. Jaku kwamba mfanyakazi huyu hakuondoshwa pale pengine kwa *interest* fulani au kwa sababu kwa maeneo yake anasema ameisaidia kamati hapana. Naomba nimfahamishe Mhe. Jaku kwamba uhamisho kwa mfanyakazi wa Serikali ni jambo la kawaida ikiwa ndani ya Wizara yako au nje ya Wizara yako wakati umo ndani ya Serikali ni jambo la kawaida na unapojaza mkataba wa kuajiriwa unajaza mkataba ule ukitambua wewe uko *time* yoyote wakati wowote kufanya kazi pahali popote hilo ndio lengo letu na wala hatukuwa na malengo mengine.

Lakini mwisho Mhe. Jaku amesema kujielewa baina ya Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wake nimhakikishie Mhe. Jaku kwamba Wizara tunajielewa tunajua nini tunachokifanya na Mwenyezi Mungu anatuona na hata Rais wetu anajua juhudi zetu tunazozifanyia kazi lakini zaidi kubwa anaitambua kujielewa kwetu ni yeye Mwenyezi Mungu Allah Subhana wa Taala sasa yeye Mhe. Jaku kama anaelewa zaidi kujielewa

kwetu hatusiti basi tunamuomba basi afike aje atufahamishe sisi hatukataii kuelekezwa kufahamishwa tukiamini binadamu mapungufu ndio sifa yetu.

Baadaa ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri sasa zamu ya Mhe. Waziri kujibu hoja.

Mhe. Waziri wa Uwezashaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima naomba nichukuwe nafasi kwanza napenda niwashukuru sana wajumbe nikushukuru wewe mwenyewe kwa kuweza kuwepo hapo na pia Mhe. Spika alikuwepo akaondoka.

Lakini nipende kusema tuu kwamba masuala haya mengi yamekuwa ni yale yaliyojibiwa ni kutokana na maagizo tuliuopewa tangu mwezi uliopita tukapewa muda mrefu kwamba yaletwe hapa kwa hiyo masuala mengi yamejibiwa mle. Sasa kama ni ufafanuzi wa ndani zaidi naendelea kuwakaribisha sana Ofisini kwetu tukikaa pamoja tukishauriana tukielekezana itakuwa ni vizuri zaidi.

Napenda nichukuwe nafasi hii kuwatambua wote waliochangia kwanza ni:-

1. Mhe. Simai Mohammed Said
2. Mhe. Ame Haji Ali
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf

Mhe. Mwenyekiti: Naam kuhusu utaratibu

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mwenyekiti kwa faida ya Hansard jina langu naomba litambulike ni Simai Mohammed Said sio Simai Mohammed Simai ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri mtaje jina lake.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Nasikitika kwamba Mhe. Simai huwa anapenda sana kurekebisha jina lake mara nyingi tuu sio kwangu kwa watu wengi na sijui kwanini huwa tunasahau utanisamehe nitaendelea kukumbuka wewe ni Simai Mohammed Said au siyo Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu.

4. Mhe. Suleiman Sarahan Said
5. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
6. Mhe. Hidaya Ali Makame
7. Mhe. Omar Seif Abeid

Napenda niseme tuu kwa heshima kubwa kwamba michango yenu inasaidia sana na kama mlivyokwishakiri wenyewe kwamba Wizara ya Wanawake na Watoto, Wazee, Vijana, Ajira na Uwezeshaji ni Wizara ambayo ina changamoto nyingi kwa sababu inagusa watu moja kwa moja ni Wizara ya jamii na nipende tu kushukuru Naibu Waziri wangu nadhani amenijibia karibu maswali yote. *(Makofi)*

Kwa hivyo sijui niseme lipi niache lipi isipokuwa niseme nikiri tu kwamba tutaendelea kushirikiana maswala ya ajira mnayozungumza kwenye nafasi za mahoteli tunaendelea kuzifuatilia hili ni jambo jipya kwasababu ni muda mrefu sana mishahara ilikuwa haijaongezwa sasa imekuwa ni kama jambo la kushitua lakini naomba wafanyakazi kokote muendelee kuvumilia tunaendelea kufanya kazi ili tuweze kuhakikisha mnapata haki zenu.

Lakini pia waajiri muliomba nafasi za kuweza kuwekeza katika nchi yetu mkiwa na mikataba na ahadi nzuri sana ndio maana mkakubaliwa kuwepo katika nchi kwa hiyo muendelee kuheshimu zile nafasi mlizopewa kwamba mumekuja kuwekesha nchi yetu tupate mapato kwa ajili ya nchi yetu, na haya yote anayosema tuongeze pesa haziwezi kuongezeka kama mapato hayapatikani na Serikali inaishi kwa kodi asiyetoa kodi anastahili sheria. Sasa naomba tushirikiane kwa pamoja tumeyachukua yote muliyosema na Mhe. Simai naomba uje Ofisini kwangu kwa mara nyengine tukae tukutane hayo unayopendekeza tuwasiliane, umesema sana haya masuala ya ajira na una nia nzuri najua na inawezekana labda na wewe ni muajiri au unawaza kuwa muajiri siku moja au mwekezaji, Mwenyezi Mungu atakubariki kwa sababu tunataka watu wanaotoka ndani ya nchi yetu watakuwa na uchungu zaidi kuliko hata watu wanaotoka nje.

Mwisho nipende kusema kwamba, masuala kama yalivyokwishasemwa hata nikisema nayarudia nitakuwa nayaharibu. Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri wangu amefanya kazi nzuri naomba tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo tu ilikuwa masuala ya walezi na watoto na tabia zinazojitokeza mitaani. Nataka kuwaambieni kwamba, mama Maudline Castico na wizara yake peke yake hawezi kuhakikisha jambo hilo limekwisha ni pale tutakaposhirikiana. Hili ni jambo la wazazi hawa watoto wanaokuja mitaani au wanatoka mahali popote wana wazazi wawili waliozaliwa nao, hakuna aliyetoka akateremshwa tu, vitabu tunaoneshwa kwamba aliyezaa katika njia zisizo sahihi ni mmoja tu labda, wawili au mmoja waliozaa katika jinsia moja, lakini wote wana wazazi. Kwa hiyo, wazazi tuwajibike kwanza. Vitendo vya ukatili vinaanza kutokea, kama hizi taarifa zilizotoka ni taarifa ambazo tumeletewa sasa, lakini zile tulizokuwa tumepewa tuzijibu awali tulikuwa tumeshaziandaa. Kwa hiyo, naomba wanipe nafasi nyengine ya kwenda kufuatilia kwa undani haya mambo yametokezea vipi.

Watu wanapokuja kuomba vibali kwenye maeneo hawaandiki wanakuja kuomba kibali wakafanye shughuli gani mule ndani, ni pale zinapofuatiliwa zikaonekana kwamba hazifai ndio zinapochukuliwa hatua. Kwa hiyo, niko pamoja na nyinyi na Mwenyezi Mungu awabariki tushirikiane kwenye majimbo, kwa sababu ndio mnaowajua watu wa majimboni, muwe karibu na watu wenu mukiwaambia nyinyi itakuwa rahisi zaidi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf alisema suala zima la mavazi kwa watu. Kweli mavazi inawezekana yanachangia lakini je, mtoto anayevaa *pampers* anabakwa kwa *pampers* yake? Naomba tusaidiane, mavazi ya mtoto mchanga anayebakwa kwa kuwa hajavaa vizuri, anabakwa kwa sababu gani? Naomba *altitude* zilioko ndani ya vichwa vya watu tuzibadilishe turudi kwa Mwenyezi Mungu tuogope, tumsaidie Rais wetu ametupa amani kusingekuwa na amani thubutu kama mtu angeweza kupata nafasi ya kubaka, akabake na

mitutu inacheza asingeweza kitu hicho. Kwa hivyo, naomba tushirikiane kasumba zilizoko ndani ya vichwa vyetu zikitoka tutaendelea salama na haya ni mambo tu nasema, tunawashukuru sana watu wa nasaha kwenye vyombo vya dini sasa hivi tunashirikiana nao kwa karibu sana, wanashauri, tunafundisha katika mashule na kila pahala. Kwa hivyo na nyinyi ninawaombeni wito wenu kwamba tushirikiane mkwakemee hao wapiga kura msiogope kura kusema kwamba tukiwasema sana hawatatupa kura, lakini kama wote wataharibiwa hata kwenye kura watakuja, watakuwa hawawezi kuja watakuwa na mashaka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba niseme ahsanteni sana kwa kunisikiliza na ahsanteni sana kwa kuturuhusu kuweza kusema haya. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana. Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu hoja nikategemea na waziri pengine ataijibu hiyo hoja Kanuni ya 59(3), Naibu Waziri alisema au sijui niisome hiyo kanuni ya 59(3) tupate faida wajumbe wasikie.

Mhe. Mwenyekiti: Soma hiyo hoja, lakini hoja tumeshaifunga hiyo sasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tatizo Naibu Waziri, *hansard* ikae sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa kitako. Sasa naomba niwahoji wale wanaoikubali hii ripoti ya Mheshimiwa, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Ahsanteni Waheshimiwa Wajumbe kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya ya kuweza kuipitisha hoja hii ripoti yetu ya Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nayo imekwenda vizuri na niwaombe kwa kumalizia katika shughuli yetu wale ambao muda huu ndio imemalizika tujitahidi kufika kwa wakati saa kumi na moja jioni. Hadi hapo naliakhirisha Baraza hili hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:04 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Wizara ya Fedha na Mipango - Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa hii inawasilishwa ili kulijuilisha Baraza la Wawakilishi hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati yake ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, uwasilishaji wa taarifa hii unalenga kutekeleza matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kama ilivyorekebishwa inayoitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwajibika katika Baraza hili tukufu. Naomba kunukuuu Sura ya Tatu, kifungu cha 43, kifungu kidogo cha 5 cha Katiba hiyo kinachotamka kuwa:

> "Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za serikali kwa ujumla na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine tunafungwa pia na Kanuni za Baraza letu hili juu ya uwajibikaji wa serikali katika Baraza kufuatia Ripoti za Kamati za Kudumu zinazotoa ushauri na maoni kwa mawizara mbali mbali. Kanuni ya 108(15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016 inaitaka kila wizara kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi mara moja kwa mwaka katika mwezi wa Septemba au Oktoba.

Mhe. Mwenyekiti, uwasilishaji huu wa ripoti za wizara mbali mbali na leo hii Wizara ya Fedha na Mipango ni muendelezo wa kutimiza matakwa ya Katiba yetu na Kanuni za Baraza lako. Kuheshimu huko kwa Katiba na Kanuni kunadhihirisha utekelezaji wa vitendo wa misingi ya utawala bora unaofanywa na serikali hii ya kipindi cha pili cha awamu ya saba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inayoendelea kutokana na kufanikiwa kwa Chama cha Mapinduzi kuiongoza serikali na inayoongozwa vyema na jemedari wake mahiri Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nimshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuniamini na kunipa nafasi ya kuongoza Wizara ya Fedha na Mipango ambayo leo hii nawasilisha taarifa hii, na kwa miongozo yake inayonirahisishia sana majukumu yangu na siku zote kunipa dira ya utekelezaji. Namshukuru pia Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais nae kwa kunipa msaada mkubwa katika kutekeleza majukumu haya niliyopewa na serikali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, siwezi kumalizia shukurani hizi bila ya kumshukuru sana Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika, Mhe. Mgeni Hassan Juma na pia kukushukuru sana wewe Mhe. Mwenyekiti pamoja na Mwenyekiti mwenzako wa Baraza hili. Kutoka ndani ya moyo wangu nashukuru sana mashirikiano yote mnayonipa mimi na wizara yangu ambayo yanasaidia sana kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya wananchi na nchi yetu. Kwenu nyote nasema ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeendelea kuundwa na wajumbe weledi wafuatao.

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe
5. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe
6. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe
7. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha - Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii nimshukuru Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati yako kwa mashirikiano ya dhati, mashauriano na maoni na ushauri wa busara lakini wenye weledi mkubwa wanaoendelea kutupatia katika wizara yetu. Wizara yangu ina deni kubwa kwa kamati hii kwa mashirikiano yake na miongozo ya kina inayotupatia, inayopelekea kuimarika kwa ufanisi wa utendaji wa wizara yangu na taasisi zake.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka uliomalizika wa fedha, kamati ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu iliyochukua jumla ya muda wa wiki sita. Katika kutekeleza kazi zake kamati ilipata fursa ya kutelembelea Unguja na Pemba kwa utaratibu ufuatao.

1. Mzunguko wa kwanza ulioanzia tarehe 29/08/2016 hadi 09/09/16. Kamati ilitembelea na kukutana na idara na taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara kwa upande wa Unguja.

2. Mzunguko wa pili ulianza tarehe 31/10/2016 hadi 04/11/2016. Kamati ilipata fursa ya kutembelea taasisi zinazosimamiwa na wizara kwa upande wa Pemba na kamati pia ilitembelea mashamba ya mipira ya serikali yaliyosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango yaliyopo Pemba. Mzunguko huu kamati ilihusisha pia kutembelea taasisi zilizo chini ya wizara kwa upande wa Unguja kwa ziara zilizofanyika kuanzia tarehe 07/11/2016 hadi 11/11/2016

3. Mzunguko wa tatu ulianza tarehe 16/01/2017 hadi 20/01/2017. Kamati ilitembelea na kupata maelezo ya shughuli za wizara kwa upande wa Unguja na baadaye tarehe 23/01/2017 hadi 27/01/2017 ilifanya kazi zake kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema katika ziara zote za kikazi zilizofanywa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo uongozi na watendaji wa wizara walifaidika sana na majadiliano ya kina yaliyofanyika na hatimaye maoni na ushauri mbali mbali wa kamati. Naomba kwa mara nyengine tena kuishukuru sana kamati yote chini ya uongozi wa Mhe. Yussuf Hassan Iddi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelekezo yaliyokuwa yakitolewa moja kwa moja wakati wa mizunguko ya kikazi. Pia kamati iliwasilisha maagizo 60 kwa wizara baada ya kukamilisha ziara yake ya mwaka wa fedha 2016/2017. Maagizo hayo yalilenga katika

taasisi, idara na miradi ambayo iko chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango kama ifuatavyo:

i. Maagizo 5 yalilenga usimamizi na ugomboaji wa madeni ya mashamba ya mipira;
ii. Maagizo 4 yalihusisha ufuatiliaji wa Maghala ya Serikali;
iii. Agizo 1 linahusu ujenzi wa ukuta wa Forodhani;
iv. Maagizo 3 yalihusu ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara ya kwa upande wa Pemba;
v. Maagizo 8 ya kiutendaji kwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar;
vi. Maagizo 4 ya kiutendaji kwa Mamlaka ya Mapato, Tanzania tawi la Zanzibar;
vii. Maagizo 4 yalihusu Benki ya Watu wa Zanzibar ;
viii. Maagizo 5 yalihusu Shirika la Bima Zanzibar;
ix. Maagizo 11 yalihusu Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*);
x. Maagizo 7 yalihusika na Mfuko wa Barabara; na
xi. Maagizo 8 yalihusika na Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi (*ZIPA*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Utekelezaji wa Maoni ya Kamati, wizara yangu iliyafanyia kazi maoni na ushauri wote wa kamati na utekelezaji umefikia viwango tofauti kama ifuatavyo:

Usimamizi wa Mashamba ya Mipira na Ugomboaji wa Deni. Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo matano ya kamati katika suala hili yalihusu namna bora ya kumalizana na Kampuni ya *Agrotex* iliyokuwa imekodishwa mashamba hayo, kuhakikisha kuwa maslahi ya SMZ yanalindwa katika mchakato huo wa kumalizana na kutafuta namna bora ya kuyasimamia baada ya kukamilisha na Kampuni ya *Agrotex*.

Mhe. Mwenyekiti, hatua mbali mbali zimechukuliwa katika usimamizi wa mashamba hayo, miongoni mwa hatua hizo ni tayari serikali imevunja mkataba na Kampuni hiyo ya *Agrotex*. Pili usimamizi wa mashamba umehamishiwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Tatu Serikali ya Mkoa wa Kaskazini Pemba imeelekezwa kuacha kuruhusu uvunaji wa mpira kutoka katika mashamba hayo kwa watu wasiohusika. Wizara inaendelea na juhudi ya kufuatilia deni la dola laki nne la kodi ya mashamba liliochwa na Kampuni hiyo ya *Agrotex* wakati serikali ikiendelea na mipango yake ya kutumia mashamba hayo kwa kilimo cha mazao mengine ya biashara.

Ufuatiliaji wa Maghala ya Serikali. Mhe. Mwenyekiti, kimsingi mapendekezo manne ya kamati katika suala hili yamelenga katika kuimarisha usimamizi wa mali za serikali, ikiwemo maghala na kuhakikisha kuwa serikali inapata mapato ya ukodishaji kulingana na thamani halisi ya sasa ya mali hizo.

Mhe. Mwenyekiti, hatua za kuyatambua maghala, viwanja na maeneo yote ya serikali zimekamilika kwa upande wa Pemba na zinaendelea kwa hapa Unguja hivi sasa. Matarajio ni kuwa kazi hii ikamilike ifikapo mwezi huu wa Oktoba, 2017. Sambamba na zoezi la utambuzi, wizara kupitia Idara ya Mitaji ya Umma tayari imefanya mapitio ya mikataba 11 ya ukodishaji wa majengo mbali mbali ambapo kiwango cha ukodishaji kimeongezwa kwa baina ya asilimia 20 hadi 75 kutegemea hali ya jengo mahala lilipo na

matumizi yake. Kuhusu matengenezo ya maghala hayo serikali kupitia wizara inayosimamia maghala hayo itatenga fedha kutegemea na mahitaji na uwezo wa serikali.

Ujenzi wa Ukuta wa Forodhani. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilishauri wizara kuwa makini katika uteuzi wa washauri wa kusimamia miradi. Wizara imekuwa ikijitahidi kufuata utaratibu na kupunguza washauri kabla ya kuingia nao mikataba, hivyo imeupokea ushauri wa kamati na itaendelea kuufanyia kazi. Kwa sasa kazi ya ujenzi wa ukuta huo na eneo lote umekamilika, na eneo hilo hivi sasa kama wananchi wanavyoliona limependeza sana. (*Makofi*)

Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Wizara Pemba. Mhe. Mwenyekiti, wizara ilipokea ushauri wa kamati kuhusiana na haja ya kuwa makini katika usimamizi wa jengo hilo, kulipa kwa wakati ili mradi uweze kukamilika mapema kama ilivyopangwa na kusimamia vyema ujenzi huo ili jengo liwe madhubuti. Wizara inaendelea na utekelezaji wa mambo yote hayo na ujenzi unaendelea vizuri sana, msimamizi ameshaidhinisha hati saba za malipo kwa Mkandarasi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.74 na zote zimelipwa kwa wakati. Aidha, vikao vya usimamizi vinaendelea kufanyika baina ya Wizara, Mkandarasi na Msimamizi ambapo tayari vikao kumi vimefanyika. Matarajio kuwa jengo hilo litakuwa imara na litakamilika kwa muda uliopangwa.

Bodi ya Mapato. Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo manane ya kamati kwa *ZRB* yalilenga zaidi katika kuhakikisha kuwa *ZRB* inakuwa na ofisi ya kudumu na ya kutosha kwa upande wa Pemba, inaimarisha elimu kwa walipa kodi na inaimarisha usimamizi na kuchukulia hatua walipa kodi wasiokuwa waaminifu.

Kuhusu upatikanaji wa ofisi Mhe. Mwenyekiti, tayari serikali imekipatia kiwanja *ZRB*, kiwanja ambacho kina Nam.711 kilichopo Kwale Gombani na ramani Nam.183 iliyosajiliwa kwa Nam. *DP* 1459/2017 kwa barua ya tarehe 06/04/2017. *ZRB* imekuwa ikifanya operesheni za mara kwa mara za kubaini walipa kodi wasiolipa kodi yao kwa wakati na kwa uaminifu, ambapo kwa kipindi hicho operesheni kumi zilifanyika Pemba na operesheni 22 zilifanyika kwa hapa Unguja. *ZRB* pia inaendelea kutoa elimu kwa walipa kodi na kwa jamii kwa ujumla, ambapo jumla ya vipindi 27 vya redio, 14 vya televisheni na semina 24 zimefanyika. Bodi pia inaendelea na mazoezi ya kutembelea hoteli, inatembelea mabaa na mikahawa kwa madhumuni hayo hayo na huwaadhibu wote wanaobainika kwa kufanya makosa ya kutolipa kodi zao zinavyostahiki.

Mamlaka ya Mapato. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitoa maoni manane kwa Mamlaka ya Mapato *TRA*, tawi la Zanzibar yakilenga kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuongeza ufanisi wa bandari na kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato kupitia udanganyifu wa baadhi ya wafanyabiashara kupitia miradi ya maendeleo. Kuhusu kuhakiki walipa kodi, tayari *TRA* imekamilisha kazi ya kuhakiki taarifa za walipa kodi wote na kuwapatia nambari mpya za utambulisho. Aidha, utendaji wa bandari yetu umeimarika zaidi hivi sasa kufuatia kupatikana kwa vifaa vipya vya kupakia na kuteremshia mizigo katika Shirika la Bandari.

Mafanikio hayo kwa kiasi kikubwa yamepunguza msongamano wa makontena katika eneo hilo la bandari, na *TRA* pia inafanya kazi kwa karibu na Wizara ya Fedha na

Mipango katika kubaini na kuwachukulia hatua wafanyabiashara wanaokusudia kupoteza mapato ya serikali kwa kutumia njia ya miradi ya maendeleo na njia nyengine za udanganyifu.

Benki ya Watu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wa kamati katika PBZ umejikita katika kuipatia benki Makao Makuu yenye hadhi, kudhibiti hasara kutokana na wakopaji wasiolipa madeni yao kwa wakati, lakini pia kufanyia marekebisho Sheria ya *Property Transfer*, ili iendane na wakati na kujipanga ili kunufaika na Soko la Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa Makao Makuu ya *PBZ* kwa sasa uko katika hatua ya kumtafuta Mshauri Elekezi na vile vile kutayarisha michoro kwa ajili ya ujenzi huo. Mchakato huo unatarajiwa kukamilika katika robo hii ya pili ya mwaka na kutoa fursa ya kutangazwa kwa zabuni ya ujenzi. Benki ya Watu wa Zanzibar pia imekuwa ikichukua hatua kwa wakopaji wasioheshimu makubaliano juu ya malipo ya mikopo yao, ikiwemo kukamata na kuuza kwa mnada mali walizoziweka rehani au walizoziweka kama dhamana kwa madhumuni hayo.

Benki itazingatia suala la kujitanua zaidi katika Soko la Afrika Mashariki kwa kuzingatia uwezo wa kimtaji na matakwa ya msimamizi wa benki ambaye ni Benki Kuu. Wizara itafanya kazi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Tume ya Kurekebisha Sheria, ili kuangalia marekebisho yanayohitajika katika mfumo wa sheria ikiwemo zinazosimamia masuala ya uhaulishaji mali.

Shirika la Bima. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitoa mapendekezo saba kuhusiana na Shirika la Bima yanayohusiana na upatikanaji wa hati ya kiwanja cha Chake-Chake Pemba, umuhimu wa elimu ya bima kupitia wananchi lakini bima kwa taasisi za serikali kukatwa kwenye Shirika letu la Bima, matumizi ya Soko la Afrika Mashariki na haja ya shirika kuwa makini katika ulipaji wa fidia, matumizi ya mawakala na udhibiti wa bima za kughushi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (*TIRA*)

Mhe. Mwenyekiti, tayari shirika limeshapatiwa hati ya kukodishwa kiwanja kwa miaka 49 tokea tarehe 27/01/2017. Aidha, shirika limekuwa likitoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari na mawakala wake. Shirika pia limepokea ushauri wa kutumia Soko la Afrika Mashariki. Hata hivyo, italifanyia kazi suala hili kwa kuzingatia uwezo wa shirika kimtaji na matakwa ya sheria ya kutumia soko hilo. Shirika limekuwa likichukua hadhari kubwa katika ulipaji wa fidia na linafanya kazi kwa karibu sana na *TIRA* katika kudhibiti matukio ya kughushi bima. Hivi karibuni katika mazoezi hayo viligundulika vyombo 138 vilivyokuwa na bima za kughushi Kisiwani Pemba na wahusika walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Mhe. Mwenyekiti, maoni ya kamati kwa *ZSSF* yalijikita katika kuhakikisha kuwa wanachama wote wanatambuliwa na kulipa michango yao kwa wakati, Mfuko unalipa mafao kwa wastaafu kwa wakati, miradi ya *ZSSF* inakuwa na tija ikiwemo ya Kiwanja cha Watoto cha Umoja Tibirinzi na utoaji wa elimu kwa jamii na uwezekano wa mfuko kuekeza katika shamba la Zanzibar, shamba la RAZABA lilioko Bagamoyo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia *ZSSF* imetekeleza kwa kiasi kikubwa maoni yote ya kamati yaliyotolewa. Mfuko umekuwa ukichukua jitihada za kuwatambua wanachama na kuwaadhibu wale wasiojisajili au kusajili wafanyakazi wao. Aidha, mfuko umekuwa ukilipa mafao kwa wanachama mara tu wanapostaafu na hesabu zao za mafao kuhakikiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kuhusu elimu kwa jamii, *ZSSF* imefanya vipindi vya redio 77 na vya televisheni 6 katika mwaka wa fedha 2016/2017. *ZSSF* itafanya kazi na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuangalia fursa zilizopo za uwekezaji katika shamba la RAZABA na kwa kuzingatia muelekeo wa serikali katika uwekezaji katika shamba hili.

Mfuko wa Barabara. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitoa mapendekezo yaliyolenga katika kuimarisha upatikanaji wa fedha za Mfuko wa Barabara ikiwemo zinazotoka Hazina, lakini kuongezwa kiwango cha kuchangia na ufuatiliaji wa ulipaji wa leseni ya barabara. Maoni mengine yalihusu kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha za mfuko yanakuwa na tija iliyokusudiwa, fedha kwa ajili ya uendeshaji wa mfuko na ushirikishwaji wa mfuko katika maamuzi ya ujenzi wa barabara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kiasi kikubwa suala la upatikanaji wa fedha kwa wakati kwa mfuko limepatiwa ufumbuzi na sasa hakuna ucheleweshaji wa kuwapatia fedha. Wizara inalifanyia kazi pendekezo la kuongeza mapato kwa ajili ya barabara. Aidha, kuhusiana na fedha kwa matumizi ya mfuko, tayari kiwango kilichopendekezwa na kamati cha asilimia 10 kimefikiwa.

Kuhusu mapato ya leseni ya njia kwa sasa tatizo hili limeondoka kwa kiasi kikubwa kufuatia uamuzi wa kuweka malipo yote ya leseni na *sticker* katika ununuzi wa mafuta. Hatua za kuimarisha ushiriki wa mfuko katika barabara zinazojengwa kwa fedha kutoka mfuko nazo zitaongezewa au zitachukuliwa kama ilivyopendekezwa.

Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi. Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikuwa na takriban maoni 15, katika maeneo tofauti kwa *ZIPA* ikiwemo kuimarisha utendaji kama kituo *One-Stop-Centre*, kuimarisha mashirikiano ya *ZIPA* na taasisi nyengine za serikali katika kuhudumia wawekezaji, lakini kuongeza ruzuku kwa *ZIPA*, uwezekezaji katika eneo la RAZABA nao pia ulijitokeza hapa, hatua kwa wawekezaji wasio waaminifu, lakini pia ulinzi wa mazingira na uwekaji wa huduma muhimu katika maeneo huru ya Fumba na Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, utendaji wa *ZIPA* kama kituo kimoja cha ufanikishaji uwekezaji unaendelea kuimarika, tayari Idara ya Uhamiaji imeikuza ofisi yake iliyopo *ZIPA* na kuweka Mtendaji Mfawidhi mwenye kuweza kufanya maamuzi. Kwa sasa uamuzi wa vibali vya ukaazi na kazi vinatoka *ZIPA* kwa ufanisi zaidi. *ZIPA* pia imeanzisha kwa mafanikio jukwaa la uwekezaji linalowaleta pamoja watendaji wa taasisi mbali mbali za serikali zinazohusika sana na masuala ya uwekezaji ili kuwa na uelewa unaofanana na kuwa na maamuzi ya haraka.

Mhe Mwenyekiti, hitimisho. Maelezo niliyoyatoa ni muhtasari tu wa utekelezaji. Taarifa kamili ya utekelezaji kwa kila ushauri wa kamati umeambatanishwa katika ripoti ambayo

wamepatiwa Waheshimiwa Wajumbe na kwa upande wetu tunaendelea na utekelezaji wa maoni na ushauri wa kamati na tupo tayari kupokea ushauri zaidi kutoka kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa uwasilishaji wako wa ripoti. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Karibu.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Menyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*), Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, ambaye ametujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa ndani ya Baraza lako tukufu tukiendelea kutekeleza majukumu yetu ya kikatiba.

Aidha, natoa pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha Hotuba ya Kamati kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa Wizara ya Fedha na Mipango yaliyotokana na ripoti yetu iliyowasilshwa ndani ya Baraza hili katika Mkutano wa Tano uliofanyika Mwezi Febuari, 2017, ambapo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitoa maoni na maagizo mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pongezi za pekee ziende kwa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ujasiri wa kuiongoza vyema nchi yetu na kudumisha amani na utulivu kwa kipindi chote cha uongozi wake hadi leo. Hii inadhihirisha wazi kwamba yeye ni kiongozi shupavu na shujaa, tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema, amzidishie uwezo na uvumilivu wa kuendelea kuitumikia nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia tunatoa pongezi zetu za dhati kabisa kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi kwa miongozo anayoitoa kwa Baraza hili tukufu na kuliwezesha kufanya shughuli zake za kuwatumikia wananchi kwa ufanisi mkubwa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii adhimu ya kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Khalid Salum Mohammed, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa ushirikiano wao wa hali ya juu waliouonesha katika kazi zetu za kamati. Aidha, pongezi za pekee ziende kwa Naibu Katibu Mkuu mpya ndugu Iddi Haji Makame kwa uteuzi na heshima kubwa aliyoipata, hii inadhihirisha wazi kwamba juhudi na

uweledi wake katika utendaji ndio nyenzo iliyomfanya Mhe. Rais kumuona yeye kuwa ni mtendaji atakaeisaidia sana Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, tunamtaka azidi kukaza kamba katika kuchapa kazi na kamati itakuwa bega kwa bega ili Zanzibar iweze kwenda mbele kimaendeleo. Sambamba na hilo, tunaipongeza wizara kwa kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya kamati yetu na kutupatia majibu fasaha na yenye muruwa katika kikao cha majadiliano ya utekelezaji wa maagizo hayo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ambao tumeshirikiana kwa pamoja kutekeleza jukumu hili la kikanuni la kupokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Ni dhahiri kabisa umakini wa wajumbe hao ndio uliowezesha kazi hii kuwa ya ufanisi mkubwa hadi kumalizika kwake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue kwa majina wajumbe hao mmoja baada ya mmoja kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
5.	Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
6.	Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Mjumbe
7.	Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
8.	Ndg. Said Khamis Ramadhan	-	Katibu
9.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa yetu ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwezi Febuari, 2017 kamati ilitoa maoni na maagizo mbali mbali kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa nia ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa wizara hiyo. Aidha, mnamo tarehe 11/09/2016, kamati ilikutana na wizara ili kupokea majibu na ufafanuzi wa hoja zilizojitokeza kwenye taarifa hiyo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kutekeleza matakwa ya Kanuni ya 108 fasili ndogo ya (15) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa agizo la mashamba ya mpira ya serikali, kamati yetu iliarifiwa kwamba hatua za uvunjaji wa makataba na kampuni ya *AGROTEX* zimekamilika na mashamba hayo yamesharejeshwa serikalini na kukabidhiwa kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kuyaendeleza zaidi. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango imesitisha uvunaji wa mpira katika mashamba yote ya serikali kwa kumuandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Kuhusu deni la *AGROTEX* la USD 400,000/-, kamati imearifiwa kuwa wizara tayari imeshakaa na mwekezaji ili kuhakikisha deni hilo linalipwa serikalini. Kamati kwa kweli inapongeza sana juhudi hizo zilizochukuliwa na Wizara ya Fedha na Mipango na kuwataka waongeze kasi ya ufuatiliaji wa deni hili kwani deni hili ni la muda mrefu sasa.

Katika suala zima la utekelezaji wa agizo la kuyaendeleza maghala ya serikali, kamati iliarifiwa kwamba Wizara ya Fedha na Mipango wakishirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wanaendelea kuyahakiki majengo, viwanda na maghala ya derikali ili kubaini kama yanatumika kwa mujibu wa malengo yaliyowekwa na serikali. Baada ya uhakiki huo, taarifa itawasilishwa serikalini kwa hatua zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la agizo la utanuzi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*), kamati iliarifiwa kuwa benki hiyo imeanza kutafuta Mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu yake katika kiwanja chake kilichopo eneo la Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa wadaiwa sugu, benki huwafuatilia kwa karibu wadaiwa hawa na baadae huzitangaza au kuziuza dhamana zao ili kufidia deni lao. Aidha, *PBZ* wamejipanga kuanzisha kitengo maalum kwa ajili ya usimamizi mzuri wa marejesho ya mikopo benki hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la benki kuingia katika Soko la Afrika Mashariki, kamati yetu iliarifiwa kuwa kunahitajika maandalizi makubwa ikiwemo Rasilimali Fedha na Rasilimali Watu ili kumudu ushindani wa soko hilo. Hata hivyo, kamati inaitaka wizara kupitia *PBZ* ianze maandalizi ya kuingia kwenye Soko la Afrika Mashariki sasa na isingoje kesho.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa agizo la operesheni za mara kwa mara zinazofanywa na Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), kamati yetu iliarifiwa kwamba jumla ya operesheni 32 zimefanyika kwa Unguja na Pemba, kilichogundulikana kupitia operesheni hizo ni kama ifuatavyo:

a) Baadhi ya vyombo vya moto havijasajiliwa;
b) Baadhi ya Wafanyabiashara wanaandika thamani ndogo katika risiti zao wanazozitoa kinyume na bei halisi za bidhaa hizo; na
c) Mabaa, hoteli na nyumba za kulalia wageni nyingi hazijasajiliwa (baa na hoteli bubu).

Hivyo basi, kamati inawashauri sana wafanyabiashara wetu wabadilike wasifanye biashara kwa mazowea bali wafanye biashara kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inawapongeza sana Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) kwa hatua inayochukua na tuwaombe Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuzidi kuwaunga mkono na kuwapa moyo watendaji hawa wa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), ili wazidi kuleta ufanisi wa majukumu waliokabidhiwa na taifa letu
.
Mhe. Mwenyekiti, tuunaiomba Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) wasimuonee haya mfanyabiashara yeyote anayekwepa kodi na umefika wakati kwa Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) kukitumia kifungu cha 58 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi kinachotaka Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) kuwatangaza hadharani wale wote wanaokwepa kulipa kodi kupitia vyombo vya habari. Hatua hii itasaidia sana kwa wafanyabiashara kulipa kodi zao ili kuepuka kuwekwa hadharani katika orodha ya wasiolipa kodi.

Kwa upande wa matumizi ya mashine za risiti za kielektroniki (*EFD*), kamati yetu imearifiwa kuwa wizara imo katika hatua za mwisho za manunuzi ya mashine hizo na inategemewa mwezi wa Novemba, 2017 zitaanza kutumika. Tuwaombe Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*) waendelee kutoa elimu kwa walipa kodi ili wale watakaokabidhiwa mashine hizo wawe na uelewa mzuri wa matumizi ya mashine hizo ili kupunguza changamoto zilizojitokeza za mashine hizo kwa upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF*), kwanza tunampongeza kabisa tumpongeze Mkurugenzi mpya wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, Bibi Sabra Issa Machano kwa kuteuliwa kwake na Mhe. Rais, tunamtakia kila la kheri katika majukumu ya ujenzi wa Taifa letu. Pia, tunamshukuru Mkurugenzi mstaafu wa *ZSSF* kwa mashirikiano mazuri aliyoipatia kamati yetu, naye tunamtakia mapumziko mema na maisha marefu.

Kuhusu tatizo la uvujaji wa mapato kwenye viwanja vya kufurahishia watoto Unguja na Pemba, kamati imearifiwa kuwa *ZSSF* ina mpango wa kuweka mifumo ya kisasa ya kutumia kadi za kielektroniki katika viwanja vyotevya kufurahishia watoto Unguja na Pemba ili kuwa na usimamizi mzuri na udhibiti wa mapato. Sisi kamati tunaipongeza sana *ZSSF* kwa juhudi hizo za usimamizi mzuri wa mapato katika viwanja vyetu hivyo na tunaomba waongeze kasi ya usimamizi na ufuatiliaji kwenye miradi mengine ambayo wanaisimamia ili imalizike kwa wakati na iweze kuleta tija iliyokusudiwa kwa Mfuko na Taifa kwa ujumla. Miradi yenyewe ni:

1) Mradi wa Nyumba za Mbweni;
2) Mradi wa Ukarabati wa Jumba la Treni; na
3) Mradi wa Ujenzi wa *'Shopping Mall'* katika eneo la Michenzani.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa agizo la kupambana na *sticker fake* za bima zilizopo nchini, kamati iliarifiwa kwamba Mamlaka ya Bima Tanzania (*TIRA*) kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Zanzibar (*ZIC*) na Vyombo vya Ulinzi na Usalama wanaendelea na zoezi la ukaguzi wa vyombo vya moto barabarani kwa kutumia mtandao wa (*TIRAMIS*), ili kugundua *sticker fake* za bima. Hivi karibuni tumeshuhudia kupitia vyombo vya habari kuwa jumla ya magari 138 yamegundulika na *sticker fake* za bima kisiwani Pemba, kati ya magari zaidi ya 168 yaliyohakikiwa.

Kamati yetu inaipongeza sana juhudi hizo zinazochukuliwa na *TIRA* wakishirikiana na *ZIC* na vyombo vya ulinzi na usalama ya kukabiliana na changamoto hii ambayo inakwaza maendeleo ya nchi yetu. Aidha, tunaliomba Shirika la Bima liwe makini na baadhi ya wateja ambao wanaunguza vyombo vyao au kuviharibu kwa makusudi kwa lengo la kupatiwa fidia ya chombo vipya.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa agizo la ujenzi wa ukuta wa Forodhani (*sea wall*), kamati iliarifiwa kuwa mradi huo wa ujenzi wa ukuta utamalizika mwishoni mwa mwezi wa Septemba, 2017 na umechelewa kukamilika kutokana na changamoto nyingi zilizojitokeza wakati mradi unaendelea. Changamoto hizo ni kugundulika kwa mashimo makubwa yaliyosababishwa na maji ya bahari pamoja na kugundulika kwa mabomu zaidi ya mia moja ambayo yamechukua muda kuyaondoa ili yasije kuleta madhara. Kamati

inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mradi wa *ZUSP* kwa kukamilisha mradi huu ambao umeleta haiba mpya na nzuri katika eneo lote la Forodhani.

Mwisho Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inaipongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuyatekeleza maoni ya kamati kwa kiwango kikubwa na kamati imeridhishwa sana na majibu ya hoja hizo. Ila kwa zile hoja ambazo ni endelevu, Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo itafuatilia kwa karibu zaidi kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa Wizara yetu hii ya Fedha na Mipango. Nichukue fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa usikivu na utulivu wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii.

Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe, waijadili ripoti hii ya utekelezaji, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimaye waunge mkono utekelezaji wa maagizo haya ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa uwasilishaji wako. Waheshimiwa Wajumbe inao mbele yangu hapa wachangiaji lakini bado fursa ipo leteni majina yenu kwa wale ambao wataendelea kutaka kuchangia. Sasa tutaanza na Mhe. Ali Suleiman Ali na baadaye atafuatia Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia ripoti ya maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016-2017.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri kwa dhati kabisa kwa kazi zake nzuri pamoja na busara zake katika shughuli zake na usimamizi mzuri juu ya kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanakuwa vizuri na wanatekeleza maagizo au taratibu uliowekwa.

Lakini pia nimshukuru Katibu Mkuu sana nimpongeze yeye Naibu katibu Mkuu, Wakurugenzi, Makamishna na vitengo vyote vya fedha bodi zote Benki, Bima na wengine neo wanaohusika na mambo yetu ya fedha. Kwa ufupi Mhe. Mwenyekiti niseme tu kwamba, wenzetu wanastahili kila pongezi hasa kutokana na hali halisi ya nchi yetu na mapato ambayo yanapatikana siku hadi siku. Nawaomba waongeze bidii ili pato ya serikali liongezeke kuleta faida kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kwanza Bodi ya Mapato Zanzibar. Kwa kuzingatia hili niseme tu kwamba roho ya nchi yoyote au maendeleo ya nchi yoyote yanategemea makusanyo ya fedha na yanategemea vyombo vilivyowekwa kuhakikisha kwamba fedha zinaingia serikalini na zinakwenda moja kwa moja kwa maslahi ya wananchi wetu kwa faida ya maendeleo ya kila siku. Bila ya makusanyo mazuri, bila ya usimamizi mzuri basi huwa faida haipatikani baada yake hupatikana hasara. Kwa hivyo, nachukuwa fursa hii maalum kwa kuwapongeza kwa dhati kabisa na nawaomba sana waongeze bidii katika kuhakikisha kwamba juhudi inaongezeka pato la nchi lipatikane ziadi.

Mhe. Mwenyekiti, tumezoea sana katika makusanyo yetu ya fedha huko nyuma tunakotoka tulikuwa tunafanya kama mazoea, lakini baada ya kupangwa mikakati, sheria na kanuni mbali mbali sasa hivi naamini wafanyakazi wetu wengi au takribani wengi au wote anaelewa wajibu wao. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba bidii hii iongezwe, jitihada yao nzuri tunaipongeza lakini pia wawe na changamoto ambazo zipo wazitanzuwe ili mafanikio yapatikane. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, juzi hivi karibuni nimelisikia tangazo lakini nashukuru liko tangazo linaendelea kutoka *ZMUX* likasema moja kwa moja tu kwamba watu wote wanaotumia vyombo vya usafiri wa aina yoyote kama alinunua chombo hicho kwa mtu fulani au kitengo fulani lakini jina si lake yeye basi kipelekwe haraka katika Bodi ya Mapato ili ahaulishiwe yeye fedha zipatikane zile kwa njia ya uhakika.

Kwa kweli, uzoefu Mwenyezi Mungu atunusuru kama linatokea janga lolote au tatizo lolote wenye chombo halisi huyu mtu wa pili aliyeuziwa anaweza kurusha akasema mimi hilo halikunihusu. Lakini kumbe mtu halali aliyekuwa nacho chombo kile si chake ambaye alikuja nacho akamuuzia mwengine.

Kwa hivyo, naunga mkono hili lakini ningeshauri kidogo tu pale likitangazwa sasa hivi tulipo Mamlaka ya Mapato inatangaza mwenye chombo chochote akibadilishe mpaka tarehe 30 kuanzia leo, sijaifahamu vizuri. Nitamuomba Mhe. Waziri akija hapa atueleze kuanzia tarehe angapi agizo lile lilitoka na hadi tarehe ngapi kwa sababu wananchi wengi vyombo vya wamenunua kwa watu binafsi au vimetoka kwa watu mbali mbali niuzie halafu kakaa na kadi ya mtu mwengine. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili mamlaka yetu itupe taaluma pamoja na mimi sote tujue tu kwamba chombo hichi alikinunua pahala fulani lakini mwenyewe nataka kuwa mimi lakini kilianza tarehe 1 ya leo mpaka tarehe fulani huo ndio usahihi.

Kwa mfano tuliona Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Tanzania Bara walipokuwa wanakusanya kodi ya nyumba walitoa muda wa miezi mitatu, lakini ilipoonekana wananchi wameshajihika na wamekubali kulipa kodi ile waliongeza tu tunaongeza kutoka tarehe 1 ya leo mpaka tarehe 30 mwezi huu au mwezi ujao wale watu wanaelewa. Kwa hivyo, niwaombe sana nawapongeza utaratibu mzuri na naamini watu watakwenda kubadilisha kadi zao bila ya matatizo.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na kamati maoni yake au maagizo yake nawapongeza sana kamati wamefanya kazi nzuri wamefanya juhudi yao kubwa ya kutoa mambo mbali mbali au kuona mambo mbali mbali ambayo yana faida kwa serikali yetu. Kutoa elimu Mhe. Mwenyekiti katika chombo chochote ni muhimu. Kwa hivyo, chombo chochote ambacho kinakusanya fedha kinatakiwa kuwa na taalama nzuri, hivyo Mhe. Mwenyekiti ukimpa mtu taaluma atakuelewa na ukisema mtu anakwenda kimafamba mafamba unamwachia atapotea. Kwa hivyo, niwaponze sana na hapa Bodi imekubali moja kwa moja maana inaendelea na taaluma yake kwa wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi.

Mhe. Mwenyekiti, si kulipa tu hata ununuzi ukinunua udai risiti Mhe. Mwenyekiti hili la kawaida. Kwa wenzetu ukitembea ukitoka hapa unanunua sindano ya kushonea utapewa risiti hasa waliozoea huku hawajui faida yake utaona ah! Ya nini hiyo, unaambiwa

chukuwa bwana usinikamatishe. Kwa hivyo, anwapongeza kwa dhati na nawaomba tushirikiane nao kwa sababu sisi ni wajibu wetu kuwaelimisha wananchi wetu. Wananachi wetu wasikubali kununua na kuondoka bila ya kupewa risiti, risiti ile ina faida.

Kwa kuwa na mambo mengine yameyaandaa kuna wakati wanafanya kama ukaguzi, wanapofanya ukaguzi naomba sana waangalie sana vitabu vyao vya risiti. Wafanyabiashara wengine wajanja wanaweza kudai risiti kitabu hichi kumbe hewa cha ukweli hawakitoi. Kwa hivyo, na hili nawaomba waangalie lakini si wafanyabiashara wote wengine waaminifu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, suala la makusanyo nishasema moja kwa moja wanakusanya vizuri waongeze bidii, ili waendelee katika juhudi zetu.

Suala la magendo katika nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza *ZRB* kwa kushirikiana na Vikosi vyetu KMKM na wananchi wengine wenye imani na nchi yao kwa kuokoa mambo mengi ambayo yanajitokeza na hapa yamezungumzwa magendo ya mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana *ZRB* wawasaidie nyenzo wenzetu hawa wawasaidie kwa kila hali waweze kwenda masafa marefu kukagua vyombo ambavyo vinachukuwa mafuta ya magendo kuleta katika nchi yetu. Kwa kweli, mafuta ya magendo hayana hasara kwa muuzaji, lakini yana hasara kwa nchi yetu tunakosa faida. Kwa hivyo, niseme tu kwamba hili nawapongeza na waongeze bidii.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *Package Tourism* hili ni suala zuri sana. Kamisheni ya Utalii kukaa na *ZRB* nimeona hapo wamekaa na wameandaa mpango mzuri navipongeza vyombo viwili kwa kukaa pamoja na kufatilia suala letu hili la utalii. Mhe. Mwenyekiti, mimi Mjumbe wa Kamati ya Maedeleo ya Wanawake Habari na Utalii tumekwenda katika kutembelea Uwanja wetu wa Ndege tumeona namna gani wanapoingia watalii na mapokezi yake ambayo hayaridhishi mara wakati mwengine.

Kwa kweli, mwenye dhamana ya pale kupokea wageni wanaoingia katika nchi yetu wanakuwa Idara ya Uhamiaji. Lakini pale ukifika mtu wa utalii hayupo mamlaka yanawekwa pembeni *ZRB* shida inayowakuta hapo atakae huyo Idara ya Uhamiaji anaweza kukaa siku ya kwanza ya pili ya tatu ndio akampekea tamwimu ile ni hatari na naamini patakuwa na udanganyifu siku nyengine ambapo tutakosa pato letu katika serikali.

Kwa hivyo, naomba vyombo vyetu hivi vitatu *ZRB*, Kamisheni ya Utalii na Idara ya Uhamiaji hawezi kukaa pamoja katika kusajili watu wanaoingia. Lakini wawe nao karibu pale kuhakiki kila mgeni anaeingia pale ajulikane, kwa sababu vyengine vyovyote itakayobakia hasara. Kwa hiyo, nawapongeza na hili waliangalie.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kufanya vizuri katika kazi ni nidhamu ya kazi, nafikiri kuna nyimbo ilimbwa zamani"Nidhamu ya kazi ni msingi kwa mafanikio mema kazi ....", yaani popote ulipo uwe na nidhamu ya kutosha ufanye kazi zako vizuri ili faida ipatikane.

Kwa hivyo, nawapongeza wenzetu kwa kuwapa elimu zaidi wafanyakazi wajue nidhamu zao nzuri ili kupata kodi zetu nzuri ziendelee katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Mwenyekiti wa Kamati alisema tu kukwepa kodi wakwepa kodi hao hawa wasionewe huruma. Mhe. Mwenyekiti, mfanyabiashara yeyote anajivutia yeye na mfanyabiashara hakwambii hata siku moja anapata faida atakwambia anapata hasara tu faida hakuna ukweli hausemi.

Mimi Mhe. Mwenyekiti nilikuwa mfanyabiashara nilikuwa anasafirisha bidhaa mpaka nje na nilikuwa naye mshiriki wangu lakini simtaji, maana tulikuwa ubia na mwezangu, alikuwa hatari tuligombana, mimi nikamwambia kuwa sitaki kufanya kazi kwa hili, anakanambia kuwa Mheshimiwa kwani ukilisha kidogo tu pale wewe ukiwapelekea chochote watapokea nikamwambia hapana. Kwa kweli, nimezaliwa hapa na namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie nife hapa hapa nchini kwangu, lakini sitoisaliti nchi yangu chukuwa funguo zako nakwenda zangu. Mhe. Mwenyekiti, alinitafuta kwa nai nai, anakuja ananambia nilikutania tu mimi maana yeye si kwao hapa yeye kaja kuekeza tu hapa.

Kwa hivyo, suala la kukwepa kodi ni hatari na hili tusiliachie. Mhe. Mwenyekiti, najua unaniangalia kutokana na muda....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako umemaliza.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika moja tu.

Mhe. Mwenyekiti: Haya malizia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nawapongeza wenzetu hawa kwa kufanya ziara za kushitukiza, nawaomba hizi waongeze na wala wasiwe na muhali kwa sababu ukishitukiza ndio unapa faida.

Kwa hivyo, niseme tu kwamba nawapongeza Mhe. Waziri, watendaji wote wa wizara hii kwa taasisi zote nimezitaja mwazo na niliokuwa sikuzitaja nawaunga mkono katika kazi zao nzuri juu ya kupata faida ya mapato katika nchi yetu.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Ali Suleiman Ali, na kama una zaidi wasilisha kwa maandishi mchango wako. Sasa namwita Mhe. Jaku Hashim Ayoub na baadaye atafuatia na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza Wizara ya Fedha na Mipango kwa utendaji wao wakiongozwa na Mhe. Waziri makini ambaye sina utendaji wake. *(Makofi)*

Jana tulikuwa tukichangia ripoti ya Kamati ya Wizara ya Afya nilisema mimi hata sisimizi anahitaji afya, kila kiumbe hai kinahitaji afya, lakini bila ya afya huwezi kuishi

na leo hii ni wizara muhimu sana ya fedha na ndio macho yetu yote yako hapa. Hata hapa tumekaa tunategemea posho tulipwe ili tupate fedha yenyewe. Kwa hiyo, ni wizara muhimu sana ambayo ndio wizara mama za wizara zote hizi, hapa tanaka tulielewe hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikuombe sana Mhe. Waziri, hili ni ombi na wala si kosa kuiba ni kosa kuliko kuomba na ikiwemo wananchi wa Donge unaowaongoza wewe Mheshimiwa. Kumekuwa na usumbufu mkubwa kwenye vyeti vya kuzaliwa mtu anatoka Donge nauli yake shilingi elfu nne elfu tano kwenda kulipia cheti cha mtoto anakwenda Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pale Mazizini kuchukuwa cheti, anaambiwa akalipe shilingi elfu moja mia tano au shilingi elfu mbili anakwenda *PBZ*, kuanzia saa 12 mtu wa shamba yule kafika pale mpaka saa kumi huduma ile hajaipata. Mhe. Mwenyekiti, hapa serikali haitengezi kimtazamo wangu na mimi elimu yangu ni ndogo, hapa serikali inakula hasara.

Niulize kwa nini Mhe. Waziri serikali inakuwa hasara inakula hasara mtu yule keshatoka Donge, au Paje nauli yake shilingi elfu tano anatoka anakwenda Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuchukuwa kile cheti anakwenda kulipa benki anakuta msongamano anataka kulipa shilingi elfu mbili, keshatumia shilingi elfu tano kwenda na kurudi na hakupata huduma ile anarudi tena Donge na Paje siku ya pili. Kwa kweli, nia ya serikali ni nzuri kudhibiti pesa zisipotee lakini hapa serikali hapa inakosa pesa kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti. Sasa naomba nikueleweshe, mwananchi yule angelikuwa keshalipa pesa ile angekwenda tena akenda kufanya majukumu yake akatafuta pesa nyengine na serikali ingepata pesa zaidi.

Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri na naamini kwa utendani wake harudi nyuma. Kwa kweli, cheti kile ni shilingi elfu mbili au elfu moa mia tano anatoka Donge au Paje kwenda pale anashinda *PBZ* na mle ndani hatari *PBZ* ukiingia, tuulizeni sie tunaopita kule ndani benki lakini Waheshimiwa Mawaziri wao wanakaa kwenye magari makubwa na kuagiza tu, na mwenye kuumia yule mnyonge. Kwa hiyo, naomba lengo ni kubwa angeweka alu *limit* la shilingi elfu hamsini au thalathini ya kwenda kulipa benki hivi tunaumiza wananchi wetu. Hili namuomba sana nafikiri atalifikiria kwa makini kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *ZRB* nilikuwa nikipiga kelele sana kuhusu *IFD Machine*. Kwa kweli, sioni sababu ya msingi mashine hizi kwenda kununuliwa nje wakati *TRA* pamoja na mashine hapa zipo, tutatumia shilingi ngapi kuziagiza mashine hizi tuta-*save* pesa ngapi tukinunua mashine hizi kwa ndugu zetu hapa Tanzania *TRA* wenyewe ni moja. Kuna kitu gani hapa, hata mashine zinakununulie huko nje wakati mashine zipo pesa hizi zingetusaidia kwa mambo mengine Mhe. Waziri gharama zitakuwa ni kubwa na programu yenyewe ya kunasa tu pengine ziliwe pesa basi tukafanya maarifa mengine. *(Makofi)*

Lakini nije hapa hapa *ZRB* jana nilisema hapa Wizara ya Afya niliomba sana itumie kidogo ulimi kuulainisha maneno mazuri nikasema ni sadaka jana nilizungumza hata masaa 24 hayafika. Niwaombe wenzangu wa *ZRB* sisi tunawahitaji na kazi wanayofanya tunaithamini na tunaiona mchango wao ni mkubwa.

Sasa kufika pale hapa mengine kuna harufu wanakwenda mpaka na askari kazi itafanyika kweli kwa wafanyabiashara huko duniani kote hakuna mambo kama haya hakuna njia nyengine mpaka kwenda na askari kutishia ipo harufu hiyo, tuwaelimishe watu maneno mazuri ni sadaka tusitumie nguvu kama hiyo. Hivyo, hakuna utaratibu mwengine mpaka kufika na askari kodi ikusanywe kwa askari, ah! Sifikirii huko duniani kote sijaona utaratibu kama huo. Hili liangaliwe kwa makini.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo *PBZ* bado wananchi wanateseka muda unapotea mkubwa kwenda kutafuta huduma ya pesa, pesa zao wenyewe utafikiri wanagaiwa pale au wanaenda kuomba sadaka pesa zake mwenyewe kuna *ATM* miezi sita mtu kadi hajaipata *PBZ* kidogo walikwa wakienda mbele mwendo wao lakini sasa hivi kidogo hauridhishi kwa wananchi na naweza kuthubutu ni benki inayowateja wengi kwa Zanzibar sasa hivi. Lakini mateso yamekuwa makubwa kwenda kutoa pesa *PBZ*, na sio kama zinatolewa bure ni haki yake mwenyewe mwanachi anakwenda *ATM* pale utaambiwa bado usahajaza fomu ah haionekani jaza tena upya. Kwa hivyo, unasubiri kadi ije mimi mwenyewe yamenikita. Bado pana msongamano wa *PBZ* wananchi wanatesema sana na wakati mwengine hata taa haziwaki ndio huwa kuna joto *PBZ* kama mko juu huko mimi ni mdau wenu mkubwa, lakini hapa tuko kwa niaba ya wananchi tusameheane.

Vile vile, sasa nije na masikitiko yangu Mhe. Waziri *ZIPA*. Kwa kweli, niwapongeze sana jamaa wa *ZIPA* kwa kazi wanayoifanya na hii ndio ikampelekea nafikiri Mkurugenzi yule mara kadhaa kutokana na utendaji wake ulio makini na watendaji wake. Mhe. Mwenyekiti, hapa pafuatiliwe nilisema juzi kuna miradi sasa hivi karibu mitano hiyo harufu nimeisikia Kamisheni ya Ardhi Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira hayupo hapa sasa. Wawekezaji wanapata usumbufu alipokuwa akiamua tu *ZIPA* watu hawateseki wanafanya mazoezi ya kupanda ngazi na kushuka bila ya kutaka, mazoezi yale wanafanya mazoezi ya nguvu, maana yake kama wamelazimishwa ngazi kupanda shuka.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna pahali paliooza ni Kamisheni ya Ardhi, Mhe. Waziri husaini mikataba ile kutoa Katibu Mtendaji au Mkurugenzi basi utalia mule ndani nimeshahudia si mara moja si mara mbili. Kuna miradi karibu mitano sasa hivi imekwama Kamisheni ya Ardhi ilipokuwepo *ZIPA* hakuna tatizo hilo hiyo harufu nimeisikia naomba aifuatilie. Mhe. Waziri, na hapa alijibu juzi Mhe. Waziri akasema wawekezaji hawapati shida, lakini kwa kweli wanapata shida Mhe. Waziri akiwemo muwekezaji wa Mahonda naye anadai nyumba zake mpaka leo kwenye serikali pamoja na amri ya Mhe. Rais bado hazijatoka mpaka hivi sasa ninavyozungumza suala hilo. Mwekezaji yule kafanya kazi kubwa pale kwenye Kiwanda cha Sukari tena sana, mpaka leo hajapewa tokea mwaka 2005 mpaka leo, tusiwe na huruma ya mdomo na vitendo vinatakiwa, yule kafanyakazi kubwa mno.

Lakini wawekezaji wazalendo. Mhe. Mwenyekiti, naomba tena Mhe. Waziri ule mradi wa jengo la Bakhresa kule kama haukupita kwa njia nyengine, na ungepitia Kamisheni usingejengwa mpaka leo ule na hili jina la Kamisheni lifutwe. Haya majina nilisema mimi majina mwengine kuita watu ni mabaya. Hata mtoto wako mwenyewe kumwita jina lililokuwa sio zuri anaweza kufanya vitendo sio zuri, Kamisheni, Kamisheni

inachukua *commission* au. Maana yake *commission* kudai mapato, kuna matatizo Kamisheni ya Ardhi. Kuna Kitengo sasa hivi kinaitwa *UDCA* ndio kinatoa vibali vyote, utakaa sijui Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya asaini usumbufu mtupu, sisi tunawahitaji wawekezaji kumbe hakuna wawekezaji. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye *ZSSF*. *ZSSF* ndugu zanguni hapa hizi pesa wanazozitumia katika kuwekeza sijui zinakwenda kwa uangalizi uliokuwa mzuri. Tumekuwa tunashuhudia miradi mingi sasa mnataka kuwekeza, kuna nyumba hapa njiani zinaendelea kujengwa, kuna jumba la treni, kuna viwanja vya michezo. Kuna ujenzi unataka kuanza sijui lini pale Michenzani, hizi pewa za wananchi jamani ziko salama.

Mhe. Mwenyekiti, juzi mlipitisha sheria hapa kuongeza angalau kipato kiongezeke kidogo, lakini ilikuwa ni mtego mtego kidogo pale, hizi *ZSSF* ziko salama za wananchi. Miradi ni mingi lengo ni kuongeza lakini biashara yenyewe imeshuka sasa hivi, hata humu *PBZ* wanalalamika wenyewe katika ripoti yao, kuna watu hawawezi kulipa au wamekuwa wakipunguza makodi yao kulipa, kutokana na hali ya kibiashara ilivyo, biashara imekuwa ngumu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi nafikiri nimalizie hapa, mchango wangu ni huu Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid, na baadaye Mhe. Simai Mohammed Said ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na baada ya kuniruhusu nianze kutoa mchango wangu. Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataallah* mwenye kuweza kuumba mbingu na ardhi, na usiku na mchana akatupa na sisi uhai waja wake tukakutana hapa. Lengo na madhumuni yetu ni kuwatumikia wananchi waliotuchagua, ili tuweze kuyafikia malengo tuliyoyakusudia ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu.

Pia narudia kama nilivyotoa shukrani zangu na pongezi zangu na kumtakia dua Rais wetu Dk. Ali Mohammed Shein, kwa mambo yake mazuri na bidii yake anayoifanya ya kutuletea maendeleo. Nia na madhumuni yake ni kuona kwamba taifa letu linasonga mbele, linasonga mbele linakuwa kwenye uchumi kama tunavyoona kwenye bajeti yetu, mara hii imekuwa ni nzuri imetoka kwenye zaidi ya *billion* 8 na imekwenda mpaka *trillion* 1.1. Kwa kweli nawapa hongera sana watendaji, kuanzia Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na timu yake kwa kazi kubwa wanazozifanya za kusimamia mapato. *(Makofi)*

Pia tumpongeze kiongozi wetu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, sisi kama na yeye kuna mtu wa kuweza kumpelekea pongezi ni yeye, kwa sababu hizi wizara zote mafanikio yote yanayopatikana kwenye wizara yeye ndiye chachu, kwa sababu zingeharibika hapo, basi kila kitu kingeharibika. Kama nilivyosema kwamba kama ilivyokuwa mwili pasipo roho umekufa, basi nina imani bila matendo nayo imekufa. *(Makofi)*

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze katika pale nilipopakusudia. Naomba nende moja kwa moja kwenye ukurasa wa 9 na 10 kwenye agizo namba 4. Udhibiti wa Mapato *TRA* na *ZRB* waanzishe mpango maalum wa kuhakikisha kuwa wanadhibiti tatizo la uvujaji wa mapato Kisiwani Pemba na Zanzibar. Ni visiwani Unguja na Pemba au wangeandika Zanzibar pia ingetosheleza, lakini uvujaji wa mapato kisiwani Pemba na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nimekuja hapa kwa sababu gani, vyanzo vya mapato na udhibiti wake tunataka uutizame ndio kitu kikubwa kwa ulimwenguni kote, mapato ndiyo yanayoendesha serikali, kodi ndizo zinazoendesha serikali. Unapokosa kudhibiti kodi na kushindwa kuweka mfumo mzuri wa kodi basi kila kitu chako hakiwezi kuwa vizuri. Hao wawekezaji unaowazungumza watakukimbia, wafanyabiashara watakukwepa, wakulima watakosa kulima na kila kitu. Lakini tutakapoweka mfumo mzuri wa kodi ukawavutia watu, ukawavutia wawekezaji, ukawavutia wafanyabiashara wa ndani na nje, basi tunaweza tukapiga hatua na hili ndio lengo tunalolitaka na ndio mambo tunayoyataka yaje katika nchi hii.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nini tufanye. Ushauri wangu wa kwanza. Jambo hili huwa nalizungumza kila wakati, kwamba hatuwezi kupanga mipango yetu bila ya kuwa na takwimu halisi ya kitu tunachotaka kukifanya. Hapa ili twende vizuri ni lazima tuwasajili wafanyabiashara wetu wote. Hatua ya kwanza tuwasajili wafanyabiashara wote tuwajuwe, wafanyabiashara wanaoingiza mizigo kutoka nje.

Hivyo, ni vyema tuwasajili wafanyabiashara wenye maduka, tuwajuwe hawa wanaingiza biashara kutoka nje na wana maduka au hawa wanaingiza biashara zao tu kutoka nje. Tukifanya hivyo basi tutaweza kupanga mipango yetu ya kukusanya kodi vizuri, kwa namna gani kwa sababu mizigo inaingia hapa kwa sehemu mbili, inaingia kwa kupitia bandarini na *airport.* Kwa hiyo, inapoingia kwenye bandari tutaweza kumfahamu kwamba fulani kaingiza mizigo, tunafanya tathmini ya mizigo anayoiingiza.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua bei ya soko ilivyo kwa sasa basi biashara hii itauzika kwa kiasi fulani, tunatizama bei pamoja na gharama halafu tunaweka kodi yetu, hatumlazimishi na wala tusimlazimishe kulipa kwa wakati ule. Lakini kama tukiwa tumemsajili, tunajua alipo na tunamjua fulani ana kodi ya serikali kiasi fulani, basi tunaweza tukakusanya mapato yako kwa vizuri, yasitusumbuwe na tusipigishane na watu mbio, tusiende huku na huku, kazi nyepesi. Vyenginevyo tutakuwa sisi tunaingia kushoto wafanyabiashara wanaingia kulia, kila mmoja anamkwepa mwenzake, tutakapofanya hili basi litatupunguzia matatizo. *(Makofi)*

Sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu mwengine kuangalia viwango vya kodi, tupunguzeni utitiri wa kodi. Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa kwenye ripoti kutoa elimu ndio kitu peke yake kitakachowafanya watu waweze kuwa karibu na walipa kodi. Lakini nakubaliana na Mhe. Mjumbe mwenzangu aliyetangulia kwamba tukalipe kodi leo kwa mtutu wa bunduki kwa nini, watu wafikie hali ya kupelekewa askari kwa ajili ya kulipa kodi, sio kitu cha kupendeza wala sio kitu cha kufurahisha. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, elimu itolewe wananchi wafahamu nini umuhimu wa kulipa kodi, viwango vya kodi tuviweke ambavyo vinaweza kuwa vinalingana na biashara tuliyonayo. Tusiendelee kuweka utitiri wa kodi watu kweli watatukimbia, wawekezaji watatukimbia, tutakapowawekea kodi kubwa zaidi basi watu watatukimbia hilo bilaya shaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunataka tukusanye kodi kwa wingi. Kwa mfano, tuangalie ni wakulima wangapi na wavuvi wanaochangia katika kodi, hatuwajui. Lakini kwa wenzetu Tanzania Bara kule kuna benki tele ambazo zinatoa mikopo kwa wakulima, sasa mkulima yule akizalisha ataweza kulipa kodi, mvuvi yule akienda kuvua akiuza samaki ataweza kulipa samaki, mote humo muna vianzio vya kodi, lakini tujiangalie vipi tunavitumia hivyo. Kwa hivyo, sasa wakati umefika wa kubadilika tuzione sekta zote hizo ni muhimu sana kwa mchango wa kutoa kodi katika Mfuko Mkuu wa Taifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia leo asubuhi hapa kama tutakumbuka tulikuwa tunazungumza masuala mengi ya wafanyakazi. Tuyaangalie haya makampuni ambayo tulisema kwamba tuyasajili, wafanyakazi wangapi wapo ambao wamesajiliwa ambao wanalipa kodi serikalini, kuna kodi nyingi za serikali hazijulikani. Tatizo ni kukosa kuwasajili. Kwa hivyo, turudini tuwasajili wafanyabiashara, tusajili makampuni yao ya biashara ili tuweze kufahamu na tupange mipango yetu vizuri, mambo haya ya kukwepa kulipa kodi yatapungua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo tujiulize, naangalia na ninajua, tuangalieni tu kwa juu juu ni watu wangapi wenye majengo wanaolipa kodi ya mapango. Mtu anaweza kukodisha nyumba kwa dola 2,000 kwa mwezi, lakini ni kiasi gani analipa serikalini, hamna. Kwa hivyo, ni lazima tukubaliane kwamba tubadilike na mfumo wa kodi uliopo, tutafute *modality* nyengine ambayo itatufaa sisi iwe nyepesi kukusanya kodi, ili kodi iweze kuchangia katika mapato ya taifa ambayo ndio uti wa mgongo, kodi ndio uti wa mgongo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kule Tanzania wanakusanya kodi vizuri sana, lakini nina hakika kwamba leo tukifanya ukaguzi wa kina hasa, basi tutagundua kwamba asilimia 40 au 50 ya wafanyabiashara hawalipi kodi. Ukitaka hiyo mimi nitawaambieni. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum SMZ unaniangalia, lakini naomba afanye *operation*, eneo la Mlandege kaangalie, atume watu kama 10 kwa wakati mmoja, waingie madukani kama watakuja na risiti hata moja. Hatulipi kodi ukweli huo, kama inalipwa basi ni asilimia ndogo *(Makofi)*

Mhe. Mwenyeki: Mhe. Omar Seif Abeid, zungumza na kiti sio uzungumze na waziri.

Mhe. Omar Seif Abeid: Muda umekwisha Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, kodi hailipwi. Kwa hivyo, iko haja sasa ya kutengeneza mpango maalum wa kuwapata wafanyabiashara wakalipa kodi, lakini kwa njia nyengine sio ya kwenda na mtutu wa bunduki, tusiwafanyie kwa nguvu watatukimbia zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, natoka hapo nakwenda sasa kwenye benki ya *PBZ*. Wenzangu wamesema matatizo yaliopo *PBZ*, nakubaliana nao. Kwa kweli, *PBZ* kuna matatizo, yaani utakapofika mwisho wa mwezi, Mhe. Mjumbe mwenzangu aliyenitangulia kalizungumza hili, wananchi wanapata tabu, mwananchi anapata tabu kwa mshahara wake. Anatoka asubuhi anarudi jioni wakati watu tunao. Sasa kwa nini wasiangalie kwamba kipindi hiki sasa cha mwisho wa mwezi watu wamekuwa wengi wakaongeza madirisha ya huduma kama ni mawili, basi wakayaweka manne, sita au manane watu wasikae pale, mtu anakwenda anapata huduma yake au tuwaulize *PBZ* haja yao ni kuwaona watu wamewapanga foleni kutoka mwanzo mpaka mwisho *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wito wangu *PBZ* wabadilike wakati wa kutoa huduma hasa za mwisho wa mwezi, wananchi wetu wanapata shida. Si haki kama alivyosema mwenzangu Mhe. Jaku Hashim Ayoub anaweka pesa anapotaka inakwenda kumtesa, ni vizuri tukawaangalia kama kuna madirisha manne, tukafanya hata manane, lakini watu wanapokwenda wanachukua pesa yao wanaondoka, kesho mtu anakuwa na kazi nyengine au anapata muda wa kwenda kufanya kazi nyengine.

Sambamba na kutoa mikopo. Mhe. Mwenyekiti, wito wangu *PBZ* sasa waanze kwenda kibiashara, hasa kuangalia wakulima na wavuvi ambao ndio wengi katika nchi hii. Mhe. Mwenyekiti, najua wanaogopa ile *loan risk* kwamba hawajui vipi wanaweza wakarejesha mikopo, lakini waangalie kwamba *interest rate* yao iko ngapi, angalau watengeneze sheria ambayo ile *risk* yao iko kwenye asilimia 10. Wakifanya hivyo wataweza kuwasaidia wakulima wetu kwa kuwapa mikopo, wataweza kuwasaidia wavuvi wetu na itaweza kusaidia uchumi wa nchi. Kwa sababu wengi wataweza kuwa-*afford* mikopo hiyo na wataweza kufanya kazi.

Kwa mfano, niliuliza swali juzi Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhusu *green house*, nikaambiwa kwa kuanzia kilimo hicho cha *green house* cha kumwagilia kwa matone mkulima anahitaji shilingi milioni saba, mkulima wa kawaida shilingi milioni saba haipati. Lakini kama benki wataweza kuwakopesa peza zile, basi watu wataweza kuchukua mikopo wakalima lengo likatimia, serikali ikapata kodi na wananchi wakaweza kunufaika na uchumi wa nchi ukaongezeka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako umemalizika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya kwa heshima na taadhima natamka wazi kwamba, nimeiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, sina pingamizi nayo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Omar Seif Abeid. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said na baadaye Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajitayarishe.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nianze kwa kukushukuru wewe, lakini pia nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mwenyekiti wa Kamati na wajumbe wote, juu ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya mwaka huu 2017, katika kutimiza majukumu

yetu sisi tukiwa kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana pamoja na meza yako na serikali yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi ya kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa vifungu ambavyo ameeleza katika ripoti yake, *style* yake ni tofauti na wengine, lakini kimoja ambacho kimenivutia sana kwa jinsi ambavyo amenukuu vifungu vya katiba. Katika ukurasa wa kwanza naomba ninukuu.

Sura ya Tatu Kifungu 43kinasema kwamba:

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera na serikali kwa ujumla na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais, watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki ni kikubwa sana na kwa jinsi Mhe. Waziri ametupa heshima ya kipekee kwa kutambua umuhimu wake, basi niunge mkono na niombe pia kifungu hiki kiendelee kutambuliwa na wizara nyengine na watendaji wote ndani ya serikali katika kutimiza majukumu yao, huku wakiheshimu muhimili wako huu wa Baraza la Wawakilishi.

Pia katika Kanuni ya 108(15) inasema kwamba:

"Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016 naitaka kila wizara kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi mara moja kwa mwaka katika mwezi wa Septemba au Oktoba".

Hili ni jambo muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ni kubwa sana kwa wananchi wetu, elimu hii inapokwenda kwa wananchi wanazidi kufahamu haki zao na sisi tukiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaweza kuyachangia na kuweza kuishauri serikali.

Baada ya hapo niende moja kwa moja katika mchango wangu na nitaanza kwa upande wa *ZRB*. Mhe. Mwenykiti, *ZRB* iliyokuwa ya zamani sio ya leo, *ZRB* iliyokuwa ya miaka mitano sio ya leo fedha ambazo tulizokuwa tunakusanya zamani sio za leo. Lakini nikiri kwamba kwa jinsi ya uchumi wa visiwa unavyokwenda visiwa vyetu vya Zanzibar tutategemea sana maeneo matatu ambayo yametajwa katika MKUZA ambayo ni utalii, biashara na huduma.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya utalii sasa hivi ndio imekuwa ipo juu zikiungana na sekta ya huduma, lakini moja ambalo huwa linanisikitisha sana wakati mwengine unakuta watendaji au baadhi ya watu huwa wanaitilia ufa serikali kwa kauli zao, nasema hivyo. Kwa mfano, kutothamini wawekezaji na wafanyabiashara mtu hutoa kauli kusema kwamba asiyetaka aende nyumbani kwao, au asiyetaka aondoke. Mhe. Mwenyekiti, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein anafanya juhudi kubwa sana kwa kushirikiana pamoja na Makamo wa Pili na serikali yake katika kuhamasisha biashara na uchumi katika visiwa vyetu. Hivyo, ni muhimu sana watendaji ndani ya serikali kuthamini na kutambua hotuba za Rais, lakini pia kutambua Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa umuhimu wake hasa katika kuhamasisha kwamba uchumi wetu tunazidi kuujenga kwa ubora zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, changamoto zilizokuwepo katika sekta ya utalii zinajulikana lakini moja ninalotaka nilizungumze ni suala la *package tourism* ambalo limegusiwa katika ripoti. Mhe. Mwenyekiti, *package tourism* ipo na yanakuja denge zao hapa zinaingia kwa siku sita au saba zinaondoka. Lakini ndege ambazo zilikuwa zinakuja miezi ya nyuma au miaka ya nyuma zikitua pale siku ya Jumatano ulikuwa unakuta ndege 10, 11, 12 lakini hivi sasa ndege zinazidi kupungua. Lakini hii inaonesha kuwa *package tourism* haiko juu lakini tuna *direct arrives* ambao wanaotoka bara baada ya kukamilishwa kuwa *runway* yetu pamoja na *apron* saa ndege nyengine nyingi zimeanza kutua, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akijaalia tutakapokamilisha *Terminal II* ndege nyingi zitazidi kuja na naamini hao ambao wananunua *holidays* kwa kutegemea *package tourism* itapungua.

Lakini hii *package tourism* katika visiwa vyote na maeneo yote katika sekta ya utalii utaikuta na sisi tunashindana na maeneo mengi sana. Sasa niseme tu kwamba *package tourism* sio kama ni kitu kibaya ni nzuri ikiwa wastani isiwe moja katika eneo kubwa la kukuza utalii wetu na mapato yetu katika sekta hii. Kwa hivyo, ni vizuri kuiangalia lakini si vizuri pia kuanza kuikemea au kuinyooshea vidole kwamba haifai ni vizuri tukapata kufahamu umuhimu wake. Kwa kweli, hii wanapokuja wageni hawasimami kutoka mwezi wa Julai mpaka mwaka unaofuata mwezi wa March na mwezi wa April.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nichangie suala la *PBZ*. Mhe. Mwenyekiti, benki zetu hizi ni moja ya maeneo ambayo Wazanzibari tunazipenda na kupata huduma tofauti katika benki yetu ya *People Bank of Zanzibar*. Lakini unapokwenda wakati mwengine mwisho wa mwezi unakuta foleni kubwa wakati mwengine, jambo linalonisikitisha zaid kuona wale wazee wetu, ambao wanasimama nje ya benki hizi wakisubiri kupata fedha zao za pencheni.

Namuomba sana Mhe. Waziri kwa kupitia kiti chako Mhe. Mwenyekiti, aangalie utaratibu mpya kama tungeweza kuweza kuwalipa wazee wetu kama katikati ya mwezi, ili kupunguza bughuza na mashine hizi za *ATM* zote kuvamiwa mwisho wa mwezi kwa pamoja. Lakini pia ikiwezekana wapiganaji wetu pia tuweke katika kundi hilo hilo la watu wanaopokea pencheni, kuwe kuna tofauti baina ya wale ambao ni wafanyakazi ndani ya serikali zetu au katika sekta yetu ya umma na wale ambao wanapokea fedha kutoka serikalini katika njia tofauti, huduma hizi za benki zizidi kusogezwa vijijini na maeneo tofauti katika mashamba yetu.

Lakini pia niseme tu kwamba aina ya mavazi katika maeneo yote ya Wizara hii husika kuanzia *ZRB, ZSSF* pamoja na *PBZ* kwamba mavazi ikiwa akinamama na akinababa basi waangalie mavazi ambayo unapotoa huduma hasa kwa watu ambao wanakuja wanatoka vijijini ziendane na mazingira ambayo wanachokitarajia. Kwa mfano, mtu anapokuwa na madhahabu pete tatu au nne umezivaa haipendezi kwa yule mtu ambaye ni masikini anakuja benki kupata pencheni yake, ambacho anaifuata kuangalia mazingira ambayo yanaleta utafauti wa aina yoyote, au umetoka katika sherehe au harusi kama kuna *gloves* za kuvaa.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni vyema utaratibu upatikane lakini nahisi watu wengine wanapoangalia wanakuwa wamevimba uso lakini sio kwa nia njema lakini haileti usawa

baina ya watu wetu. Kwa hivyo, niseme tu kwamba utaratibu wa mavazi na *uniform* zao wanapokuja katika kutimiza majukumu yao, yaendane kwa mujibu wa sheria zetu na utaratibu ambao utakaopendeza kwa wananchi wetu.

Lakini pia kwa upande wa *ZURA*. Mhe. Mwenyekiti, tumeona mabadiliko ya *ZURA* waliyoyatekeleza juu ya masuala haya ya *BPS* ambayo ni *Bulk Procurement System* waliyoanza karibuni, lakini tumeona bei ya mafuta kumekuwa kuna mabadiliko ya karibu shilingi mia moja na hamsini na zaidi. Sasa hapo hapo kuna kima cha chini sasa hivi kimepandishwa mpaka laki tatu hawa makampuni ya mafuta na gesi ambao wanauza katika maeneo tofauti ya vituo natambua sasa hivi wanataka kupandisha tena mafuta, wapandishiwe kwa shilingi arubaini mpaka hamsini pengine ili waweze kutimiza majukumu yao na kulipa mishahara yao ipasavyo.

Sasa Wizara hii ya Fedha na Mipango natambua haisimamii taasisi ya *ZURA*. Lakini katika mpango mkuu wa fedha za nchi hii, mpango mkuu wa kutokusimamia dira ya nchi, mpango mkuu wa kusimamia uzalishaji na kuhakikisha kwamba biashara inakwenda ipasavyo ni vizuri Mhe. Waziri akawa anakaa nao karibu, ili kuhakikisha haya yote hayamuathiri hasa mwananchi mwenye kipato cha chini wa kati na Wazanzibari wote kwa jumla.

Suala jengine nataka niongelee ni suala la *ZIPA*. Tumekuwa tunapiga kelele sana Mhe. Mwenyekiti na niseme tumeanza kuona tofauti, nimeona kwenye vyombo vya habari kwamba *ZIPA* sasa wameanzisha hili jukwaa pamoja na kuangalia suala zima la *One Stop Centre*. Mhe. Mwenyekiti nataka nishauri kitu kimoja tuna wawekezaji wengi ambao ni wazalendo wa Kizanzibari kuna wawekezaji pia kutoka nchi zetu za Afrika ya Mashariki tuna wawekezaji pia wanatoka mabara mengine tofauti. Hivyo, ni vizuri hasa katika sekta ambazo za huduma pamoja na utalii kila mwisho wa mwaka kwa kuwashauri Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kupitia taasisi yake kabla ya kukaribisha mwaka mpya wakawa wanafanya tafrija au *cocktail,* ili kukutana na kujuana, lakini pia katika kujenga ule umoja na hasa kuleta ukaribu baina ya sekta mbili tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hali tunayokwenda sasa hivi kuna uwezekano pia sekta binafsi sio kama wanaachana lakini wanakuwa wako *distance* au wako mbali kidoto, kwa sababu unakuta kazi nyingi kwa upande wa serikali hakuna kitu kinachowaunganisha ambacho kitakaa katika hali ya umoja na upendo ili waweze kushirikiana kwa pamoja.

Ushauri wangu katika mnasaba huo huo niwaombe *ZIPA* pamoja na Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo wafanye ikiwezekana *International Convention* moja kubwa ya kibiashara Zanzibar washirikiane kwa pamoja, lakini lifanyike katika mazingira ya kuboresha ya kunyanyua biashara zetu na kutangaza mambo ambayo tunawakaribisha wawekezaji ili kuleta ile dhana moja ya *Public Private Partnership* lakini pia baada ya kupitisha ile sheria baraza la biashara ule umoja uanze kuonekana. Hatuwezi kukaa kila siku tukasema kwamba tunatarajia wawekezaji watakuja tu, lazima na sisi tujitangaze kwa ushiriki wetu na fedha ndogo tunazotumia katika kutangaza, basi tuwaalike wale ambao watapenda kuja kwetu katika visiwa vyetu, ili na wenzetu wa Tanzania Bara washiriki wapate kujua.

Mhe. Mwenyekiti, unaweza kwenda Tanzania Bara tu hapo wapo watu wana hamu ya kuja kuwekeza Zanzibar, lakini hawajui jinsi gani au njia gani wapite ili wafike. Kwa hivyo, *ZIPA* tutambue kwamba kuna watu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na nchi zetu jirani wanaweza kuja hapa wakaja kuwekeza katika sekta tofauti, lakini pia kuunga mkono juhudi za serikali katika maeneo ambayo wamejipangia.

Lakini katika suala ambalo ningependa nitoe masikitiko yangu katika ripoti hii sijaiona ni suala zima la Tume ya Mipango. Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Mipango ni katika eneo moja ambalo wanasimamia dira kubwa ya nchi hii kutupeleka wapi tunakotaka tufike. Hivyo, ni vizuri wanapokuja kutoa ripoti zao wakati wote hili eneo linakuwa linaguswa tunaelewa na tunalichangia katika maeneo ambayo serikali na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anataka wapi atupeleke, kwa sababu wao kwa lugha nyengine wanaangalia kwa kule kwa mbali kabisa. Sasa, katika kulenga huko sisi lazima tuweze kuona wapi tunakwenda nao sambamba, ili tuweze kutoa ushauri wetu kwa niaba ya wananchi ambao tunaowawakilisha katika chombo hichi kikubwa cha nchi yetu.

Kwa mfano, kima cha chini cha mshahara kilichotangazwa sasa hivi kimeleta mpasuko katika maeneo tofauti na sekta tofauti. Lakini ukiangalia katika sekta hizi zinagusa kwa njia moja au nyengine Wizara ya Fedha na Mipango katika mapato yake. Tuangalie *ZSSF* ikiwa wafanyakazi watapungua katika maeneo tofauti ina maanisha kwamba *collection* ya fedha ambazo zitakazolipwa *ZSSF* zitakuwa zinapungua. Mhe. Menyekiti, naomba kushauri Waziri wa Fedha na Mipango aangalie sana pamoja na Tume yake ya Mipango kuangalia na kushirikiana na wizara nyengine zote, ili kuhakikisha hakuna ufa unaoingia katika uchumi wetu kwa mazingira ya kuleta umoja na kuilinda na kuipenda sekta binafsi na kuifanya pia sekta binafsi na kuifanya waipende usimamizi wote wa serikali katika mambo tofauti.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia tena kwa…….

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda wako umemaliza.

Mhe. Simai Mohammed Said: Namalizia mwisho……

Mhe. Mwenyekiti: Nakuongeza dakika moja.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti nimalizie tu kwamba kwenye suala la *ZSSF* waendelee kuiga wigo kuwekeza kama wenzetu *PBZ* wamefungua matawi mengi Tanzania bara, lakini pia katika *pension fund* wanazotaka kuwekeza waangalie pia nje ya Bara la Afrika kama inawezekan, lakini pia niwapongeze sana taasisi zake kama *Zanzibar Insurance*, *PBZ* kwamba tayari wamefika Bara unapopanda gari *taxi* sasa hivi ukienda Dodoma na maeneo mengine ya Iringa, Mwanza, Arusha unakuta *stickers* za Shirika la Bima la Zanzibar haya ni mambo mazuri tuendelee na bidii hizi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mchache niliokuwa nao naamini haya nitaweza kuishauri wizara husika. Nampongeza Mhe. Waziri, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa muda huu mengine nitampelekea Mhe. Waziri kwa maandishi. Hivyo, naunga mkono hoja mia juu ya mia. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunisikiliza

pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili la Wawakilishi, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana, Mhe. Simai Mohammed Said. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na baadaye Mhe. Suleiman Makame Ali ajitayarishe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana. *Bismillahi Rahmani Rahim*. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuanza kuchangia ripoti hii ya Wizara ya Fedha na Mipango ambayo imeletwa hapa mbele yetu, lakini kwa kuwa wizara hii kubwa na ina mambo mengi nitajaribu kuchangia machache nitakayowahi.

Nikianza na *page* Nam. 6 kuwepo kwa mtandao unaochapisha bima *fake*, jambo ambalo linasababisha kurudisha nyuma maendeleo ya shirika. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti hapa niliwahi kuzungumza na Mhe. Waziri naomba hili suala aje anisaidie kuja kunijibu. Hapa wizara husika imeshakiri kwmba kuna mtandao kuna mashine ambayo inachapisha bima *fake*, ikiwa *road license*, au *Insurance fake*. Lakini jambo la kushangaza Wizara ya Mhe. Waziri wa Fedha imeanza au imeendelea kukamata wananchi kuwasimamisha na mapolisi gari zao sehemu ambazo wanakamatwa wanapelekwa Madema moja kwa moja, wakifika pale sasa wale wananchi ndio wamekuwa wahalifu sio wale ambao waliomiliki hii mashine.

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, walilipishwa watu wote elfu hamsini hamsini (50,000) na walioshindwa wamewekwa ndani hili suala linasikitisha, kwamba Wizara yenyewe wameshajielezea hapa kwamba kuna mtandao maalum, kwa maana hiyo huu mtandao sio wale wanyonge au wale waliokamatwa. Sasa imekuwaje wizara imekwenda kutoa *go ahead* kwamba Polisi pamoja na *ZRB* kwenda kukamatwa wananchi ambao hawana makosa naomba Mhe. Waziri akija anijibu, fedha zile za watu atazirudisha lini kwa wenyewe na badala yake huyu ambae amesababisha kuchapisha vitu feki hivi watamkamata alipe yeye faini.

Kwa kweli, hili linaonesha dhahiri kwamba hawa watu hawana makosa lakini wametumiliwa njia za kinguvu kwenda kukamatwa. Sheria ile ya mwananchi nilizungumza juzi wizara husika imeshindwa kudhibiti vitu hivi kwa muda mrefu hawajavijua. Sasa je, yule mtu ambaye masikini hajui kitu ataweza kujua *road license fake* na *insurance fake*. Naomba Mhe. Waziri hili suala lisijirudie tena katika jamii, kwa sababu ni suala la udhalilishaji kwa upande wa masuala ya kuwaonea wananchi, hatuwezi kuwalipisha wananchi kitu ambacho hawakijui na wahakukitaka watu wamelipa na taasisi zinazotoa zikamatwe sio wananchi ambao wanakosea.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye wizara hii kwa sababu hii wizara nzito, nitaendelea kuchangia kwenye mada ambazo ninazo hapa lakini na nyengine nitamaliza baadaye. Jengine nitazungumzia kwamba Benki za Zanzibar zote, kila benki ina wazimu wake, nazungumza ina wazimu kwa sababu zina makato ya maajabu hasa kwenye *transaction* ambao za *ATM* na ukisafiri ukitumia *credit card* ya kulipia basi ina makato ya ajabu. Utakuta pengine Benki ya *PBZ* unapofanya *transaction* ya dola umetumia nje dola mia utatozwa mfano shilingi laki mbili, wakati ukichenjisha huku Zanzibar unapewa shilingi 223,000. Kwa maana hiyo, shilingi 23,000 hapo wameshakukata tayari.

Halafu kuna gharama nyengine ambazo zinakuja kwenye *transaction* nyengine. Ukienda benki nyengine ukitumia dola mia ile ile kwenye *transaction* utatozwa shilingi 2,100 wakati benki ziko hapa hapa Tanzania au Zanzibar lakini tofauti yake ni kubwa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri ni vyema akaangalia haya makato wananchi au fedha benki inatumia udanganyifu kwa njia hizi za kukata fedha nyingi. Kwa mfano, mwananchi ambaye atatoa fedha kwenye *ATM* ya Zanzibar yoyote shilingi 10,000/= mnyonge katoka shamba huko anatoa pesa hizo, basi kato lake litakuwa mfano shilingi 1,000. Tizama cha maajabu akitoa shilingi 400,000 kwenye *ATM* hiyo hiyo kato lake shilingi 1,000.

Hali hii inaonesha dhahiri kwamba wizara husika bado haijaweza kuwa-*challenge bankers*, haiwezekani mtu atoe shilingi 10,000/= akatwe shilingi 1,000/= kwenye *transaction* na anayetoa shilingi 400,000 akatwe shilingi 1,000/=. Sasa wale wenye mshahara mdogo wanaumia vipi wanaotaka kufanya *transaction* kubwa ambao hawana uwezo wa kutoa shilingi laki moja kwa pamoja wameshazowea kutoa kila siku shilingi elfu tano au kumi.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango mabenki haya yanayofanya utapeli wao kwa njia ambazo wananchi hawazitambui wakaweza kuzidhibiti, wakaweza kuweka *fixed rate* ambazo wanajua *charge* hizi zitakuwa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la miradi Wizara ya Fedha na Mipango ndio inayohusika na fedha za nchi na Mhe. Waziri tunamuamini akituangusha katuangusha yeye. Kwa hivyo, suala la miradi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inafanyika ndani ya nchi yetu karibu yote au mingi asilimia 80 kwa 90 *value for money* haipo, utakuta miradi imegharimu unajua hasa hii imegharimu shilingi bilioni mbili kwa mtu mwenye uzoefu, yaani *Engineers* kabisa anakwambia hasa hii inagharibu shilingi bilioni 2, lakini unakuta imewekwa 4.5 bilion shilings utafikiri ile nyumba imekwenda kujengwa na ma-*engineer* wa Dubai *Tallest Building in the World*.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kwenye *project* zao hasa yeye ndiye anayesaini hizi fedha, lazima fedha za wananchi, fedha za serikali tuzionee uchungu, isiletwe *project* tu tukaambiwa mabilioni tukaamini kuna vitu vinaonekana kabisa hivi *nonsense* haviingii akilini, lakini fedha ni nyingi zinazotajwa. Miradi ambayo tunaijua hii miradi haifiki fedha hizi lakini watu wamo tu wanapeleka.

Jengine kwenye miradi hii hii wanaposaini *contract* utakuta imesainiwa shilingi milioni tano utaambiwa mpaka inamaliza, lakini miradi ile haiwahi kumaliza fedha zinaongezwa tena kwa njia wanayoijua wenyewe, watakwambia sijui kitu gani wamesahau, sijui kitu gani kimeongezwa hapo mwanzo hatukujua. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri awe makini sana kwenye suala hili, kama sio hivyo tutakuja kumlaumu yeye tutakuja kumkaanga yeye humu ndani, kwa sababu yeye ndiye muidhinishaji wa fedha na yeye ndiye msimamizi wa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu jengine ningetoa ushauri, tuna sababu gani ya kujenga majengo ya wizara makubwa kila kona ndani ya nchi hii, kwa nini wizara isitafute eneo

moja kubwa likajenga majumba manne marefu ya ghorofa kumi kumi ya ghorofa saba saba, wizara zote zikatupwa humo ndani. Hii itarahisisha wananchi kwenda kwenye mawizara katoka Wizara ya Fedha kaingia *ZIPA* kaingia *ZRB* kaingia zake Katiba na Sheria, kaingia Tawala za Mikoa lakini leo utakuta Katiba na Sheria ghorofa kumi, *ZRB* ghorofa kumi na mbili, *TRA* ghorofa thalathini haya tunakwenda wapi nchi yenyewe ndogo mambo yote ya nini kutumika mabilioni.

Kwa mfano, *ZRB* tumetuliwa zaidi ya shilingi milioni 12, na sasa hivi tunafanya ma *project* mengine makubwa makubwa, kwa nini tusitafute *idea print tower* mbili ambazo zitakuwepo Zanzibar kwa ajili ya mawizara ya serikali lakini leo watu wanatafuta zile njia ambazo wanazozijua wao ujanja wa mjini wajenge maghorofa *value for money* haipo matokeo yake ndio haya tunawauza wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba dakika ishirini baada ya kumi na tano. Kamati nimesoma kitabu hichi, kamati karibu mambo yote wao wanashauri tu, kodi zikusanywe kwa nguvu eee kamati waoneeni huruma wananchi mtawauwa. Kamati inashauri tu wao hawajui kusema ipunguzwe kodi au itumiwe njia ya hekma wao wapo kwenye kushauri *TRA*, *ZRB* wabinye watu wao wakamue watowe fedha, hizo fedha ziko wapi. Nchi hii ukijumlisha kodi tunazolipa ni zaidi ya asilimia arubaini, tukitaka nchi yende kwenye uchumi lazima kodi iwe chini.

Kwa kweli, Mhe. Waziri tunamuamini tena, lazima akae kwenye mikakati mizuri ya kuhakikisha kodi ndani ya nchi inachuka, sio inapanda kila siku na hata kama watasema haipandi lakini haijawahi kushuka, watakwambia hatujapandisha lakini matokeo yake itakwenda juu haichuki chini.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba kuona mabadiliko kipindi cha miaka mitano ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, mabadiliko ya *investment* na kitu kinachovutia *investors* duniani kwanza ni kodi kuwa ndogo, pili miundombinu imekamilika ndio nchi itakwenda la sio hivyo hapa tutakaa hivi hivi, tupigwe na *AC* humu ndani tuzungumze tunayoyataka maendeleo nje hayaji. tutakaweka kodi ndogo tutapoweka miundo mbinu kwa wepesi leo tutapata kila mwaka *project* mia ndani ya nchi. Lakini tutapoweka kodi ndogo miundo mbinu ikaimarika tutapata *investment* mia tano katika mwaka.

Sasa ni bora ni vipi, bora tuweke vitu ghali tupate *investor* mia kwa mwaka au bora tuweke tupate *investor* mia tano kwa mwaka ni kipi bora, tunachotaka kujenga nchi yetu watu wavutiwe lakini leo wakisikia tu. Zanzibar kuna asilimia 45 ya kodi ukizijumlisha zote kuanzia *TRA*, *ZRA*, Mhe. Tawala za Mikoa na kodi zake Waziri wa Biashara na kodi zake ukienda kila kona kuna kodi, ukizijumlisha hizi ni zaidi ya asilimia 40 ndani ya nchi watu wanalipa.

Sasa nini watu watavutiwa nacho kikubwa watakimbia tu na hawa waliokuwepo wanalalamika msione wamekaa kimya. Mhe. Mwenyekiti, kamati wanashauri watu wabinywe kwenye kodi nawapongeza sana *ZRB* wana huruma sana na Wazanzibari, na ikiwemo na *TRA*. Lakini sasa wajibu wao wakusanye kodi kwa njia ya halali, leo mapolisi wanakwenda ndani ya mahoteli, polisi na watu wa *ZRB* kukusanya kodi tumeona wapi masuala haya, wageni wenyewe watakimbia.

Kwa kweli, Mhe. Waziri haya masuala nashauri yaondoshwe na tuweke *fixed rate* kwa ajili ya mahoteli, hoteli mshakuwa na uzoefu nao hoteli hii inalipa kiwango hichi wapigeni tu, miezi sita tunataka *amount* hii lakini leo kila siku leteni funguo za vyumba wanaenda kwenye vyumba kuna wageni ndani haya mambo vip, Mhe. Mwenyekiti nchi tunaiangusha nchi tunaitia kwenye jina baya. Mhe. Mwenyekiti, kama kodi haijachuka nchi hii, kama vitu ambavyo havijaangaliwa vizuri hasa kwenye masuala ya *investment ZIPA* hawa watu wa mambo ya ardhi wakawa walaini wepesi, masuala ya kodi tukawa watu waaminifu tukawa watu ambao tunaweza kuwaonea huruma wananchi basi nchi haitokwenda, siombezei vibaya, lakini kwa hali tunayokwenda nayo, na naona hii ripoti imesheheni watu wabinye.

Mhe. Waziri, ningeomba uchukulie mambo taratibu kodi watu wa walipe kwa njia ya kibinaadamu…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe zungumza na kiti sio Mhe. Waziri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, nishakutaja sana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie jengine kuhusu suala la *ZSSF*. Kwa kweli, *ZSSF* ni fedha za wananchi ni fedha za wananchi. Sasa jambo la kushangaza *investment* kwa kupitia fedha zile za *ZSSF* wananchi wanafaidika nini. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aje anijibu fedha zote ambazo zinafanyiwa *investment* na *ZSSF* ikiweko kariakoo kuna *income* majumba yanayojengwa maghorofa na mingineyo wananchi wenye fedha zao zile ambazo wanakatwa kwa mwezi mshahara, wanafaidika vipi kwenye kuongezewa faida ile. *(Makofi)*

Kwa upande wa wale ambao wanaachishwa kazi haujafika muda wao pesa zao wanapewa pale pale au watasubiri miaka sitini (60) ndio warejeshewe fedha zao. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala la *ZSSF* nije nijibiwe hilo. Lakini jengine nimekuta kuna nyuma zinajengwa za *ZSSF* nyumba ya chini shilingi milioni mia moja na sitini na saba (167), ambapo hapo Mbweni ndio ya chini yenye vyumba viwili. Hivyo, hizi nyumba namuomba Mhe. Waziri aje anijibu, yaani nyumba hizi wamekusudiwa nani, wananchi wa chini au wageni ndani ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ni wananchi ataweza kununua nyumba milioni mia moja na sitini na saba 167 vyumba viwili vya *apartment* wakati akijenga mwenyewe nyumba ya chini atasimamia milioni tisini 90 yenye vyumba vinne, mshahara wenyewe tumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kazidisha laki tatu 300,000/-, hapo mwanzo ilikuwa laki na nusu 150,000/- tutakaa miaka 35 ukatwe mshahara wote mwananchi wa chini ndio ataweza kununua nyumba ya milioni mia na sitini na saba (167) hilo suala liko dhahiri, sasa hizi nyumba tumempontia nani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli haya mambo yako mingi ni vyema Wizara ya Fedha na Mipango ikakaa ikaangalia vipi, itakaa upya kwenye kuendeleza nchi kwenye suala la uchumi. Lakini kwa *system* tuliokuwa tunayo sasa hivi bado hatujafika kokote, siwezi kumlaumu Mhe. Waziri, siwezi kumlaumu kama yupo Naibu Waziri kama Katibu Mkuu

na wengineo katika wizara husika, isipokuwa ninachotaka wakae waangalie vipi tutafanya ni vyema tukawa na vitu vidogo tukapata kwa *investors* wingi kuliko tukafanya mambo makubwa tukapata watu ambao *slow slow* wakaja watu kidogo kidogo.

Nchi nzuri, nchi inamaeneo mazuri lakini Mhe. Mwenyekiti, najua utaniwashia taa kwa sababu hii karatasi nimeweka *points* tele sijamaliza humu ndani na utanigongea sasa hivi.

Kwa hivyo, nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, nakutaja tena kwa sababu umependa nikujate Mwenyezi Mungu akuzidishie afya, nampongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na watendaji wake wote. Lakini tuzingatie Zanzibar tunataka tuipeleke kwenye nchi ambayo yenye maendeleo, vipi tulivyo sasa hivi hatuko vizuri kwenye suala uchumi Zanzibar bado hatuko vizuri japokuwa…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe muda umemaliza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf : Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii kwa kuwa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, anajitahi na nishampa yangu machache naikubali asilimia 100. Nakushukuru na wewe kwa nipatia nafasi hii. Ahsante sana. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na baadaye anafuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana, Mhe. Mwenyekiti nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Ripoti hii ya Utekelezaji wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwenye Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu nende moja kwa moja ukurasa wa kumi na nane. Kamati imeitaka serikali iendelee kutoa boti na vifaa vya kisasa kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo, yaani KMKM, kuhusu masuala ya kudhibiti magendo.

Mhe. Mwenyekiti, niungane na kamati kwa hilo lakini isiwe ni boti tu, wakipewa hizo boti wapewe na mafuta ya kufanyia kazi, kwa sababu boti hayendi bila ya mafuta. Kwa mfano, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum, tulikwenda katika kambi ya Unguja Ukuu hawana boti hii wanatumia boti ya Hifadhi ya Minai kule. Kwa hiyo, kuna siku nyengine ikitokezea mgongano wa shughuli wale KMKM wanashindwa kufanya kazi zao kwa hiyo naomba sana, kwamba waweze kupatiwa na popote pale kama ni Unguja au Pemba basi waweze kupatiwa vyombo hivi ili kudhibiti magendo.

Kwa sababu hawa wamiliki wenye masheli wanaumia sana na pia tunapoteza mapato kwenye masuala haya ya mafuta, mapato yanapotea magendo yamekuwa sasa inakuwa. Lakini tunashukuru sana KMKM wanavyojitahi na nina imani jitihada hizi zimetokana na Waziri jembe Mhe. Haji Omar Kheir, kwa mikakati yake mizuri. Kwa hiyo, naomba sana Wizara ya Fedha na Mipango kutolichukua hili nalo kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa kumi na tano. Kamati imeitaka wizara kushirikiana na vyombo vya dola kuhakikisha vyombo vyote ambavyo vya moto, vinavyotembelea barabarani viwe na leseni.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili niwapongeze sana Jeshi la Polisi wa barabarani wanavyojitahidi kwa kufanya kazi nzuri zaidi, lakini hususan pongezi zangu za dhati ziende kwa *traffic* wa Mkoa kule Mkoa wa Kusini Pemba, Afande Shaaban hata juzi alikamata vyombo vya moto zaidi ya mia tatu na kuna baadhi ya Waheshimiwa tukampigia simu kuwaombea watu wale. Kwa kweli, tusiwaombe Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu watu wanafanya makosa leo mtu leseni shilingi elfu thalathini, shilingi elfu moja lakini likitokea tatizo barabarani yupo tayari kutoa shilingi milioni nzima ili kunusuru tatizo lile, lakini anashindwa kuichangia serikali kwa shilingi elfu thalathini au shilingi elfu kumi. Mhe. Mwenyekiti, ni tatizo kubwa lakini nina imani Jeshi la polisi wanajitahidi hilo na nijitihada zetu na sisi wenyewe Wawakilishi kuunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nikitoka hapo niendele ukurasa wa tisa. *TRA* na *ZRB* ianzishwe mpango maalum wa kuhakikisha kuwa wanadhibiti tatizo la uvujaji wa mapato kisiwani Pemba na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze sana *ZRB* na *TRA*, lakini Mhe. Mwenyekiti jambo la kushangaza juzi Jumamosi nilikuweko Pemba kule badala ya kumaliza uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya wilaya. Sasa nikamfuata rafiki yangu mmoja ambaye ni mfanyabiashara ni mwanachama wenzangu wa Jumuiya ya Wafanyabiasha Wenye Viwanda na Wakulima, alililalamikia kapelekewa barua na *ZRB* atakikana alipe shilingi bilioni tatu, bilioni tatu sio milioni bilioni tatu, tena mfanyabiashara yule analipa kodi vizuri maskini, anaogopa maana niseme anaogopa akitishiwa kidogo anakwenda *ZRB* analipa pesa anaogopa kweli kweli anagopa. Lakini cha kushangaza *ZRB* wamemuandikia barua hii, hivi Zanzibar nzima hii siwezi kusema kwamba kule Pemba kuna mfanyabiashara anaweza kulipa bilioni tatu hayuko. *(Makofi)*

Lakini wakamuandikia barua hii wakamwambia tujibu, akawandikia kwa hio siwezi kulipa, kwa sababu sina uwezo, maana hata mkinuuza na mimi na wanangu sitimizi. Sasa Mhe. Mwenyekiti, bilioni tatu mfanyabiashara ni kumkomoa ni kama wamwambia hama au wacha au kufa, kwa sababu masikini ya Mungu leo unamwambia atowe bilioni tatu, bilioni tatu atazitowa wapi na ni mfanyabiashara mzuri na kodi anatoa vizuri sana analipa na risiti zipo na ushahidi upo. Hivyo, leo bilioni tatu hizi zinakwenda wapi Mhe. Mwenyekiti ni kumuonea au kumvunja moyo na hata kumrudisha nyuma.

Kwa hiyo, namuomba sana rafiki yangu Mhe. Waziri alifutilie hili na akionekana kwamba kuna nini alichukulie hatua kwa sababu yawezekana akawa siku nyengine itakuwa kuna mambo yakimchezo mchezo yanataka kupita. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri alichukue hili kwa sababu haiwezekani kwamba mfanyabiashara yule bilioni tatu yaani ni jambo la kushangaza hata usingizi hauji. Bilioni tatu maana mimi nilimuuliza mara kumi, akanionesha ile barua ni bilioni tatu sio milioni tatu, bilioni tatu.

Hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri alichukue na alifanyie kazi, ili kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wanapewa moyo, wanapata nguvu ya kufanyabiashara, kwa sababu

tunawategemea wao ili serikali yetu kupata mapato wasiangushwe wafanyabiashara na wasinyanyaswe wafanyabiashara na Mhe. Mwenyekiti badala ya hapo naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana kwa mchango na sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Sarahan Said, hayupo. Kwa hivyo, namwita Mhe. Panya Ali Abdalla na baadaye Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini ajitayarishe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuleta hapa jioni hii. Lakini pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii niweze kusema machache katika wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kabla ya hayo naomba uniruhusu angalau kwa dakika moja niweze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa jambo kubwa na zuri ambalo amelifanya leo hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, amezindua Maonesho ya Kilimo, ambapo yameleta faraja kubwa sana kwa upande wetu. Mhe. Mwenyekiti, jambo lile ambalo amelifanya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, naomba tuchukuwe fursa hii sisi Waheshimiwa Wawakilishi ambao tunaongoza jamii ya wananchi wetu, tuwaombe sasa wananchi wetu waweze kushiriki kikamilifu katika maonesho yale, ili waweze kujifunza vitu vingi kabisa ambavyo vitaleta manufaa kwao na kwa nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa na mimi nichangie katika hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na watendaji wake wote. Mhe. Mwenyekiti, sio siri Mhe. huyu ni jembe na ni kiongozi ambaye anajiamini sana. Hivyo, tunaomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu na maarifa aweze kuiongoza wizara yake hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze na mchango wangu katika agizo ambalo limeagizwa na kamati kuwekeza katika shamba la Makurunge Bagamoyo. Kamati imeomba imesema ingetaka mfuko ikae pamoja na Wizara ya Kilimo na kuangalia ni namna gani wanaweza kuwekeza katika eneo lililopo Makurunge Bagamoyo.

Mhe. Mwenyekiti, mfuko umepokea agizo la umesema utalifanyia kazi. Sasa kwa msisitizo niombe sana sana wizara hii, iweze kulishughulikia suala hili la Makurunge kwa sababu tunajua eneo lile lilikuwa kubwa, na kwa sasa limepungua sana kutokana kutolifanyia kazi kwa muda mrefu, hivyo tumeweza kupoteza nafasi yetu ile nzuri. Kwa hivyo, kwa kuangalia umuhimu wa ardhi na suala zima la uwekezaji wa eneo hili na tunajua serikali ikiweza kuwekeza eneo hili tutaweza pia kupata ajira ya vijana wetu na pia tutaweza kulidhibiti eneo letu hili. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti niombe sana agizo hili tuweze kulifikiria kwa umakini ili lile eneo tusizidi kulisoka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu napenda niende katika *ZSSF*, Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wengi wameeleza lakini na mimi nilitaka nieleze katika mfuko huu. Mhe. Mwenyekiti, niombe mfuko huu, uweze kufikiria mafao zaidi kwa wanachama wake ukiancha ule wa uzazi na ulemavu ambao wanapata wanachama kwa hivi sasa, kama ilivyo mifuko mengine ya jamii. Kwa hiyo, mfumo huu uweze kuwapatia maslahi mengine wanachama wake ikiwemo mikopo waweze kufaidika, kwa sababu muda wa miaka 60 ni mingi kukaa hapo kati ukawa wewe unawekeza pesa zako na huna uwezo wa kuzifanya vyovyote kwa hivyo ni vizuri waweze kupatiwa katika kwamba watu hawa wanawekeza basi kuwafikiria kuwapa mikopo ili iweze hapo kati kuwasaidia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niombe katika eneo hili kuna miradi ambayo inawekezwa na *ZSSF*. Kwa kweli, napenda kusema miradi inayowekezwa iwe na tija kwa wanachama, kwa sababu nichukuwe mfano kwa hivi sasa tuna miradi ya ujenzi wa nyumba hizi na tayari fursa zimetoka tunasikia zikitangazwa, lakini kwa bei zilivyo na nnavyojua jinsi ya wafanyakazi wetu na mishahara yao ilivyo sijui kama wanaweza kumudu jambo hili. Lengo la mfuko huu upo zaidi kwa kutusaidia sisi wananchi wa Zanzibar, ili tuweze kuneemeka tuweze kufaidika na mfuko huu.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja basi aweze kunijibu kama, aweze kunieleza kama kuna maombi mangapi labda hivi sasa yameshafanywa na wafanyakazi ambao kupitia fursa hii ambayo imejitokeza, kwa sababu tunaelewa watu wetu jinsi walivyo, mishahara yao ni midogo sana. Kwa hivyo, sijui kama watamudu lakini Mhe. Waziri atakapokuja atanambia.

Lakini pia nikiendelea na mchango wangu nichukue fursa hii kumpongeza sana sana sana Waziri wa Fedha na Mipango, kwa sababu ni mara nyingi tulikuwa Waheshimiwa Wajumbe tukilalamika kuhusu ukushanyaji wa mapato yanavovuja. Hivyo, niseme Mhe. Waziri kwa kiasi chake amejitahidi sana kulisimamia hili, lakini pia nimuombe suala zima hili la ukushanyaji wa mapato niseme bado tunahitaji miundombinu zaidi ya kuweza kulifanya likawa zuri zaidi na likaondosha usumbufu kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie hivi sasa ukitaka kwenda kulipa, kupasisha gari au ku-*renew* leseni ni usumbufu mkubwa sana, yaani kutwa nzima wewe siku hiyo uwe huna kazi nyengine tena ya kufanya unakwenda kushughulikia suala hilo. Sasa ni vizuri tukaweza kuweka naomba nipendekeze labda matawi ya benki tunayo mengi kwa sasa, labda tungependekeza tawi moja tukawa tunashughulikia haya masuala yanahusu malipo malipo mengine, ili kuondosha msongamano mkubwa kule ambao unasabisha watu kusababisha watu kupoteza muda mwingi katika kusubiri jambo hili moja, au yale madirisha kama yalivyopendekeza wenzangu yakaengezwa, ili watu wakaweza kulipa huduma hizi kwa haraka ili wakaweza kupata tija wao wenyewe lakini na serikali ikaweza kuingiza mapato kama vile ilivyojipangia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilisema niseme machache katika wizara hii, kwa sababu hii ni wizara mama hii ndio wizara ambayo tegemeo letu sote, wizara zote zinaitegemea wizara hii. Kutokana na hali hiyo, naomba Mwenyezi Mungu amuwezeshe waziri huyu kuyasimamia majukumu yake haya, ili wizara hii iweze kutoa huduma kwa wizara

nyengine, ili Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kujiendesha na kuendelea kunawiri siku hadi siku. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja taarifa hii, na maoni ya kamati naipongeza sana kamati kwa kazi zake nzuri ambazo inampatia ushauri Mhe. Waziri wetu huyu aweze kuendelea na majukumu ahsante Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushuru sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, niwaombe sana mupunguze minong'ono imekuwa ni mikubwa kiasi ile michangio haisikikani naomba sana ili tumpe raha ambaye kuwa anazungumza kieleweke kinachozunguzwa. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini, ili na yeye aweze kutowa mchango wake.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kupata wasaa huu kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo. Naomba nichukuwe fursa hii kwa haraka sana kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa ripoti nzuri aliyotayarisha pamoja na Utekelezaji wa Maagizo waliyoyapata kutoka kwenye kamati.

Vile vile, nampongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati pamoja na kamati yake kwa kazi kubwa sana waliyoifanya kuisimamia Wizara hii ya Fedha na Mipango Mhe. Mwenyekiti ndiyo roho yetu ndiyo yenye mipango ya nchi, ndiyo wenye mfuko wa nchi. Kwa hiyo, mipango yote ya nchi na utekelezaji wake na keki yetu tunamtegemea Dkt. Khalid. Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa utendaji wao na hatuna wasiwasi nao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja zangu ni mbili tu. Hoja ya kwanza ni ya suala la mpira, nimeona Mhe. Waziri kajibu hoja vizuri sana juu ya yake madeni wanayotajiwa *AGROTEX*. Kwa kweli Mhe, Mwenyekiti naipongeza sana wizara kwa kuvunja mkataba na hawa watu. Hawa watu kwa kweli wamekuwa wanatusumbua sana na siku zote niseme ukweli wamekuwa wababaifu tu, hawalipi vibarua, hawalipi huo mpira wanaouza pesa hazipatikani, kodi ya serikali haipatikani. Kwa hiyo, naiomba sana wizara kama alivyosema kwamba watafatilia hili deni, basi namuomba sana Mhe. Waziri awabane hata kuzuia rasilimali zao ili deni letu lipatikane.

Lakini kubwa Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumza ni suala hili la matumizi mbadala ya ardhi ile kama alivyosema Mhe. Waziri hivi sasa upandaji wa mipira pale au suala la mipira tena basi, na huo ni ukweli usiofichika, kwamba ule mpira sasa ile *life span* yake imekwisha, maana yake hata kama utajaribu kuugema basi hata kile kikombe robo hupati kwa mti mmoja, ambapo wakati wake kila kikombe kinajaa chote.

Mwenyekiti wewe mtu wa kilimo unafahamu vizuri na mwenyewe Mhe. Waziri kalelewa kilimo anajua vizuri sana kwa hiyo hivi sasa kuendelea na ule mpira, kwa kweli haina tija ni kuuwacha moja kwa moja. Sasa nimevutika sana na Mhe. Waziri aliposema kwamba serikali inafikiria matumizi mbadala na yenye tija katika mashamba yale.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa rai. Mhe. Mwenyekiti, mashamba yake ya mpira, mipira ile ilipandwa katika *prime area* ya mashamba ya mikarafuu. Mikarafuu iliokuwa mizee ile tuliiwacha tukaikata tukapanda mpira kwa kufikiria wakati ule kwamba mpira ungetusaidia katika sera yetu ya kutafuta zao mbadala la fedha lakini tukaona kumbe duu hakuna zao jengine mbadala pasiwe na mkarafuu. Mhe. Mwenyekiti, rai yangu namshauri sana Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla turudishe mkarafuu katika maeneo yake. *(Makofi)*

Maeneo yale Pemba Maziwani, Konde, Kitope kwa Unguja na Mfenesini ukijumlisha hizi si chini ya eka mia tatu mpaka mia nne za mpira. Hivyo, Mhe. Mwenyekiti kama mashamba yake tunarudisha mikarafuu na maeneo yake mkarafuu unakubali sio utafiti kule, unarudisha mkarafuu moja kwa moja unakubali, wapewe Wizara ya Kilimo wayalee kama mashamba ya serikali nafikiri watauzidi hata mkarafuu wa Makuwe.

Kwa hiyo, nashauri sana Mhe. Mwenyekiti mashamba yale serikali ifikiriye kurejesha mkarafuu. Kwa kweli, kitu rahisi sana cha kuanza *the way forward* cha kuanza unajua mpira unauwa ardhi, lakini pale bahati nzuri sana kuna upupu, umepandwa mule na upupu ule tunasema ni *legume* au mkunde kunde una rutubisha ardhi. Hivyo, kama mkunde upo pale ile mikunde kunde ipo basi iendelee kuwachiwa kuota kwa miaka miwili tu, ile ardhi ijaribu kurudisha *nitrogen level* iliyopo mle, wakati huo huo ile mipira ianze kukatwa kidog kidogo na mikarafuu ipandwe.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema Mhe. Waziri mwenyewe mtaalamu mzuri sana mbali ya fedha, lakini hata kilimo naamini hayo mambo wataisaidia watu wa kilimo watandesha vizuri. Lakini nashauri sana Mhe. Mwenyekiti, mashamba yale tusifanye jambo jengine lolote isipokuwa turudishe mkarafuu na utasaidia sana. *(Makofi)*

Swali langu la mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nalielekeza kwenye *ZIPA*. Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alipofanya ziara katika Mkoa wetu au katika Wilaya yetu ya Magharibi B alipofika Fumba alipata swali la *ZIPA* kutokukabidhi ardhi ambayo wameahidiwa wananchi ni sehemu yao, na akawapa mwezi mmoja tuu watoe jawabu ardhi lile wakamilishe kuwapatiya, upande wa *investment* huku uko mbali lakini upande ule wa pili wakabidhiwe, lakini naona mwezi mmoja umeshapita.

Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili suala la ardhi ya watu wa Fumba ambao serikati imekubali iwakabidhi basi tunaomba sana tuharakishe sisi wawakilishi tunajitahidi sana kuwafahamisha mipango ya serikali wananchi wetu wakubali, lakini naomba pia na yale maombi yao mengine ni ya msingi basi tuyazingatie.

Mhe. Mwenyekiti, kwa maombi yangu mawili hayo naunga mkono hoja na nakushukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji na huyu ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa leo. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kufanya majumuisho.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii kurudia kwa mara nyengine tena kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa miongozi yake anayoendelea kutupatia katika Wizara ya Fedha na Mipango, lakini pia nichukuwe fursa hii kumshukuru sana msaidizi wake Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuongoza katika kazi zetu za kila siku ndani ya Baraza hili lakini pia katika Wizara yetu ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Nichukuwe fursa hii pia kumshukru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara kwa mchango wake na kamati yake yote nzima, lakini nichukuwe fursa pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe walipata nafasi ya kuchangia na hata wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia lakini kwa njia moja au nyengine wameunga mkono hoja ambayo nimeitoa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekti, waliochangia taarifa yangu ni Wajumbe kumi na tatu, waliochangia kwa kusema moja kwa moja ni wajumbe tisa, na waliochangia kwa maandishi ni wajumbe wanne. Naomba kuwatambua wajua hao kama ifutavyo.

Waliochangia kwa kusema ni:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe.Omar Seif Abeid
5. Mhe. Simai Mohammed Said
6. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
7. Mhe. Suleiman Makame Ali
8. Mhe. Panya Ali Abdalla
9. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Shehe Hamad Mattar
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
4. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, nishukuru na kwa niaba ya Wizara ya Fedha na Mipango tupokee pongezi kwa wale wote waliopongeza Wizara ya Fedha pamoja na watendaji wake wote kwa kazi ambayo tunaendelea kuifanya, lakini kazi hii tunaifanya kutokana na miongozo tunayoipata kutoka kwa Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini vile vile juhudi hizi ni kwa mashiriano ambayo tunayapata kutoka Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na kwa wananchi wote kwa ujumla. Kwa hivyo, naomba shukrani hizi na pongezi hizi pia ziwarudie watu wao wote niliowataja kwa sababu kwa njia moja au nyengine wameshangia katika mafanikia ambayo tunaendelea kuyapata katika wizara yetu. *(Makofi)*

Vile vile, nimuhakikishe Mhe. Yussuf Hassan Iddi na kamati yake kwamba jitihada kubwa zitaendea kuchukuliwa katika masuala ya kuhakikisha kodi zinakusanywa kikamilifu. Mhe. Mwenyekiti, nathubutu kusema kwamba hadi sasa tunaende vizuri niwapongeze sana wenzetu wa *TRA* na *ZRB* kwa kazi kubwa sana ambayo wanaendelea kuifanya, naamini kwamba bado iko fursa ya kuongeza mapato, lakini jitihada ambayo wanaendele kuifanya ni jitihada kubwa na inaleta manufaa katika ukusanyaji wa mapato. *(Makofi)*

Mhe. Mwenekiti, naomba nitoe mfano mdogo pamoja na kwamba kima kimeongezeka tulichowaataka *ZRB* na *TRA* wakusanye, lakini kima hichi kinaanza kufikiwa kwa mfano mwezi wa Julai wameweza kukusanya kwa asilimia 96. Lakini Septemba na Oktoba wamekusanya kwa zaidi ya asilimia 100, kwa maana ya mwezi wa Julai, Agosti na Septemba, Oktoba ndio inaendelea kwa zaidi ya asilimia 100. Kwa hivyo, tuko *on truck* na tunamatumaini makubwa sana kwamba kile kima tulichojipangia tunaweza tukakifikia. *(Makofi)*

Ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tuendelee kuwaunga mkono vyombo vyetu hivi *TRA* na *ZRB*, kwa sababu ukusanyaji wa mapato ndio hatua itakayotuwezesha kutekeleza yale mambo ambayo tumejipangia na tumeyapitisha ndani ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima hili la matumizi ya *EFD* limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi, na wakatutaka kwamba tuhakikishe mashine hizi zinaweza zikatumika zinaanza kutumika kwa mara moja. Naomba nieleze kwamba jitihada kubwa imefanya kuihakikisha kwamba mashine hizi zinapatikana kwa wakati, lakini pia nieleze kwamba ugumu wa suala zima wa kuweka mfumo wa *EFD* sijambo rahisi, na hasa suala lenyewe linalohusha ukusanyaji wa mapato ya serikali ni kima kikubwa sana cha fedha ambacho tunakusudia kiwe kinakusanywa kupitia kwenye mtandaoo huo wa ki-*eletronic*.

Kwa hivyo, ni lazima tuchukuwe tahadhari kubwa kwa sababu katika dunia unatengeneza mfumo, lakini wako wenzako wanatengeneza mfumo wa ku-*hack* na hizi fedha za serikali, hivyo tunafanya jitihada kubwa kuona kwamba hatukosei katika hilo. Tulianza na kuhakikisha tunatangaza tenda kumpata *supplier* ambaye anaweza kutusaidi katika uwekezaji wa mfumo huu, zilijitokeza kampuni mbili katika zile kampuni sita ambazo zilikuwa *short-listed* ambayo ni kinyume na Sheria zetu za Manunuzi kwa sababu bila kuwa na *bids* tatu tenda hiyo inaonekana kwamba iko *non repose.* Kutokana na hali hiyo, bado tunaendelea na juhudi ya kuhakikisha kwamba tunatanga upya tenda hiyo, ili tumpate mtu ambaye yuko makini na anaweza akaifanya kazi hii na itakayoweza kufanyika kwa ufanisi ili mbele isituletee matatizo.

Kwa upande wa Mhe. Ali Suleiman Ali na yeye alizungumzia suala la kuongeza mapato na alipongeza sana juhudi za *ZRB* na *TRA* kwa kazi nzuri tunachukua pongezi hizo. Lakini nimuhakikishe pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote waliozungumzia suala la ukusanyaji mapato kwamba *ZRB* na *TRA* itaendelea na *operations* zake za kufuatilia mapato ya serikali, hilo lazima lifanyike, na kwa wale ambao hawana matatizo katika kulipa kodi zao wala hawabuguziwi, hakuna mtu yeyote ambaye atalipa kodi yake kihalali kwa mujibu wa sheria atakayebuguziwa.

Suala la zoezi hili ni kuwatafuta wale ambao wanakwepa kulipa kodi za serikali. Zoezi hilo niseme kwamba litaendelea na wale ambao watajaribu kukwepa kodi basi hatutowaonea haya, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Hivyo, tunawaomba pamoja na taaluma inayoendelea kutolewa tunazidi kuwaomba na kuwanasihi, basi sote tutii sheria ziliopo za nchi na kama kuna vikwanzo, basi ni vyema waje tuzungumze na ufumbuzi utapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tumedhamiria ndani ya mwaka huu wa fedha kuhakikisha tunafanya zoezi zima la kuhakiki mfumo wetu mzima wa ukusanyaji wa mapato. Kwa hivyo, hapa maoni pamoja na fikra zao tunazikaribisha, ili tuhakikishe kwamba tunakuwa na mfumo ulio imara ulio mzuri ambao ulio rahisi kwao pia katika kuhakikisha wana *comply* na sheria za kodi nchini. *(Makofi)*

Lakini pia tutaendelea na suala zima la uthibiti wa misamaha ya kodi, na kuendelea na zoezi zima la kuthibiti magendo hasa magendo ya mafuta ambayo yanaonekana yanashamiri katika nchi yetu na kuikosesha mapato halali serikali.

Sambamba na hilo, pia tumefanya juhudi kubwa ya kuhakikisha kwamba malipo hayaendi mkono kwa mkono na badala yake malipo yote yanapita katika vyombo vyetu vya kibenki. Sasa hili kwa upande mmoja limeleta manufaa ya kuongeza makusanyo yetu lakini kwa upande mwengine limeleta usumbufu kwa sababu ya zile foleni ambazo tunaziona katika vituo vyetu na katika benki zetu. Kwa kweli, kuna hilo tatizo na niwaahidi kwamba tatizo hili tunlielewa na tunalifanyia kazi na tunahakikisha kwamba si muda mrefu sana tutaondokana na tatizo hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo tunaendelea na zoezi la kuhakikisha kwamba tunayagawa maeneo yetu kama ni maeneo ya kodi, kwa maana ya *Block Management System* na ndani ya kuyagawa tunasajili walipa kodi wapya, na kazi hiyo inafanyika na inaendelea kufanyika kama tulivyoahidi wakati nilipowasilisha hotuba ya wizara kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Ali Suleimana Ali alitaka kujua lile tangazao ambalo tumelitoa la watu kusajili vyombo kwa majina yao baada ya kuuziana, tangazo hili limetoka tarehe 4 Oktoba, 2017 na liliwekwa kwamba liwe zoezi la siku thelathini kwa mujibu wa sheria ilivyo hivi sasa. Lakini pamoja na hayo tunaendelea kuchukua hatua ya kuwashajihisha wananchi kusajili vyombo kwa majina yao wenyewe kwasababu ilikuwa ni tabia ya kwamba watu wananua vyombo lakini bado wanabaki na majina yale yale ya yule aliyekimiliki mwanzo.

Sasa hiyo ina hasara mbili, hasara ya kwanza inaikosesha mapato serikali na hivi juzi tumepitisha sheria hapa, Sheria ya *Stamp Duty* juzi tu na inataka kwamba hawa watu walipe kodi zao pale wanapofanya uhaulishaji wa vyombo hivyo. Lakini kwa upande mwengine hata yeye mwenyewe chombo kitakapopata ajali na kama kimekatiwa bima hatostahiki kulipwa yeye, bima hiyo kwa sababu kile chombo kinakuwa bado hakijawa chombo halali kwake. Kwa hiyo, kuna faida kwake pia lakini pia kuna faida na upande wa serikali.

Hivyo, sisi tutaendelea kuwaelimisha, lakini huu muda wa mwezi mmoja sio kwamba ni muda wa kuendesha zoezi hili, nataka kuwashajihisha watu wajisajili kwa sababu hayo ndio matakwa ya kisheria. Lakini bila shaka tutaendelea na zoezi hili hata kama huo mwezi mmoja utavuka bado tutaendelea kuwasajili kwa majina yao halisi wenye vyombo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mwakilishi wa Jimbo la Paje alizungumzia suala la usumbufu wa vyeti vya kuzaliwa, lakini suala hili lilizungumzwa sana na Mhe. Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum alilitolea ufafanuzi wa kina sana. Nimjuilishe kwamba huduma hizi za usajili zipo katika wilaya, wilayani zinapatikana wananchi waende katika Wilaya zao. Kwa kweli, huduma ambapo watu hutakiwa kuja mjini ni wale ambao wanachelewa wenyewe kwenda kusajili. Kwa hivyo, zile *late registration* ndio zinawapasa watu sasa kusafiri kuja huko, kwa hivyo badala ya kuchelewa kujisajili ni vyema utumie fursa yako mapema uende kujisajili katika vituo vilivyoko wilayani.

Mhe. Mwenyekiti, mfumo mzima wa usajili serikali inafikiria kuurekebisha na kuuweka kielektroniki zaidi, ili kurahisisha wananchi kuweza kusajili na hasa huu mfumo utakuwa ni wa usajili wa matukio yote muhimu ya kijamii. Katika kikao hiki Mswada wa Sheria utasomwa kwa mara ya kwanza, kwa hiyo yote hiyo ni katika jitihada za kuhakikisha kwamba tunarahisisha usajili wa yale matukio yote muhimu ikiwemo ya kuzaliwa, lakini vile vile na vifo nayo pia yatarahisishwa kwa utaratibu huu ambao utakuja baada ya kupitisha sheria hiyo ya usajili wa mfumo kwa njia ya kielektoriniki. *(Makofi)*

Suala la mashine za *EFD* tayari nimeshalitolea maelezo, lakini kuna suala la *ZIPA* Mhe. Jaku Hashim Ayoub alilizungumzia la kwamba kuna vibali na hasa alizungumzia kuhusiana na vibali vya ujenzi kuchelewa. Kwa kweli, suala hili hivi sasa linaratibiwa na Kitengo ambacho kinahusika na Maendeleo ya Mipango Miji, kwa maana *the Development Control Unity*, ambapo kitengo hiki kiko chini ya Kamisheni ya Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi *ZIPA* tunashirikiana nao na hivi karibuni tulikuwa na kikao cha pamoja, kikao hicho nilikiongoza mimi mwenyewe baina ya Kamisheni ya Ardhi, lakini vile vile na *ZIPA*. Tukasema kwamba sasa tuweke utaratibu maalum ambao kile Kitengo cha *DSU* kitateua baadhi ya wajumbe, ambao wajumbe hao watakuwa wanafanya kazi kwa karibu sana na *ZIPA*, watakuwepo *ZIPA* ili kuhakikisha kwamba vibali vya ujenzi vinatoka bila ya kuchelewa. *(Makofi)*

Juzi hapa wakati najibu swali nilieleza kwamba tunadhamiria ndani ya kipindi kisichozidi wiki mbili kuhakikisha ule Mfumo wa *One Stop Center* tunauwasilisha serikalini. Kwa hivyo, kazi hiyo nimeichukua na tuhakikisha kwamba tunaifanyia kazi, ili ndani ya muda huo basi tuwe na Mfumo mzima wa *One Stop Center*, na hivi karibuni tumeanzisha Jukwaa la Uwekezaji kama ulivyosema wewe mwenyewe, na bahati nzuri nilipata nafasi ya mimi mwenyewe kuzindua kikao chao cha kwanza. Kwa hiyo, haya mambo yanafanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba wawekezaji wetu wanapata urahisi katika masuala mazima ya uwekezaji na kupata vyeti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Seif Abeid na yeye alizungumzia suala la mapato, alihimiza zaidi suala la taaluma. Nimuhakikishie taaluma itaendelea kutolewa kwa njia mbali mbali kupitia vyombo vyetu vya redio, televisheni, lakini pia na mikutano tutafanya nao, wafanyabiashara pia tutafanya nao mikutano mbali mbali wawekezaji nao tutakutana nao kama tunavyofanya hivi sasa kuwanasihi kwamba tufuate sheria, lakini vile vile maoni na fikra zao tutazichukua kama serikali na tutazizingatia hasa wakati ule tutakapofanya mapitio ya mfumo wa kodi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwanaasha Khamis Juma na yeye alizungumzia kuhusiana na suala la wawakezaji hasa katika sekta ya viwanda. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mjumbe, kwamba sasa serikali mtizamo wake ni kuhakikisha kwamba serikali yetu inatoa mkazo zaidi katika uwekazaji ndani ya sekta ya viwanda. Nakuthibitisha dhamira hiyo tayari Shirika la Uvuvi limeshaundwa na limeundwa na makampuni yetu ya serikali na jitihada zinafanyika za kuhakikisha kwamba basi wanatokea wawekezaji ambao wataingia ubia na chombo kile hasa katika kuendeleza sekta ya viwanda katika suala zima la uvuvi, uvuvi wa bahari kuu, kusindika samaki pia na kuhifadhi samaki hao ili kuweza kutumika ndani na kusafirishwa nje ya nchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika mtizamo huo huo chombo chetu cha *ZSSF* nacho kimepewa jukumu la kuangalia uwezekano wa kuwekeza hasa katika masuala ya viwanda. Na kwa kuanzia *ZSSF* wanajitayarisha kuekeza katika Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo pamoja na yote hayo watashirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kuona maeneo mengine ambayo *ZSSF* itaweza kushiriki katika uwekezaji wenye tija. Hapa nisisitize kwamba uwekezaji wote unaofanywa na *ZSSF* unafanyiwa tathmini ya kina na wananchi wasiwe na wasi wasi, wanachama wa mfuko wasiwe na wasi wasi tunafanya tathmini ya kina na kuona kwamba yale maeneo ambayo kweli yana tija ndio fedha za Mfuko wa *ZSSF* zinaekezwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti, na serikali inafanya hivi kwa sababu inajua dhima iliyonayo, kwa sababu mfuko huu uki-*collapse* dhima yote ya madeni inachukuliwa na serikali. Kwa hivyo, serikali haitokuwa tayari kuona kwamba mfuko huu unakufa, na ndio maana hivi karibuni tumefanya mabadiliko ya sheria baada ya kupata ripoti za tathmini tumefanya mageuzi kuona kwamba mfuko wetu unakuwa *sustainable*, leo unakuwa na faida kwa wanachama lakini pia na wanaokuja watafaidika na mafao yao kupitia chombo hiki muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mashamba ya mipira nilieleza kwenye taarifa yangu kwamba mashamba ya mipira sasa yamerejeshwa katika wizara inayosimamia masuala ya kilimo, na yamerejeshwa huko kwa ajili pia ya kutizama na serikali imesema inaangalia namna bora zaidi ya kuyatumia mashamba hayo. Taarifa itatoka baada ya pale serikali itakapoamua maeneo haya yatatumika kwa ajili gani. Hivi sasa tunaendelea ndani ya serikali kuzingatia kwa kina maeneo yote yaliyokuwa mashamba ya mipira ili yaone yanaweza kutumika kwa kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, pia mkataba na *AGROTEX* nimesema tayari umeshavunjwa rasmi, na hivi sasa kupitia Wizara ya Fedha tunaendelea kuhakikisha kwamba deni walilinalo wenzetu wa *AGROTEX*, basi linapatikana kwa maana zile dola 400,000 kwa sababu

mashamba haya yalikodishwa kwa dola 100,000 kwa kila mwaka. Sasa zile dola 400,000 nazo ziweze kupatikana kwa sababu ni mapato ya serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Simai Mohammed Said alizungumzia masuala ya *PBZ* na misongamano kwa maana hasa wakati wa mwisho wa mwezi kunakuweko na misongamano mikubwa. Nimueleze tu kwamba foleni hizi kama nilivyosema mwanzo zilitokana na hasa kubadilisha mfumo wetu sasa kuwataka walipa kodi wote na wanaolipa ada mbali mbali kulipa moja kwa moja benki, sasa hiyo nayo imesababisha msongamano. Lakini suala zima la ule mfumo wenyewe uliokuwa ukitumika na *PBZ* kwa maana ile *Core Banking System* nayo imezidiwa na wateja, na kuja juhudi kubwa sana inayofanya ya kuhakikisha kwamba system ile inabadilishwa ili iwe na uwezo wa kuchukua wateja wengi zaidi na sio wale waliokuwepo hapo mwanzo ambao wakati mfumo huo unawekwa. Lakini zipo njia nyengine zinatumika za kuongeza *ATM* katika maeneo mbali mbali, pia kuruhusu sasa kuwa na mifumo ya matumizi ya simu za mikononi za kuweza kufanya malipo moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bei ya mafuta alilizungumza Mhe. Simai Mohammed Said na kazungumzia masuala ya ununuzi wa mafuta kwa ujumla kwa maana ya *bulk purchase*. Suala hili linafanyiwa kazi na *ZURA*, *ZURA* ndio mwenye jukumu la ku-*regulate* bei za mafuta. Kwa hiyo, hili suala tuwaachie *ZURA* na wizara inayohusika na suala hili wana wanaweza wakalitolea maelezo zaidi pale itakapo hitajiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na Tume ya Mipango kwamba hakuiona katika ripoti yetu, na hili Mhe. Mwenyekiti niseme tu kwamba tulichojaribu kuelezea hapa ni zile hoja na ushauri uliotolewa na kamati. Kwa kweli yapo mengi ambayo tungeweza kuyazungumza kama tulivyowahi kuyazungumza wakati tulipowasilisha hotuba ya bajeti yetu katika Baraza hili, lakini haya tuliyoyaleta hapa tulikuwa tunajibu au tunatoa maelezo kwa zile hoja na ushauri uliotolewa na Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara. Kwa bahati mbaya sana suala la tume halikuguswa lakini nakubaliana na yeye kwamba suala hili la tume ni muhimu, kwa sababu tume ndio inayopanga mipango ya muda mfupi na muda mrefu ya maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na yeye alizungumzia suala la *ZRB* na polisi kuwakamata watu wenye magari yenye bima *fake*, na akasema kwamba hawa watu hawana makosa. Naomba sana ndugu yangu Mhe. Mjumbe akubaliane na mimi kwamba mtu anayekutwa na bima *fake* na yeye mwenyewe na makosa. Yule anayetengeneza bima *fake* ana makosa lakini na anayekutwa na bima *fake* na yeye ana makosa hivyo hivyo, huwezi kumtoa makosa. Na hata tuna usemi akamatae na ngozi ndiye mwizi, kwa hivyo haepuki hilo. Kwa hivyo, hakutokuwa na utaratibu wowote wa kurejeshewa fedha zao, kwa sababu wana makosa kwa mujibu wa sheria zetu za nchi hii.

Pia alizungumzia suala la benki na akalizungumzia kidogo kwa jazba, kasema kwamba hizi benki zinawazimu, mimi nikashangaa kidogo. Benki haiwezi kuwa na wazimu, na Benki za Biashara zote zilizopo hapa nchini zinafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria, lakini benki hizi zinasimamiwa na Benki Kuu. Benki Kuu ndio *regulator* hawafanyi shughuli zao wana vigezo walivyowekewa na wakienda kinyume na vigezo hivyo benki zinafungwa na ushahidi upo. Kwa hivyo, kuna chombo kizima ambayo ni Benki Kuu

inayozisimamia benki hizi, na benki zote zinafanya kazi kwa maslahi ya nchi na maslahi ya wananchi wake. Kwa hiyo, hilo Mhe. Nadir na Waheshimiwa Wajumbe niwatoe wasi wasi kwamba linafanyika kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la miradi ya maendeleo na matumizi ya fedha na akataka wizara yetu tuhakikishe tunasimamia na hasa kuona thamani ya fedha katika miradi hiyo (*value for money*). Nimuhakikishie kwamba Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ambayo tumeipitisha mwaka 2016 katika Baraza hili, inafanya kazi na nimshukuru sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein hivi karibuni amemteua Kamishna wa Kamisheni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali ya Umma.

Mwanzoni haikuwepo kwa hivyo sasa kuna Kamisheni na Kamishna ameshachaguliwa, na Kamishna huyo sasa anafanya kazi zake chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa kweli, imefanywa hivyo makusudi ili kuwa na uratibu na usimamizi wa masuala yote ya manunuzi katika nchi hii. Kwa hivyo, sisi tutaendelea kuhakikisha ndani ya wizara yetu tunasimamia zoezi zima la manunuzi, lakini kubwa tutaanza na kutoa taaluma kwa wote wanaohusika ili tuhakikishe kwamba wanafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tutaendelea kuhakikisha kwamba tunashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika udhibiti wa mikataba. Mikataba nayo ni sehemu muhimu sana nayo itabidi tuidhibiti lakini Mwanasheria Mkuu anafanya kazi nzuri sana kuhakikisha mikataba yote inayohusika na na masuala ya ununuzi, basi kwanza wanaiangalia kuangalia maslahi ya nchi na maslahi ya taifa letu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, suala la *ZRB* kutotumia nguvu hili nimeshalizungumza na suala la *ZSSF* na nyumba zake nimeshalizungumza kwamba miradi ile inafanywa kwa mujibu wa tathmini inayofanyika kuhakikisha kwamba miradi ile ina tija.

Suala la kwamba wananchi wa aina gani wanaweza kumudu nyumba zile, ziko njia mbali mbali ambazo mtu anaweza kuzipata nyumba zile. Kuna njia moja ya kununua moja kwa moja kama una fedha zako unaweza kununua, lakini kuna njia nyengine unalipa kwa *installment* kukupa unafuu, lakini kuna njia nyengine pia ya kutumia mkopo nayo pia inaweza kutumika ili kukupa fursa ya kuweza kuzimiliki nyumba zile. Kwa hiyo, kama huwezi kulipa moja kwa moja unaweza kutumia njia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini uchumi wetu amezungumzia kwamba akawa na mashaka na uchumi wetu. Nimuhakikishie Mhe. Nadir kwamba uchumi wetu mzuri, unakuwa vizuri. Mwaka 2016 uchumi wetu ulikuwa kwa asilimia 6.8, mwaka huu wa 2017 tunatarajia uchumi utakuwa kwa asilimia 7.1 mpaka 7.2. Lakini mapato yetu yameongezeka kwa zaidi ya asilimia 100 na ndio maana tumeweza kutoka kwenye bajeti ya bilioni kwenda kwenye bajeti ya *trillion*. Hayo ni mafanikio makubwa sana wala tusiyabeze na kuyasahau. Pia tumeweza kudhibiti mfumko wa bei kubakia kwenye tarakimu moja ni mafanikio makubwa sana na tumpongeze sana Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mafanikio haya. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kwamba tunazungumzia suala la uwekezaji bado *FBI* zetu zimeongezeka, kwa hivyo tuko vizuri. Lakini pamoja na kwamba tuko vizuri kuna haja

ya kutia kasi zaidi ili kuhakikisha kwamba tunafanikiwa zaidi. Hivi sasa matumizi ya serikali yetu kwa kiasi kikubwa sana yanatokana na fedha zetu zinazokusanywa kwenye mapato kutokana na vyanzo vyetu vya ndani. Lakini hata utegemezi wetu umepungua kutoka asilimia 12.5 mwaka 2010 na 2011 kuja mpaka asilimia 7.2, ni mafanikio makubwa sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Suleiman Makame Ali alizungumzia suala la huyu mfanyabiashara aliyetakiwa kulipa alisema bilioni 3. Mimi sishangai inawezekana huyu mtu ana malimbikizo ya muda mrefu. Lakini upo utaratibu kama mlipa kodi yeyote yule hakuridhika na kodi aliyopewa na Kamishna wa *ZRB*, basi upo utaratibu wa kisheria wa kukata rufaa. Ipo Bodi ya Rufaa za Kodi tumfahamishe mwekezaji huyo akate rufaa kwenye bodi hiyo, rufaa yake itasikilizwa na kama ana haki basi atapewa haki yake. Kwa hivyo, bado asikate tamaa na kulalamika utaratibu uko wazi kwa walipa kodi wote wasioridhika na kodi wanayopewa na *ZRB* basi wakate rufaa katika Mahakama ya Rufaa za Kodi.

Mhe. Panya Ali Abdalla tunakushukuru sana kwa kupongeza na nirudie tu kusema kwamba Mfuko wa Hifadhi ya Jamii tutahakikisha na utahakikisha kwamba unawekeza katika miradi yenye tija, lakini vile vile tutahakikisha kwamba kodi inakusanywa bila ya usumbufu na pia tutawaelimisha walipa kodi wote wahakikishe wanalipa kodi zao kwa hiari, kwa sababu hicho ndio kitu ambacho tunakilenga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini kuhusu kutaka mashamba ya mipira tuyapande mikarafuu ni wazo tunalichukua na litazingatiwa katika mazingatio ya serikali yanayoendelea ya matumizi mbadala ya mashamba haya ya mipira.

Mhe. Mwenyekiti, pia tutashirikiana na yeye kuhakikisha tunafatilia hayo malalamiko ya wananchi wa Fumba katika maeneo yao. Suala hili nalo tutalichukua kupitia *ZIPA*, ili tuone wananchi wote wanapata haki zao na hawapati usumbufu wowote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitamke kwamba yote mliyotupa, ushauri mliotupa tunauchukua na tutaufanyia kazi na tutashirikiana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini pia tutashirikiana na wananchi wote kuhakikisha jukumu tulilopewa ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango tunalitekeleza kwa ufanisi mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa majumuisho yako. Sasa naomba niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaounga mkono hoja, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Ahsante sana.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza tumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha kufanya shughuli yetu hii jioni hii na tukamaliza kwa vizuri sana, na hatimaye hoja zote mbili leo zimemalizika kwa ukamilifu. Niwashukuru sana na hadi hapo itakuwa ni mwisho wa kikao chetu cha leo nakiakhirisha hadi kesho saa 3:00 asubuhi panapo majaaliwa. Ahsante sana.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 11/10/2017 saa 3:00 asubuhi)